ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim — **Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 25 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka 2011/2012. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 175

Mnara wa Kuongozea Meli (*Signal Tower*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Inaonekana kuwa Mnara wa Kuongozea Meli wa Zanzibar (*Signal Tower*) ni wa muda mrefu sana, na vifaa vyake ni vya zamani; tangu mnara huo ulipoanza kutumika. Aidha, vifaa vinavyotumika kwenye mnara wa kuongozea havikidhi haja katika maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Je, serikali ina mpango gani wa kuupatia vifaa vya kisasa mnara huo au kuweka mnara mpya na wa kisasa?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 175 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Mnara wa kuongozea Meli wa *Signal Tower* uliopo Beit-el-Ajab ni wa zamani na unatumika kwa kazi za kuongezea meli tangu zama hizo na vifaa vyake vimepitwa na wakati, vifaa hivyo ni *SSB* na *VHF*.

Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari tayari imeshaagiza mitambo mipya ya kisasa, kwa matumizi ya mawasiliano ya kuongezea meli inayojulikana "*Global Marine Distress and Safety System" (GMDSS)*. *(Makofi)*

Mitambo hiyo tayari imeshawasili na hivi sasa shirika limo katika utaratibu wa kuifunga *Signal Tower* Unguja na Pemba. Sambamba na kuwasomesha wafanyakazi wa vituo vyote viwili namna ya kuitumia mitambo hiyo.

Mitambo hiyo itakuwa na uwezo wa kuwasiliana na meli zote na vituo vyote Duniani kwa madhumuni ya kuongoza meli, mawasiliano ya kupeana habari ya kiuslama baharini na utabiri wa hali ya hewa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana.

(a) Mhe. Naibu Waziri nakuomba utueleze mitambo hiyo imefika lini? Vile vile lini mitambo hii imeanza kufungwa na lini itamalizika kufungwa?

(b) Mhe. Mwenyekiti, mitambo hiyo, kufungwa Beit-el-Ajab ni sahihi kutokana na uchakavu wa jengo hilo na utahakikisha vipi usalama wa vifaa hivyo?

(c) Kuna mpango gani wa kujenga *Signal Tower* ya kisasa ukilinganisha jengo hilo ni la zamani tokea Zanzibar ilipoanza hadi sasa?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti,

(a) Katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba mitambo hii imefika Zanzibar sio muda mrefu sana. Sasa mitambo hii kufika kwake tumesema kuwa tunaandaa utaratibu wa kuifunga, lakini sambamba na kufanya mafunzo kwa watu wetu, ili kuweza kuitumia baada ya kuifunga na matumizi yale yawe matumizi endelevu, kwa ajili ya kuitumia kwa mnasaba wa kutoa huduma bora, pia uwezekano wa kuishi uwe mrefu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa maana ya Shirika la Bandari wanamiliki mnara tu katika jengo lile. Jengo la Beit-el-Ajab Shirika la Bandari wanaomiliki ni ule mnara na

lile jengo liko chini ya wenzetu wa Idara ya Nyaraka na Mambo ya Kale. Hivyo, napenda kumthibitishia Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu kwamba mnara ule na jengo lile liko salama Shirika la Bandari linashirikiana na wenzetu hawa katika ukarabati wa jengo pale inapobidi kufanya ukarabati huo.

(c) Mpango wa serikali wa kujenga mnara mpya kwa hivi sasa katika eneo la mjini haupo. Mhe. Mwenyekiti, haupo kwa sababu jengo lile la Beit-el-Ajab hivi sasa kwa Zanzibar ndio jengo refu lenye urefu wa karibu mita 40, uwezekano wa kuviona vyombo na uwezekano wa kutumia kwa kipimo cha *height* bado eneo lile na jengo lile linakidhi. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwanza naishukuru sana serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Shirika la Bandari kwa kuleta vifaa vipya ambavyo vitakuwa vinaongozea meli katika nchi. *(Makofi)*

Pili sasa napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kutokana na majibu yake aliyojibu kwamba vifaa hivyo vimeshafika hapa Zanzibar na wanahitaji kutoa mafunzo kwa watendaji wao, ili vifaa hivyo vidumu na vikaae kwa muda mrefu zaidi.

Je, hao watendaji watakaopewa mafunzo watapewa mafunzo hapa ndani ya Zanzibar au nje ya Zanzibar?

Je, vifaa hivyo vimegharimu kiasi gani cha fedha mpaka kufika hapa Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mafunzo yatatolewa kwa wafanyakazi wanaofanyakazi hivi sasa pale Beit-el-Ajab na tutachukua vijana wengine wanne kutoka Pemba na yatatolewa na Chuo cha Mabaharia Dar-es-Salaam. Vile vile wataalamu waliotengeneza chombo hiki nao pia watafika kwa ajili ya kuwapa *practical training* namna ya kuki-*operate*.

Mtambo huu umenunuliwa kwa dola za Kimarekani 68,600 sawa na Tanzania shilingi milioni 101 na umenunuliwa kutoka Afrika ya Kusini. *(Makofi)*

Nam. 223

Ukosefu wa *Air Condition* Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Serikali hivi sasa imo katika maboresho ya Sekta ya Afya ili kutoa huduma bora za afya kwa wananchi. Hata hivyo, katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja kuna tatizo la ukosefu wa vipoza hewa (*air condition*) katika vyumba vya upasuaji.

(a) Je, Mhe. Waziri serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo hili?

(b) Ni vipoza hewa vingapi vinahitajika kwa vyumba vyote vya upasuaji katika hospitali hiyo na vitagharimu kiasi gani?

(c) Je, hali ya joto kali inayotokana na ukosefu wa *air condition* na ukizingatia mfumo wa vyumba vyenyewe haviwezi kuleta madhara kwa madaktari na wagonjwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 122 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wakati walipopita Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Usatawi wa Jamii katika Wizara ya Afya na kutembelea Hospitli ya Mnazimmoja walikuta matatizo ya *air condition*, lakini wa sasa matatizo hayo yapo tena.

Kwa hiyo, nafikiri maswali ambayo nilikuwa nikitaka kuyajibu yatakuwa hayana maana tena, kwa sababu *air conditions* zote zimeshatengenezwa na mazingira ni mazuri na wala hakuna tena usumbufu kwa madaktari wetu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa ajili kuondoa usumbufu katika Chumba hiki cha *Operation* katika Hospitali ya Mnazimmoja.

Kwa hivyo, napenda kumuuliza Mhe. Waziri, kwa sababu amekiri vifaa hivyo tayari vimeshatengenezwa. Je, wametengeneza vile vifaa vibovu au wameingiza vipya?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, vifaa ni *brand new* na wala si mtumba. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Hivi Mhe. Naibu Waziri atakuwa tayari kamati kwenda kuionesha hivyo vifaa? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, rejea swali lako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, namuuliza hivi Mhe. Naibu Waziri atakuwa tayari kamati kwenda kuionesha hivyo vifaa alivyovifunga vipya? *(Makofi)*
Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ruhusa. *(Kicheko/Makofi)*

Nam. 226

Mrundikano wa Wanafunzi Madarasani

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 – Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa asubuhi hii ya leo, namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, ambaye ndiye aliyetuwezesha kuamka katika afya njema, ili kukamilisha mambo ambayo tunayaendesha kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuona kwamba kuna haja ya wizara hii kuendelea, kwa sababu ni kiungo muhimu.

Vile vile nichukue nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana wizara hii, ambayo ni wizara nyeti katika maisha yetu na niwapongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa jinsi walivyokipanga kitabu hiki na kueleza hali halisi ya mwelekeo wa kuleta tija katika maisha ya binadamu. *(Makofi)*

Pia nichukue fursa Mhe. Mwenyekiti, mimi niungane kwa kuwapa pole kwa ndugu yetu marehemu Rahma Moh'd Mshangama, ambaye alikuwa mtendaji mahiri sana katika wizara hii, kwa sababu mimi ndiye niliyeanza naye kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hii. Kwa hivyo, nichukue fursa hii mimi mwenyewe binafsi pamoja na familia yangu kutoa pole kwa wizara hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa niingie kwenye mchango wangu. Kwa kweli tumeingia katika wizara ya nguvu kazi, tena ni wizara ambayo ndio inayoendesha maisha ya jamii katika familia zetu. Kwa nini nikasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu unapomuelimisha mwanamke basi umeelimisha jamii kwa jumla. *(Makofi)*

Kwa kweli kabla sijaendelea nichukue fursa hii niwapongeze wanawake wa Zanzibar wote, kwa jinsi wanavyojituma, wanavyoendelea kulea, yaani wanaanza kumlea mtoto, mwana mpaka baba wa ndani ya nyumba na wala haoni matatizo ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niombe sana wizara ambazo zinagusana na wizara hii na ni Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Mifugo, na Uvuvi, ziwe karibu sana na wizara hii ili kuonekana kwamba yale mambo ambayo akinamama wanajishughulisha nayo, basi waweze kusaidiwa kikamilifu.

Pamoja na hayo, niwaombe akinamama kwa upande mwengine, kwa sababu hivi sasa malezi yetu yamepotea sana, ndio maana tukaona matatizo mengi yanawakumba watoto wetu pamoja na vijana wetu. Kwa hivyo, nitoe wito kwa akinamama tufuate malezi ambayo tumelelewa sisi, ili kuhakikisha vijana pamoja na watoto wetu hawapati matatizo kama ilivyoelezwa kwenye hotuba hii. *(Makofi)*

Vile vile niwaombe akinababa, kwa sababu penye mwanamke kama hapana mwanamme basi hapawezi kufanikisha kitu chochote. Hivyo, niwaombe akinababa kwa moyo mmoja kabisa wawasaidie akinamama pale ambapo wanakuwa na matatizo ya hapa na pale. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tuambizane ukweli, kwamba kumeingia mtindo akinababa kuwatelekeza akinamama pamoja na watoto. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana wizara hii tuchukue tahadhari za kina na mwanamme yeyote kama ni mfanyakazi serikali akimtelekeza mwanamke na watoto. Kwa hivyo, tusikubali lazima tushirikiane kwa pamoja kwamba baba yule anakatwa kima chake cha mshahara, kwa ajili ya kuhudumia mama pamoja na watoto. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaona jinsi akinamama wanavyojihangaisha. Kwa kweli mwanamke wa hivi sasa utamuonea huruma jinsi anavyobeba ndoo au susu la samaki, yaani wanawake siku hizi wanauza samaki, mama lishe. Sasa wewe mwenyewe mwanamme huoni huruma ukaona kwamba anakusaidia malezi katika nyumba, lakini bado unamkandamiza mwanamke yule, ukirudi nyumani wewe mkali kama hujafanyiwa mambo yanayohusu ndani ya nyumba. Hivyo, mwanamke yule atoke asubuhi na afanye kila aina ya mbinu kuhakikisha kwamba bwana mkubwa ukirudi chakula kiko tayari, siku nyengine umeondoka hukumuachia chochote katika nyumba, basi anachoka mwanamke.

Mhe. Mwenyekiti, siku hizi mtindo watu kuoa wanaoa kwa masharti, yaani watatizama huyu mtoto ana nini, anayo kazi, nyumba yake pamoja na kila kitu chake ndio utamuona mtu anapiga hoji kwa ajili ya kutaka kuoa. *(Makofi)*

Kwa kweli anahakikisha atasaidiwa katika nyumba na wala si vibaya kusaidiana, lakini hivi sasa akinababa mtuonee huruma kwamba na sisi tunachoka, kwa sababu kuna mambo ndani ya nyumba mengine ni ya lazima, yaani kuchoka kote usiku ukifika ukielekea kiambazani bwana mkubwa hakubali, kwa kuwa hayo ni ya lazima. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana akinababa kwamba watuonee huruma na wajue kuwa mwanamke ana kazi ngumu.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu vijana wetu. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli vijana wetu hatukuwapatia malezi bora akinamama, ndio maana hivi sasa vijana wengi wanajishughulisha na masuala ya madawa ya kulevya, kuvuta bangi na wengine wanakuwa wavivu hawataki kufanyakazi.

Kutokana na hali hiyo, hapa niwaombe wazee wote wawili, yaani baba na mama, kwa sababu malezi ya mtoto yanahitaji mapenzi ya baba na mama. Mhe. Mwenyekiti, niwaombe walezi wote wawili baba na mama tuweze kudhibiti mambo haya, ili kuwanusuru watoto pamoja na vijana wetu katika mambo ambayo hivi sasa ndio yaliyoingia na hasa kuwanusuru katika janga la UKIMWI. Kwa kweli ni janga ambalo limeingia na wala hatujui tulifanye nini, lakini Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, naishukuru pamoja na kuipongeza sana wizara kwa kuongeza kima cha wazee ambao hawajiwezi. Kwa kweli niseme kwamba Mwenyezi Mungu atawasaidia, kwa sababu unapomsaidia mzee basi ujue kuna kima ambacho Mwenyezi Mungu anakupa.

Sasa kama wangeliacha tu kima kile basi ingekuwa si lolote wala chochote. Lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake na hasa ninavyomjua Mhe. Waziri, yaani Mhe. Zainab Omar Mohammed ni kwamba ni mtu mwenye imani kubwa sana, kweli tunamuona jinsi anavyohangaika na kila siku tunamuona anavyotuelekeza jamani wazee na wala hawezi kukaa wiki kama hajenda kuwatembelea wazee hawa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Waziri na kule Pemba kuwe na jengo kama hili kwa ajili ya kuwanurusu wazee walioko kule. Mhe. Mwenyekiti, najua lipo, lakini lifanyiwe matengenezo makubwa.

Vile vile nichukue nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, kwa kuipongeza tena wizara kwa jinsi walivyokaa na kutafakari kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Kwa hiyo, niwatakie kila la heri na niiombe serikali kwamba itilie mkazo wapate fedha hizi, ili kuhakikisha suala hili linafanyiwa maamuzi ya haraka iwezekanavyo.

Kwa kweli tunawaona baadhi ya watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu, lakini bado hatujakuwa na uwezo wa kuhakikisha, kwamba watoto hawa tuweze kuwaenzi pamoja kuwaweka katika mazingira mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, niishukuru wizara na niombee ipewe fedha na pale ambapo inaonekana kuna kitu kinataka kufanywa kwenye wizara hii, basi nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aweze kumsaidia Mhe. Waziri pamoja na wizara yake yote kwa jumla, ili kuhakikisha kwamba haya ambayo ameyapanga yanatekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba vijana hawa wanaozurura ovyo, basi nitoe tena wito kwa wazee, kwa sababu tunawaona vijana Darajani wanaomba, kwamba hivyo si jambo la busara kuwa wewe mama umekaa nyumbani na kumtuma mtoto awe mwanamke au mwanamme. Kwa kweli hivi sasa umeingia mtindo ambao si mzuri wa kubaka watoto ikiwa mwanamke au mwanamme, niseme Mhe. Mwenyekiti suala la ubakaji na suala la kuwateketeza watoto wetu mimi nasema kuwateketeza chonde kinababa tunakuombeni hili suala limekuwa kubwa na limekuwa sugu, watu wanasema mla kuku wa mwenziwe na wako huliwa. Wewe jifikirie unamchukua mtoto wa mtu mtoto wa miaka mitatu, mtoto wa miaka mitano ambae kwa kweli hakutoshelezi mahitaji yako.

Kuna wajane wamezagaa, nawaomba sana akina baba tuwe na imani na tuwe na huruma maana yake siku hizi imefika mpaka mtu mwanawe anambaka, astaafirullahi Mungu tusamehe, mtoto wake anambaka imani imetutoka. Naiomba serikali kwa nguvu zake zote kwanza hatutaki tuletewe listi ya kesi tunataka ushahidi wa watu ambao wa watu ambao wamekamatwa na ushahidi

kama alivyosema Mhe. Waziri kwenye kitabu chake, kwamba mambo yote yameshawekwa sawa hapo Mnazi Mmoja hospitali, hawa wasionewe huruma kama ni mtu amembaka mtoto amemharibia maisha yake basi na yeye awekwe mahabusu afungiwe kifungo cha miaka 30 au 40. Tusiwe na huruma kwenye suala hili limekuwa sugu hebu tutie adabu ya kuhisi kwamba hii ni adabu ambayo mwengine hatoitarajia kuirudia.

Mhe. Mwenyekiti , tusiwe na huruma katika suala hili naiomba sana serikali kupitia Wizara hii, kwa kweli kuna vijana ambao utawaonea huruma. Halafu jengine kubwa la kusikitisha Mhe. Naibu Mwenyekiti, hata wale walemavu, hata wale wenye taahira jamani kweli Mwenyezi Mungu atakuwa pamoja na wewe wallahi Mwenyezi Mungu hayuko pamoja na wewe na ujue atakulipa hapa hapa duniani. Akhera itakwenda hesabu kwa sababu ni jambo kubwa sana nawaomba sana akina baba na niwaombe waheshimiwa wenzangu katika Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Mwenyekiti, kwamba katika majimbo yetu tuwe macho na watu ambao wanafanya vitendo hivi.

Mhe. Mwenyekiti niwaombe wazee tusifike kwa sababu wewe umeshakula dunia unamfichia mtu maisha yake, wewe umeshakula dunia ndio ukamzaa yule unampotezea maisha yake mtoto wako mwenyewe uliyemzaa, naomba kutoa wito kwa wazazi wote wawili wa baba na mama linapotokea tatizo hili usifiche eleza ukweli unapoficha mungu hayupo pamoja na wewe na unapoficha basi hata wananchi hata serikali haitokuwa pamoja na wewe, naomba sana tena naomba sana wananchi wa Zanzibar tukumbuke tunakotoka nyuma, imani zetu zilikuwa nzuri mimi Mhe. Mwenyekiti samahani nimeolewa mdogo sana na nimekaa na mume hakunigusa mpaka nilipohitajika na nimekaa nae ndani ya nyumba moja, kwa imani yake tu mpaka nilipohitajika.

Mhe. Mwenyekiti, tuwe na imani turudishe imani hii yote ni kwamba imani imetutoka naomba sana hili jambo tuliache na turudishe imani ili kuhakikisha kwamba watoto wetu tunawapa raha ya kuwasomesha, watoto wetu tunawapa raha ya malezi bora, watoto wetu tunakuwa nao pamoja ili kuonyesha mapenzi na wao waweze kuhudumia taifa hili kama ni viongozi wa kesho na leo. Hawa hawa ndio Marais hawa hawa ndio Mawaziri, hawa hawa ndio watendaji wakuu, hawa hawa ndio watu ambao wataliendesha taifa hili wakati sisi hatupo tena, leo tukiwavuruga haitowezekana.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo nichukue tena nafasi hii kuipongeza tena Wizara na niombe tena zile wizara husika za kushirikiana na Wizara hii, zisaidie kama iwezekanavyo ili kuhakikisha wale wazalishaji wakuu wa nchi hii ya Zanzibar wanapatiwa mahitaji yao kwenye vikundi vyao, kwenye ushirika wao, kwenye umoja wao ili kuhakikisha kwamba taifa hili liondokane na umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, naiunga mkono hoja mia juu ya mia na namuombea Mhe. Waziri huyu apewe kila alichokiomba katika wizara hii ili kimuwezeshe yeye na watendaji wake kushughulikia wizara mama, maana hii ni wizara mama. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa siku ya leo kuweza kuchangia na kuitolea baraka Wizara hii Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana asubuhi hii na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Wanawake na Watoto, kwanza nimshukuru Mama yangu pamoja na Makatibu Wake, Wakurugenzi wake na watendaji wake kwa kutuletea kitabu hiki kizuri mauzui yake yamajipanga vizuri sana. Lakini niseme bajeti yao tu ni ndogo kutokana na uzito wa kitabu hiki na hasa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ni pana sana lakini nisema kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Dk. Ali Moh'd Shein alimuona huyu mama akasema kuwa madhali ni mama na katibu wake ni mama basi pamoja na upana wa wizara hii basi itakuwa finyu kutokana na maadili yao, kwa hivyo nimshukuru Mhe. Rais na yeye kumteua mama yangu huyo wala hakukosea kabisa. Siku zote waheshimiwa tunajaribu kuiambia serikali kutokana na uzito wa wizara zenyewe hasa ziangalie kwa hali ya huruma kabisa, kwa sababu wizara hii jamani ndani yake ina mambo mengi sana Mhe. Mwenyekiti, ina wanawake hao tumeambiwa humo, kuna vijana humo, kinababa wamo humo, na wazee wamo humo, leo unampa shilingi tano Mhe. Waziri atafanya vipi kazi zile. Mhe. Waziri hivi kweli ataondoa matatizo sugu kwanye wizara hii ba bajeti hii.

Halafu pamoja na hayo basi Mhe. Waziri na watendaji wake wamejitahidi kuipanga na kuipanga basi angalau hizi fedha tunazosema humu ndani ya kitabu basi angalau tuje kupewa pesa hizi, basi steel hizo watakuwa hawapewi na watafika miaka mitano hawatimizi asilimia ya kupewa pesa hizi, leo tuje kumsema tena mama hapa ukiangalia ukurasa huu wa kwa mfano wa sita, anasema Wizara kipindi cha miaka minne kumi na moja na kumi na tano, kwa mujibu wa mpango mkakati amejipangia kutekeleza malengo makuu yafuatayo. Hayakamiliki si kweli malengo haya atayakamilisha kweli kwa kutimia miaka mitano.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa bado nasumbuka sana te nasana tu kwanza anakwambia anataka kuhakikisha kuwa mapungufu katika sera zinazohusi watoto na wanawake, vijana na wazee yanafanyiwa kazi Mheshimiwa hana vitendea kazi na hana pesa yatafanyika vipi, kwa kumstahi tu mama yangu ningesema bajeti hii kitabu hiki kirejeshwe kina mapungufu mengi sana, kuna

data nyengine humu sio za ukweli wala sio za uhakika na maeneo mengine yaeachwa kabisa yenye matatizo sugu hayakutiwa humu.

Lakini kwa kuwa mama yangu basi kidogo jicho moja nitalifunga hivi kwa kumuhurumia, kwa sababu tukimuangalia jamani hapa katika *paragraph* hiyo hiyo ya sita kifungu cha tano kuangalia na uhalisi wa maendeleo haki zile zenyewe za watoto jamani ni kweli, ukitaka kuombewa masuala haya kwanza uwe na maafisa waliotimia kuanzia ngazi za Wilaya hadi Mkoa mpaka Wizara yenyewe na kuwe na vifanyia kazi hizi *transport* za vihonda na vespa wapewe hapo ndio tutajua tunafanya kazi. Lakini vitu hivi hawana hawa halafu leo hatimae tunakuja kuletewa data humu ndani ya data mnasikitisha sana.

Kwanza humu nikiangalia hata kwenye jimbo langu hamna humu kwenye figa zake Mhe. Waziri, na kule kuna watoto wa hali ngumu sana na watoto sugu, hivi kweli jamani katika kuangalia kwangu nimeangalia angalia hata sijui kama walemavu wametiwa humu na wao ndio wanajumuika na wao humu wizara hii hii, kwa kweli bado Mhe. Waziri hatumtendei haki kabisa hili ukweli tuliseme. Lakini kwa kuwa ameshaleta basi twende.

Mhe. Mwenyekiti, hebu twende ukurasa wa tisa kifungu cha 19 hapo kuna mambo ya kijinsia haya wanayofanywa ndugu zetu na wenetu pamoja na hapa hii naambiwa imejumuishwa wajumbe kutoka wizara zote hizi, Polisi, Afya, Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria hawa tumeweka boshan tu hatuwapi vitendea kazi vitakavyokamilika kufanya kazi zao jamani, ndio yale yale mambo yatakuwa kasoro sheria kule inamtoa mtu.

Mhe. Waziri namuomba hapa akazane kweli na sisi tutampigia debe kuona jinsi gani mapungufu haya ya kitengo chake hiki yatapokuwa hayakamiliki sisi itabidi tupige lele yakamilike, ndipo haya masuala yetu ya ubakaji na mambo mengine yatakapokamilika. Juzi moja Mhe. Jaku Hassan alisema je katika hiki kipimo kinachowekwa umeme ukizimwa si ushahidi unapotea, sawa sawa mimi nakubaliana nae tusiamini umeme wetu huu wa nenda rudi nenda umeme wenyewe wa kuazima huu, lakini kuwe na janareta ambalo litaweza kuokoa ikitokea tatizo hili anawesha janareta lile tunapata umeme vipimo vinapatikana kwa uhakika, kwa sababu hili suala tunategemea wakati wowote kule kutakuwa wazi Mheshimiwa.

Kwa hivyo naomba sana Mheshimiwa kitu cha ziada lazima kiwepo, serikali lazima iangalie upya kuweka fedha ambazo kwa makusudi harambee ya kuchangisha wizara hii fedha zile ziwepo ili kuweza kusaidia na kuokoa na kuondoa matatizo haya, kwa sababu wizara hii imebeba mambo mengi sana ili kuweza kusaidia vijana kwenye ukurasa wa kumi na tano kwenye Ustawi wa Jamii hapo. Waheshimiwa hii ni kweli Ustawi wa Jamii kama tulivyosema

kuna watoto wenye hali ngumu kuna ndugu zetu walemavu. Mhe. Waziri nakushukuru sana juzi kutupa semina, semina ile imetusaidia sana kwa wale ambao tulipata na tuliotoa mchango ule mazingira ya watoto wa hali ngumu hili sio jamba la kulichezea, watoto wetu inapelekea wakafanye vitendo vilivyokuwa havihalisi na maumbile yao kutokana na hali ngumu ya maisha.

Mama yangu hapa aliyekaa aliwatetea sana akina mama lakini saa nyengine kinamama ndio wachokozi hao nipe talaka bwana nipe talaka bwana, sasa haangalii zile taasira zake na dume nalo linataka nafasi hapo linatoa talaka sasa yule bwana akitoa talaka anatoa talaka kwa hasira na watoto wako chukua mwenyewe ee kakataliwa. Sasa tuangalie sehemu zote mbili hizi mimi nakubaliana midume mikorofi lakiini na mama nao wakorofi hii tuangalie sote tusisemane turekebishane. Mheshimiwa watoto tunawatelekeza sote lakini asilimia kubwa niwape na niseme kinababa ndio wanatekeleza watoto hilo nalisema nalo kwa sababu baba ndio mwenye uwezo wa kumsaidia yule mama, tuna ubaya na sisi kinababa wewe damu yako wewe kweli utaitelekeza kwa kuwa yule mama umemuwacha, mimi mtu kama huyo sina imani nae sana tu.

Mhe. Mwenyekiti, damu yako mwenyewe unaitekelekeza mpaka wengine wanafika hadi kuonyeshwa kwenye televisheni mtoto anafika kusema mimi nimefanywa kitendo fulani, hili suala linahudhunisha na inafaa hasa kiongozi mwenye ujasiri hasa basi atoke machozi hapa kwa sababu ni suala ambalo linasikitisha kweli, mtoto unamkuta wa *age* kabisa mwanamme ameshaanza kuharibiwa halafu wewe unajidhatiti mwanangu huyo, mwanao?.

Mhe. Mwenyekiti hili suala sio la mzaha wala sio la wizara hili na waheshimiwa tunatakiwa lazima kwenye maeneo yetu tulishikilie bando hata si hasha tukasema maposho yetu tuyapeleke huko sio vibaya kabisa ndio kusaidia huko sio masihara jamani hili suala linakwenda vibaya sana kwa sababu tegemeo lako mtoto wako upate *strong*. Lakini leo ni hatari hii kwa kweli hili suala mimi nawaunga mkono Wizara hii kwa semina ile nitakuwa nao bega kwa bega, mguu kwa mguu lakini tuhakikishe hilisuala linatokomezwa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani tuachie tu hivi hivi hata siku moja, sasa niingie ukurasa wa 16 katika kifungu cha 36 hapa wanasema Idara ya Ustawi wa Jamii imetekeleza yafuatayo. Wizara inaendelea kutunza watoto katika nyumba ya kulelea watoto Mazizini hadi sasa kituo kina watoto kama hao. Hapa kidogo sina haja ya kumwambia mama yangu kuwa mkali nae naamini mama karithi lakini kurithi kwake kwa hili asilikubali karithi vibaya hili suala, kwa sababu urithi mwengine unakuwa mzuri na mwengine unakuwa mbaya.

Mimi nataka Waziri wangu ukija hapa unieleze watoto wameondolewa kule Forodhani na wakapelekwa katika nyumba ya Mazizini juzi wameingiliwa na

majambazi, hiyo sio taarifa rsmi wameingiliwa hawakuibiwa tu lakini wameingiliwa, lakini hawakuingiliwa ndani ya maumbile wameingiliwa nyumba yao. Siku moja Mhe. Waziri alisema yeye ndio kwanza mpya katika kujibu maswali hili suala yeye bado hajalijua lilivyo, hiyo nyumba ya huko Mazizini akija Mhe. Waziri aniletee hati nasema mapema na Hansard yangu ikae hivyo, aniambie sababu zilizowatoa kule watoto kwenye lile jumba na wakapelekwa kule, isitoshe lile jumba kapewa nani. Naomba nielezwe kwa jina kapewa juma au kapewa nani, lakini la pili kulikuwepo na ndugu zetu walemavu pale chini ndio maana nikasema ni jambo la kusikitisha wakaondolewa masikini ya mungu wale hawaoni wakenda kupelekwa mikokoni kule kweli tunawasaidia hatuwasaidii lengo pale ilikuwa wanafanya kazi zao nzuri tu tena za asiri ya Kizanzibari tumeona wanapata tumeona tuwaondoe tumekwenda kuwapeleka kule hatukuwatendea haki, hili sikulaumu wewe hili wewe umerithi sasa njoo uliseme.

Mawaziri wetu wengi jamani tunakusakameni msikiri tunakusakameni lakini mnarithi tu nyie sasa nyie msifiche tupeni ukweli ulivyo hapa, hakuna hata waziri mmoja aliyekuwa sasa hivi nje aliyeanza kufanya madudu niambieni hakuna mmerithi, sasa nyie wakati mmerithi mkija hapa tuambieni ukweli msifiche. Wananchi wanalalamika kule wanasema mnakula pesa za bure mnavimba matumbo kwa haya sasa leo tunasema, kwa hivyo jamani tunasema hapa Mheshimiwa wangu hansard yangu ikae ziletwe *document* ionyeshwe kama hii hati ya jumba lile wamekabidhiwa serikali, na sababu za kutolewa kula na kuletwa huku nielezwe sababu gani na nani kapewa hilo jumba, kwa nini wale walemavu wakaondoshwa kule wasirejeshwe wenyewe tunataka warejeshwe kule mara moja. *(Makofi)* na njia ifunguliwe.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye maendeleo ya vijana nashukuru sana katika maeneo ambayo saa hivi unadili nayo moja wapo ni hilo pamoja na watendaji wako wakuu, umeona vijana wanapata matatizo na nashukuru juzi tu ulifanikiwa kupewa pesa nyingi tu za kuwasaidia vijana, lakini wasi wasi wangu mmoja tu hapa katika utoaji wa pesa kwanza uwape taaluma. Ndio maana mara nyingi sana watu wanafeli ndio maana hizi pesa za JK na AK hazipatikani kutokana na taaluma haikupewa hawa watunzaji wanaokopa, leo mtu anakwambia nataka pesa nifanye biashara nipeleke kuni Michenzani mmeona wapi watu wa Michenzani wakitumia kuni. Lakini bila ya kutumia taaluma unampa pesa yule unategemea nini atazirejesha kweli kweli kuni ikauzwe Michenzani.

Lakini akikwambia nataka kupeleka biashara Michenzani ya kupeleka Mkaa halali yake mpe yule kwa sababu Michenzani takriban wote wanatumia makaa, sasa taaluma hizo hakuna tunawapa watu fedha tu basi hivi kweli Kitope ukauze ndizi na ndivyo ilivyokuwa hivyo watu wamepewa pesa kiholela holela

bila ya kuwafanyia mafunzo kwanza. Lakini mtu akija mwambie habu tuonyeshe *business* yako iko je, *in come* yake itakuwaje hapa tutafanikiwa. Lakini leo bado vijana wanadhalilika wanakimbilia kwenye mahoteli na huko mahotelini wananyanyaswa yale aliyosema ndio hapa yanapoanzia, ile jinsia yenyewe ya kufanyiwa mambo yaliyokuwa si mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kukwambia kule mahotelini kuna ma- PO Mheshimiwa toto likiwa zuri anapewa kazi mara moja ndio, watu sio masihara sisi wengine tuliokuwa na sura za buti hatupati kazi kwa sababu hatupendwi na mtu hiyo imo, halafu kazi za kitalii mfano kule kuna hoteli ya *GOIN* kuna wanawake wanafanya kazi za Kizanzibari kuwapaka watu piko sasa wanafanya wazungu nenda pale *Kitope Goin* wale pale sasa hivi wazungu kazi ya kupata mwananchi mwenyewe, ndio yale tunayosema mama anasema mimi sitaki uhuni sitaki chochote nafanya kazi yangu tunamlazimisha akafanye uhusi kwa sababu kazi ile mzungu kupaka hina sio yake.

Mhe. Waziri hii nakwambia jua lisitue waambie maafisa wako wende kule wazungu wakawaondoe mara moja waache kazi hiyo, watu wa Kiwengwa wafanya kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo sitaki nipige mengi mama angu lakini kwa hili la watu wa Kitope, Kiwangwa naomba sana watu wa Kumbaurembo kule na Kairo ndio kazi zao ambayo mmewapeleka nyinyi nema ile lakini sio leo ndio kazi zao za kufanywa wao ndio watumwa kukosa ile ajira, hapana Mheshimiwa hiki kitu mimi sikubaliani nacho. Mhe. Waziri maafisa wako ni wazuri sana ni watendaji wazuri kwa hili kama hawana petroli mimi nitatoa pesa, lakini leo waende wakawaondoe wale wazungu mara moja sina mzaha kwa hilo hapana wananchi wanachoka, neema yao wao, nchi yao wao, ardhi yao wao bado wanataka kutawaliwa hapana.

Mhe. Mwenyekiti mimi nimalizie tu kwa kumpa pole mama yangu na kumpa hongera, lakini nimalizie hapa katika idadi ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu yanayotambuliwa Unguja nikiangalia hamna jimbo la Kitope hapa mimi nasema nimekamilika mimi sikukamilika bwana, nina sensa kamili ya jimbo la Kitope watoto wako hali ngumu watoto yatima wenye mazingira magumu tena magumu halisi wewe mwenyewe utasikitika sana ukiwaona.

Lakini kwenye hisabu yako ndio maana nikasema hiki kitabu chako Mheshimiwa kina upungufu kuwa leo imeonekana Unguja na Pemba hata jimbo la Kitope ukubwa wake wote huo hawamo mimi aaa! Hii mimi sikubaliani nae, lakini kwa kuwa ndio kwanza mpya kwa hili nitakusamehe mama yangu, najua ndio kwanza mpya tumo katika hamu ya kufanya kazi hii

leo ukipata kanzu mpya basi una hamu ya kuivaa siku ile ile kwe ile hamu yako ikiwa nzuri au mbaya. Kwa hivyo mama yangu kwa kuwa wizara hii ndio kwanza mpya hapa sikupigi nakuacha kama ulivyo.

Mhe. Mwenyekiti kwa haya machache nijali wakati wako naomba kuunga mkono asilimia mia kwa mia, lakiini nangojea kwenye vifungu ila naungu mkono kwa asilimi sabini tatu nazitia mfukoni nangojea jibu langu la nyumba ile nipewe na hati nisije nikaambiwa hazikuja kwenye *brif case* hapana nataka zije kabisa na nionyeshwe hapo. Kwa hayo machache nashukuru sana ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima na kiweza kufika katika kutekeleza majukumu yetu ambayo tumetumwa na wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa ya kuwapa pole watendaji wote wa wizara kwa kuondokewa na mfanyakazi wao bibi Rahma Mshangama Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi Amin, tujaalie kwamba mbele yake nyuma yetu na si Mwenyezi Mungu atuondoshe katika njia ambayo ameiridhia Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza mimi kwanza nina masikitiko makubwa ya bajeti hii, bajeti ambayo imebeba mzigo wote mzito ni bajeti ya wanawake, watoto, vijana, wazee. Ukitizama gurupu hilo lote ni gurupu ambalo lina mzigo mzito. Lakini ukitizama siku zote ndio bajeti inayopewa makisio dhaifu sana, inaudhaifu wa bajeti yake. Mimi ningeliomba uongekane mzigo mkubwa wa mwanamke. Tumchukue mwanamke peke yake uzigo aliyonao kabla hujatia watoto, vijana, wazee.

Wakati unapofanya harusi ya mtoto wako wa kike gharama zinakuwa kubwa zaidi kuliko mtoto wako wa kiume. Kwa hivyo tujue mwanamke lazima atakuwa na matumizi makubwa. Ningeliomba iangaliwe sana bajeti hii, iangaliwe ili wizara iweze kutekeleza majukumu yake yote ambayo yaliyobeba katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza ukurasa wa 14 katika kitabu cha bajeti kimeelezea kwamba Wizara ililazimika kuhama katika jengo la Mwanakwerekwe na kuhamia jengo lililokuwepo Shangani. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli jengo hili la Shangani haliridhishi, linaufinyu wa kutosha. Kweli wizara ililazimika kuhama pale na sisi kama wanawake tulikuwa tunajivunia kwamba Wizara hii ya Wanawake ina jengo lake zuri pale Kwerekwe.

Lakini kwa hali iliyokuwepo sasa katika ufinyu kama ule uliokuwepo, pamoja na idara zake zote naomba wizara hii onekane kwamba ina shida. Ukiangalia Idara ya Ustawi wa Jamii inawafanyakazi 21, waingie katika jengo lile. Ukiangalia katika Idara ya Wanawake na Watoto ina wafanyakazi 14 na ina vyumba viwili tu. Kwa kweli hii hali ni dhaifu ya kukaa kufanya kazi. Ukiangalia ni lazima pale tuwe na chumba cha Ushauri Nasaha. Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana chumba cha ushauri nasaha. Mimi naomba serikali iyone hali hii ngumu waliyonayo wizara hii.

Mhe. Spika, kuna kitengo cha Hifadhi ya Mtoto kuna wafanyakazi 27 wamo katika jengo hilo hilo. Kuna Idara ya Maendeleo ya Vijana kuna wafanyakazi 17 lakini wamo katika chumba kimoja tu. Kwa hivyo hii hali tuiyone Mheshimiwa. Mimi nadhani kubaki katika jengo lile ni kuwa na udhaifu wa kufanya kazi. Ningeliiyomba serikali iyone, iwasaidie kwa hali yoyote. Kwa hiyo ipo haja ya kupatiwa jengo ambalo litakidhi juu ya kufanyia kazi kwa shughuli ya idara hii.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna suala zima la uhaba wa watendaji, tena watendaji wenye sifa. Kwa hiyo naomba na hili lionekane ni lazima suala hili liangaliwe, ili wapatikane watendaji wenye sifa ambao watashughulikia majukumu watakayopewa. Kwa mfano tukitizama katika hizi idara zetu kiasi gani kuna ukosefu wa wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hali hii tuchukulie hii Idara ya Ustawi wa Jamii. Idara ya Ustawi wa Jamii wana wakosefu wa wafanyakazi ambao wanawahitaji angalau basi wapatiwe. Wapatiwe maafisa wa watoto, mtu wa data base, ningeliomba serikali waone kwamba upungufu wao huu inakuwa tatizo. Kwa sababu kuwakosa wafanyakazi ambao tunawahitaji mimi nina imani kutakuwa na uzorotaji wa shughuli zitakuwa haziendi.

Ukija Idara ya Wanawake na wao wanahitaji wapatiwe maafisa wa mafunzo, wapatiwe watu wa ushauri nasaha. Ningeliomba Mhe. Mwenyekiti, ione serikali mle kwenye mapungufu mwa wafanyakazi ipo haja ya kupatiwa wafanyakazi hawa ili waweze kufanya shughuli zao kwa umakini.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 21. Mhe. Waziri ametueleza kwamba hivi sasa kuna kituo cha Majaribio, *One Stop Center*. Mimi nimpongeze Mhe. Waziri, niipongeze wizara kwa kuona umuhimu wa kuweka kituo hichi ili kurahisisha mambo. Juu ya pongezi hizo zote bila shaka ya wasiwasi tutakuwa nao. Kwa sababu kama alivyosema mama Asha haya mambo yameshatutosha. Kituo hichi naomba Mhe. Waziri ukiangalie kwa makini, huyu mdudu muovu asije akapenya hapa, mdudu muovu hupenya popote. Wakati ibilisi alipenye katika pepo ya Mwenyezi Mungu akenda

akamtoa Sayyidina Adam na Bi Hawaa asije akapenya mdudu wa rushwa. Naomba tuwe makini, ili kituo hiki kiweze kufanya kazi zake kama tulivyoambiwa kwamba ni kituo cha kurahisisha mambo kila kitu kipo hapo hapo, madaktari wapo hapo hapo, polisi wapo hapo. Kwa hivyo kifanya kazi zake kwa umakini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba moja. Unajua lugha zilizokuwa zikitumika nyengine zinatuumiza kwa hawa watoto wetu walioathirika wenye kubakwa. Kwa sababu suala la kubakwa kila siku tukilitizama Mhe. Waziri linaendelea, linakuwa kubwa na sisi tunaathirika. Wazazi tunaweza tukaathirika kisaikolojia wazazi hivi sasa. Ukilinganisha bajeti iliyopita Mhe. Mwenyekiti na ukilinganisha bajeti ya mwaka huu jumla ya vitendo vya ubakaji vimezidi. Inamaana suala la ubakaji kila siku linazidi, halipungui.

Leo lugha iliyokuwa inaniuma katika kichwa changu mtoto wa miaka minne anachukuliwa, anapelekwa kwenda kufanyiwa uchunguzi halafu unaambiwa mtoto huyu mzoefu. Mtoto wa miaka minne anauzoefu? Madokta wetu lugha hizi wasitutumilie wazazi. Mtoto wa miaka ninne hana uzoefu. Mhe. Mwenyekiti, samahani wewe na mimi ni watu wazima kwa suala la kubakwa halina uzoefu. Hata siku moja. Sisi watu wazima, sikwambii mtoto wa miaka ninne. Kwanza mtoto huyu ndio kwanza anaanza nusury, madokta leo wanasema huyu mzoefu. Anakuumiza wewe mzazi. Haiwezikani, lugha hizi nzito kuzitumia. Mtu keshazaa mitoto mitano, hana uwezoefu kwa kubakwa, aridhie mwenyewe tu, lakini sio kwa kubakwa.

Mheshimiwa naomba hili lichukuliwe hadhari kubwa. Pia naomba kutoa maoni yangu kwa wazazi. Wazazi nao ni lazima tujipange kwa watoto wetu. Mtoto wa miaka minne kila siku unampa mwenziwe, kamkoshe huko chooni, wewe mwenyewe humshughulikii wala humjui ana tatizo gani mtoto yule. Mimi naomba kuwaeleza wazazi wenzangu. Ingawa kasema mama Asha kwamba wanawake tuna kazi nyingi kweli, pengine mtu ana watoto watano, sita, saba au wanane wanakusubiri wewe wanataka kuhudumiwa. Baba nae pia anataka kuhudumiwa. Anapokuja baba huwa mkali, kwanza umuhudumie yeye, mtoto wako hujamuhudumia. Hana subira ya kwanza asubiri ashughulikiwe mtoto. Ndio anakwenda mtoto yule kushughulikiwa na mwenziwe mpaka siku unapokuja kumbaini keshaharibiwa ukimpeleka hospitali madaktari wanakwambia kwamba mtoto huyo mzoefu. Kumbe masikini kaumia siku nyingi.

Kwa hivyo naomba wazazi tuache masuala ya kuchukua mtoto ukampa mtoto mwenziwe amshughulikie. Tujaribu kila wakati tuwe karibu nao watoto wetu. Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema mama Asha na wanaume watusaidie ulezi pia ni jukumu lao, mtoto hulelewa na baba na mama.

Mhe. Mwenyekiti, nije hili hili suala la ubakaji ambalo linatuumiza vichwa vyetu. Mimi siku zote huwa nasema. Mheshimiwa alisema katika kitabu chake kwamba mambo yatakuwa mazuri. Lakini tatizo hawa wafanyaji wa vitendo hivi tulionao, ingawa Mhe. Waziri atasema hilo si lake, lakini mimi nasema bado lake. Atashirikiana na wizara husika, hawa wanaofanya vitendo hakuna hukumu zinazochukuliwa.

Ombi langu mbakaji yeyote tunamwita kwa jina la "KITANGI" akeshakuchukuliwa hukumu tunaomba itangazwe kwenye vyombo vya habari, hukumu ile aliyopewa kila mmoja ajue, wengine watahofu. Lakini tatizo ni kwamba kesi inakwenda huko huko, husikii kitu, siku tatu nne unamkuta mtu yupo nje. Kwa kweli tunaumia, wewe kama mzazi unamkuta mtoto yule ndio aliyomdhalilisha mtoto wangu, siku tatu unakumkuta yupo sokoni pale, utajisikia vipi.

Naomba serikali, naiyomba sana lazima Mahakama ziweze kuchukua, kutoa hukumu za wahalifu hawa. Mimi nasema kwa mujibu wa sheria hawa ni watu wa kuuwawa, *Wallahi*, wahalifu. Huwezi kumchukua mtoto wa miaka minne au mitatu ukenda ukamuhiliki. Hivi sasa vimezidi vitendo, kuna *issue* chungumzima zimetokea mitaani Mhe. Mwenyekiti. Kila siku ukicha zinazidi.

Mhe. Waziri kuna kesi mbaya zinazotokea. Kuna kesi imetokea ya kusikitisha ya kuuumiza kichwa. Mtoto wa miezi mitatu kuzaliwa, mama mzazi anaona huyu ni jirani yangu mzuri nikamatie nikaswali. Anamkamata mtoto wa kiume anamtia ndani, aibu kusema Mhe. Mwenyekiti. Anakwenda kumfanya zakari yake ndio kinyonyo anamnyonyesha. Ubaya gani huu? Huu ni uhalifu.

Mimi namuunga mkono Mhe. Mshimba, anasema wanawake wabaya lakini wanaume wamezidi mara 22. Huu ni uhalifu, wanaume wamezidi mara 22. Masuala kama haya yanaumiza. Mama mzazi alipogundua suala lile kwenda kutafuta polisi, yule mtu kakimbia. Alikuwa ni mtu wa Tanga, kenda zake Bara. Hakuna udhibiti wowote, akishakutoka mtu akenda kujificha Bara tu, kesi imekwisha akirudi yamemalizika.

Kuna kesi nyengine imetokea mtoto wa kiume kabakwa. Kesi imekwenda Chwaka imerudi siku mbili tatu mtoto kakimbia, kesi iko Chwaka. Mtoto yule aliyefanya vile karudi anaranda mwanamme, kesho anakuja kubaka tena mwengine. Keshokutwa anachukua anabaka tena mwengine. Hizi ndio hali zilizokuwepo, sio kama kesi hazipelekwi, zinapelekwa. Akiona kesi imemkalia vibaya anakimbia, anakwenda kujificha miezi miwili, mitatu, minne anapiga simu anaulizia, vipi shwari huko? Shwari, anarudi. Akirudi yamekwisha basi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri na waomba wazee, wazazi, Mhe. Waziri wizara yake imesharahisisha mambo, tusiwafiche wahalifu. Tukiendelea kuwaficha wahalifu ndio tunawafuga hawa vitangi mitaani. Tusikubali kutoa hukumu na kumaliziana kienyeji mitaani juu ya masuala haya. Watatuumiza. Mama Asha kamaliza kila kitu hapa, anasema utakapombaka mtoto wa mwenzio na wewe wako akibakwa huumie weye, utaumia. Kwa hivyo tuone kwamba baba zetu, kaka zetu na weo watazaa.

Mtume Muhammad (*SAW*) wakati amekaa na Sayyidina Omar Bin Khatwab na alikaa na Sayyidina Abubakar alimjia kijana mdogo akamwambia Mtume nakuomba unipe idhini nende nikazini. Sayyidina Omar aliinuka akataka kumpiga yule kijana. Mtume akamwambia muache, usimpige. Mtume alimkamata yule kijana kwenye kifua chake, alimuona ushabiki umemjaa mpaka kwenye kifua. Akamuombea dua akisha akamuuliza. Wewe unataka nikupe idhini ukazini je, huna mama wewe? Huna dada? Huna ndugu? Akaamwambiwa ninao. Akamwambia akiziniwa ndugu yako utaona uzuri, akiziniwa mama yako utaona uzuri, akija akiziniwa mwanao utaona uzuri. Akasema sioni uzuri. Akasema basi utakapoziniwa na wewe utaziniwa japo kwenye kipenu chako.

Kwa hivyo haya wayaone, ukapombaka mtoto wa mwenzio na wewe atakapokuja kubakwa utaona utamu. Mimi naomba hukumu za masuala haya yachukuliwe. Niliwahi kusema Baraza lililopita hata juzi Mhe. Spika, alisema. Wahasiwe wanaume wenye kufanya vitendo hivi. Wahasiwe Mhe. Waziri kama hakuna sheria wala hakuna hukumu hii tunasema wanawake. Tena naomba tuwaandalie maandamano hasa ya kupinga suala hili la uzalilishaji na mabango yetu. Wahasiwe tena tuwe tunaona hasa hukumu inatolewa kwenye televisheni, kila mmoja ataogopa kufanya vitendo hivyo, vitapungua vitendo hivi. Vyenginevyo tutaendelea kuumia na watoto wetu, tutaendelea kudhalilishwa watoto wetu.

Hivi juzi kulikuwa kuna kesi Mwembemakumbi kaja mtoto kutembea tu hapa, dakika tano tu, mtoto katafutwa haonekani, katafutwa kwa muda wa siku nne. Kakutwa mtoto akikohowa choo kinamtoka. Kaondoka kenda zake kwao Bara, mtoto kaja kutembea tu hapa, anasema nimeapa Unguja siikanyagi tena. Hali kama hizo zimeshafika Mheshimiwa, kuna mambo haya tunayoyaripoti ni madogo, si kweli data hizi mimi napinga data hizi si kweli. Yapo mambo makubwa yanatokea, mbali ya wazazi wanaowachukua watoto wao waliowazaa. Haya ni mambo ambayo yanatuumisha vichwa sasa hivi. Kwa hivyo naomba serikali iwe makini kwa masuala haya. Pia wazazi tuwe makini, tusikubali watoto wetu kuwaaminisha kwa mtu yeyote.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika Idara ya Vijana. Katika bajeti iliyopita Idara ya Vijana ilijiwekea katika malengo ya utekelezaji moja ni kuunda Baraza la Vijana. Kuwashirikisha vijana katika hatua za kuunda Baraza la Vijana, kitabu hiki kinasema kuendelea na hatua za uundwaji wa Baraza la Vijana Zanzibar. Bado mimi naona Wizara haijawa *serious* mwaka mzima, Baraza halijaundwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba Mhe. Waziri aje atwambie ni lini Baraza hili litaundwa. Ni siku gani au mwaka gani Baraza hili litaundwa, ina maana kila siku kuendelea, kuendelea, yatabakia maandishi ndani ya hichi kitabu. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri aje atueleze siku gani Baraza hili litaundwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ni Wizara ya Wanawake nilitarajia leo Wizara ya Wanawake, Watoto, kuna wazee. Nilitarajia kwamba hapo juu tuwe na watoto na tuwapate wazee wa Sebleni japo wawili haje wakonge nyoyo, tukiwachukua wale wazee tukiwaweka kama hapo wangejisikia vizuri Mheshimiwa. Kwa kweli hawa wazee wetu wa Sebleni ni wazee ambao wapo pale tunawaona kama wazee. Lakini kama tukiwachukua tukiwatoa kuwatembeza tembeza wanajihisi kama wapo Peponi.

Nakuomba Mheshimiwa kupitia kwako ikiwa wewe mwanamke afanye siku Mheshimiwa wazee wale awatoe pamoja na wajumbe wanawake wa Baraza la Wawakilishi. Tukakae nao pamoja tukale nao chakula cha mchana, wajisikie na nao. Wewe jifikirie mzee wako uliyenae nyumbani. Mimi baba angu nikitoka nikinunua njugu basi nikirudi, watoto wananambia shangazi njugu, njugu, basi na baba angu na yeye anataka njugu ale kama mtoto. Mzee kama mtoto na yeye.

Kwanza niipongeze wizara kwa kuona kwamba Shs. 25,000/-hazikidhi haja. Ni kweli kila siku maisha yanapanda, hali inakuwa. Wazee wetu wale wangine angalau wanaweza kusuka makuti lakini wengine hawawezi hata kusuka makuti pale.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mtumwa tunapenda sana mchango wako, lakini umebakisha dakika 2.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Haya *Ishaallah*. Nashukuru kwamba wamezidishiwa Shs. 40,000/- kwa hivyo bado naomba mpango huu uwe endelevu wa kuwazidishia. Wazee wale wapo pale hawana daktari na chumba cha daktari kipo, wakiumwa usiku wazee wale wanafanya nini. Naomba tuwaeke dokta pale wakijawakipata maradhi usiku basi angalau dokta awe yupo pale.

Jengine ni kuhusu wafanyakazi wanaokaa na wale wazee. Kama ninavyosema kukaa na mzee ni kazi. Mzee akiumwa pengine ana maradhi ya tumbo, choo kajieneza, wamshughulikie, achukuliwe apelekwe hospitali. Naomba wafanyakazi hao wapatiwe posho. Kumlea mzee, wako mwenyewe anakazi sikwambii mzee wa mtu. Mzee kumlea ana kazi kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa niaba ya wanawake wa Zanzibar na kwa niaba ya wanawake wote wa Wilaya ya Kati, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi nichangie katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba hii. Amejitahidi sana kueleza yale ambayo Wizara yake ameyafanya na imedhamiria kuyafanya katika kipindi hichi cha mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli leo naona kwa kuwa Wizara hii ni ya wanawake naona wenyewe wamejitutumua. Sasa sisi tutakuwa tunaongezea nyama tu lakini maneno mengi Mheshimiwa Mjumbe aliyepita naona kama amekimaliza hichi kitabu na sisi tutakuwa tunaongezea ili kuiboresha zaidi hotuba ya Mhe. Waziri.

Nianze kwenye ukurasa 15 mimi naanza na Idara ya Ustawi wa Jamii. Mhe. Mwenyekiti, kwenye idara hii ina mambo mengi kabisa. Mimi nianze na kile kituo cha *One Stop Center*. Mimi kwanza niipongeze sana serikali kwa kuanzisha kituo hichi. Kituo hichi kwa kweli malengo yake hasa ni mazuri kabisa. Mimi napongeza sana kwa kuona umuhimu wa yale matatizo ambayo yanapatikana kule na kuamua kufanya kitu kama hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hii itawasaida sana hasa wale waliokuwa wakipata yale matatizo na wala hawajui pakuanzia wala pakwenda au wanapokwenda wakawa wanakosa ule msaada uliokuwa unastahiki wapate wao kutokana na matatizo ambayo walikuwa wanayapata. Mimi niishukuru sana serikali kwa kuanzisha kituo hiki na kwa kweli namuomba sana Mhe. Waziri akiangalie kweli kweli ili yale maudhui yaliyokusudiwa yaweze kupatikana na wananchi wapate manufaa.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii na mimi nizungumze kidogo kuhusu nyumba ya watoto. Mhe. Mwenyekiti, watoto hawa

walikuwa wakikaa kule Forodhani namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuona ipo haja ya kuwabadilishia mazingira na kupata mahali palipo mazuri. Kwa kweli sasa hivi watoto wale wanapokaa ni pahali pazuri zaidi kuliko walipokuwa wakikaa zamani, panapendeza, jengo ni zuri, limepambwa lina mambo yote yanayowahusu watoto yapo pale. Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kama Mhe. Mshimba alivyosema hapa alitaka kujua na mimi pia nataka kujua kwamba Mhe. Waziri atueleze ile dhamira hasa ya serikali kuwaondosha watoto wale katika nyumba inayoimiliki wenyewe serikali ikawapeleka katika nyumba ya *NGO's*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napata wasi wasi kidogo kuwapeleka katika jengo ambalo haliko kwenye milki ya serikali nahisi ni tatizo, maana mwenye jengo lile siku atakayoamua wakati wowote kwamba nataka jengo langu hivyo serikali itafanya nini pale. Lakini ningemuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze hasa kuna mkataba wowote baina ya serikali na mwenye jengo lile, au jengo lile limepewa serikali ili iweze kuwalelea wale watoto na kama imepewa basi atueleze vizuri kama alivyosema Mhe. Mshimba hapa na mimi ningemuomba aje Mhe. Waziri na mikataba au mkataba unaonesha kwamba jengo lile ni mali ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, sisi tunataka tupate ule uhalali wa serikali kulimiliki jengo hili ili ikaweza kuwaweka wale watoto katika jengo lile.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nilikuwa nataka kujua huyu mmiliki wa asili hasa ya kiwanja kile ni wa nani, maana unaweza kujenga jengo lakini kiwanja pia kikawa sio chako. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kujua umiliki hasa wa asili wa kiwanja kile ni wa nani. Mhe. Waziri utakapokuja hapa uje na maelezo hayo yakiwa na vielelezo vyake ili tuone umiliki wa kiwanja kile ni cha nani, jengo lile tunavyoambiwa ni la *NGO's* lakini mimi nahisi hiyo *NGO's* ilikuwa ikiomba misaada kwa ajili ya watoto wale. Kwa hivyo, kama ilikuwa ikitumia jina la watoto wale kuombea halafu *NGO's* ile ndio inamiliki kwa nini lisiwe la wale watoto.

Mhe. Mwenyekiti, atakapokuja Mhe. Waziri naomba unipe maelezo ya kutosha juu ya jambo hili, ili kuwatoa hofu wananchi kuona wale yatima wao wanalelewa pahali palipo salama na hapana matatizo. Mhe. Mwenyekiti, vile vile ningeomba kupata ufafanuzi wa kule ambako umewahamisha wale watoto, lile jengo umempa nani na kwa utaratibu upi maana ile nayo ni mali ya serikali lakini inasemekana kuna watu mmewapa. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kujua kidogo utaratibu gani uliotumika kuhusu hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye jengo la Mhe. Waziri la wizara unalokaa sasa hivi. Mimi nakumbuka ulikuwa na jengo zuri tu kule Mwanakwerekwe. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kujua sababu za kuhama kule ukenda ukajibana

pale ambako hapatoshi, lakini jengo la kule lilikuwa ni kubwa na ulijengewa na wafadhili. Mhe. Waziri kilichokupa uhame pale ni kitu gani ukenda kuhamia kule ambako ni kudogo hakukutoshi kwa mujibu wa maelezo yako, umesema kwa maafisa wako haenei pale. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kujua ni sababu zipi zilizokufanya uhame kule kwenye jengo ambalo umejengewa na wafadhili, wafadhili wamejenga jengo lile kwa sababu ya Wizara ya Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, wameona umuhimu wa wizara hii wakajitolea kujenga, lakini matokeo yake umeiachia Idara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, inaonekana wizara yako labda Wizara ya Kazi ina umuhimu zaidi kuliko wizara yako ukaamua wewe uondoke, sijui kama umeamua mwenyewe au au serikali ndio imeamua kwamba wewe uhame. Kwa hivyo, mimi naomba maelezo kidogo juu ya jambo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee mbele kwenye ukurasa wa 23 kwenye Idara ya Maendeleo ya Vijana. Mhe. Mwenyekiti, utaona tunarejea rejea tunapotoa michango yetu kwa sababu wizara hii haina idara nyingi, idara zenyewe ndio hizo hizo. Kwa hivyo, kila mjumbe atakayekuwa anachangia hapa utamkuta anarejea, Mhe. Mtumwa hapa alipokuwa akichangia alihoji juu ya hili Baraza la Vijana. Mimi nilikuwa nataka kujua Baraza hili hasa litaanzishwa lini kwa sababu kumekuwa na hadithi ndefu juu ya uanzishwaji wa hili Baraza ni muda mrefu sana sasa. Mhe. Mwenyekiti, hata tunapomuuliza maswali hapa Mhe. Waziri basi tunaambiwa kwamba ni hivi karibuni kila siku jawabu ni hiyo hiyo, lakini kwa kweli hiyo karibuni inaonekana haifiki. Kwa hivyo, leo Mhe. Waziri utakapokuja hapa kutoa majumuisho yetu hebu tueleze hasa nia na dhamira ya serikali juu ya jambo hili, ni lini hasa litakuwa tayari.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kuanzishwa kwa Baraza hili kutawasaidia sana vijana katika kujipanga kwenye kujiletea maendeleo. Kwa hivyo, ningekuoma sana Mhe. Waziri utakapokuja utueleze kwenye hili nililolisema. Lakini katika kitabu chako hiki ulieleza juu ya uendelezaji wa vijana, uzalishaji mali kwa kutoa mafunzo ya uzalishaji, uendelezaji wa *SACCOS*, ujasiri amali, uongozi na utunzaji wa mahesabu. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja naomba kidogo utupe takwimu zinazoonesha hizi kazi ambazo ulizifanya katika kipindi hiki cha mwaka uliopita wa fedha ambapo sasa unaomba fedha mpya kwa ajili ya matumizi ambayo umeyaeleza. Kwa hivyo, naomba huku nyuma utupe takwimu zake tujue ni *SACCOS* ngapi za vijana umezianzisha na kuziendeleza zile ambazo zilikuwepo yote ambayo umeyafanya katika sekta hii ya vijana.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ulisema kwamba wizara yako ina mpango wa kukuza ajira kwa vijana katika sekta ya kilimo, biashara na utalii. Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja hapa hebu tupe huu mkakati wa

wizara tuone ni namna gani utawakuza hao vijana katika sekta hizo ambazo umezieleza hapo, utueleze kwa upana kidogo mipango yako hii, ili vijana wetu huko wakusikie na waweze kujua kumbe serikali inao mpango huo na kwa kweli dhamira yake inaonekana kwamba kweli hili jambo litawezekana na kuweza kuwanufaisha wao vijana.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwenye suala hilo hilo la vijana Mhe. Waziri ameelezea juu ya kuimarisha mahusiano na mashirikiano na taasisi za vijana ndani na nje na kuendeleza kambi za vijana hapa Zanzibar. Mimi nilikuwa naomba Mhe. Waziri utakapokuja katika hili hebu tuchanganulie vizuri mahusiano yako na vijana wa mataifa mbali mbali ambao umeshafanya yale matawi ya vijana yaliyokuwepo kule, ushirikiano wako ukoje na mnafanya nini, na mmekubaliana mambo mengine mengine. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tupe kwa upana kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile umezungumzia kambi za vijana. Je, una utaratibu gani katika hili ni tayari umeshazianzisha, au unataka kuzianzisha na utaratibu wake ukoje. Naomba utakapokuja Mhe. Waziri basi utufafanulie vizuri ili vijana wetu nao waishi kwa matumaini kwamba sasa serikali yetu ina jambo hili na katika muda fulani tunaweza kuwa tayari ili wao waingie katika mchakato huo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nisogee mbele kwenye ukurasa wa 30 Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Kwa kweli leo Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kuwa wachangiaji hapa mama zetu leo wamechangamka kweli kweli, na mimi nataka niguse guse tu kidogo ili kuwasaidia katika kulisukuma hili gurudumu letu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka nizungumzie zaidi kwenye hili suala la kubakwa hawa watoto. Mhe. Mwenyekiti, hili tatizo kweli lipo na linasumbua sana jamii yetu, ni kitendo cha kusikitisha sana. Mhe. Mwenyekiti, kibaya zaidi ni kwamba wale ambao wanatendewa wanapokwenda kwenye malalamiko kwa kweli hawapati haki ni mara nyingi sana itakwenda kesi wataanza basi hata hujui inamalizikia vipi mtu anajikuta yule mwenye mtoto wake keshachoka kwenda kusikiliza kule na wala hakuna kinachoendelea, ushahidi hauonekani kila kitu kinapotea. Lakini kwa sababu ya ile *One Stop Center* labda tatizo hili linaweza likapungua.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba bado wizara naiomba sana iwasaidie sana kuwaelimisha wananchi kwa sababu matatizo mengi haya yanayotokea huwa hayafanywi kwa watu wenye uelewa zaidi, mara nyingi sana yanakwenda watu masikini sana au wale wenye kutokuelewa. Kwa hivyo, mtu anashindwa kabisa inawezekana aliyefanya tendo lile mtu mkubwa sana akaogopa hata kusema

kwamba nikasema hapa basi mimi nitakwenda na maji. Mhe. Mwenyekiti, mwisho wake wanarudi wanabaki wanalia tu nyumbani hadithi inakuwa imekwisha.

Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri ukajaribu kutoa elimu zaidi ili uwaelimishe wananchi wafahamu kwamba vitendo hivi vinavyofanyika wasivifiche, wavilete ili serikali iweze kuwasaidia kuhakikisha kwamba wananchi wale walioonewa wanatendewa haki. Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri ukajaribu kutoa elimu kubwa zaidi katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili vile vile nilikuwa nataka nimuombe sana Mhe. Waziri atusaidie kidogo ana kesi ngapi hasa za mambo haya ya ubakaji ambazo ziko kwenye meza yake au ambazo yeye anazifahamu, atueleze takwimu zake katika kesi hizi. Na ngapi katika hili ameshinda na ngapi alishindwa ili tuone ile takwimu ilivyo kwa sababu kama hatukupata hizi tutakuwa tunapiga kelele tu hapa. Kwa hivyo, mimi naomba tupate hizi takwimu ili tuweze kumsaidia Mhe. Waziri huko mitaani kwetu kwa sababu sisi ndio tunaokaa na wananchi, tuweze kuwashajihisha wananchi kama tatizo hili fanyeni kadha na kadha. Kwa hivyo, ikiwa sio hivyo basi wananchi hao watakuwa wanaendelea kulalamika kila siku, lakini hatua hasa huwa hazichukuliwi ipasavyo ni unyonge unaowasumbua.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia malalamiko ambayo Mhe. Mtumwa pale aliyazungumza yanaonesha jinsi gani wale watu wanavyolalamika lakini hakuna kinachoendelea juu ya kesi zile. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri atusaidie hizi takwimu na atuoneshe mkakati wa wizara katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kweli leo sina cha kuzungumza kikubwa juu ya bajeti hii ya Mhe. Waziri isipokuwa yalikuwa ni haya, lakini maelezo ambayo nimemuomba Mhe. Waziri aje atupe yananifanya nisiende mia kwa mia kwenye hii bajeti, niende mpaka sabiini, thalathini nazizuia mpaka nitakapopata maelezo mazuri hasa kwenye hili suala la watoto wanamoishi. Kwa hivyo, nikipata maelezo hayo basi hakuna tatizo lakini kwa sasa nakupa asilimia 70 Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru mchana huu kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri, hotuba ambayo kwa kweli imewagusa wa Zanzibar wote, kama sio mzee mwanamme, mwanamke au mtoto.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa jinsi ambavyo wamejipanga kuendelea kufanya kazi zao ambazo tumewakabidhi kwa ajili ya maslahi ya wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri na pamoja na matatizo mengine ambayo yamo lakini wizara hii chini ya uongozi wake Mhe. Waziri wanaendelea kufanya jitihada kubwa kwa ajili ya kuleta maslahi ya wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii na kabla ya kuendelea niseme kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia, na niwaombe sana wenzangu wajumbe tuunge mkono hoja hii mia kwa mia kwa sababu inawezekana tukataka waziri atujibu lakini kumbe mengine yapo chini ya uwezo wake yako Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, mengine tungeyabakisha tukasubiri Wizara ya Fedha tukahoji kama ile mikataba na masuala ya mali za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kutoa pongezi kwa mradi wa jinsia na niwaombe serikali chini ya Mhe. Waziri waendelee kusimamia dawati la jinsia kila taasisi ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, uamuzi wa kuweka dawati la jinsia kwenye taasisi zetu za serikali ndani ya mashirika, mawizara ni uamuzi muhimu. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri na watendaji wake wasimamie suala hili la jinsia kila penye taasisi ya serikali na ikiwezekana kila penye taasisi za watu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo wenzangu wamelisema ni suala zima la jengo la ofisi ya wizara hii kwa kweli kama mwenzangu alivyozungumza inasikitisha sana kwamba ukifika pale unawaona kwamba wamejipanga kufanya kazi, lakini bahati mbaya hawana maeneo ya kufanya kazi. Mhe. Mwenyekiti, jengo ni dogo sana, lina ufinyu wa ofisi na wengine wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mhe. Mwenyekiti, tusisahau kwamba wenzetu hawa wamehama kule Mwanakwerekwe, walikuwa wana jengo lao kubwa ambalo lingepunguza sana matatizo ya ofisi, lakini hii ni amri ya serikali walipoambiwa kuhama wamehama. Kwa hivyo, nadhani kama kuna watu ambao wangepewa kipaumbele kujengewa ofisi basi hawa wangepewa kipaumbele cha kwanza kwa sababu wao walikuwa na ofisi yao wakahama kwa ajili ya kutii amri ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani serikali ingejaribu kumuona Waziri wa Fedha ningemuomba kwamba wangepewa kipaumbele watu hawa ili wakajengewa ofisi yao ya wizara. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu walikuwa wana ofisi yao wameikabidhi serikali na wamepewa wizara nyengine na sasa wao

wanahangaika wanafanya kazi katika mazingira ambayo kwa kweli hayafurahishi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo ningeligusia ni kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii. Mimi nataka niwapongeze kwamba kwa kweli wanafanyakazi katika mazingira magumu sana, wanafanyakazi kama vile walivyo wazazi, lakini wanafanyakazi katika mazingira ambayo yanasikitisha. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba uwezo wao wa kifedha ni mdogo na jukumu kubwa ambalo kwa kweli bila ya fedha haliwezi kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niwaombe wenzangu Waheshimiwa Wawakilishi kwamba kuna haja miaka ijayo tukijaaliwa tujipange ili tuone kwamba wizara hii ndio wizara ambayo inastahiki kupewa fedha nyingi zaidi, kwa sababu ni wizara ambayo ina lengo maisha ya watu moja kwa moja. Ni wizara ambayo imekusanya wazee, imekusanya wanawake na watoto tena wengine wenye mazingira magumu sana.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii tayari imepita na hatuna namna ya kubaidilisha, lakini nadhani tukijaaliwa mwakani wajumbe wenzangu niwaombe sana kwamba kuna haja ya kuweka msimamo kwa serikali kwamba wizara hii ni miongoni mwa wizara ambazo zinastahiki kupewa kipaumbele kwenye fungu la bajeti kuu ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, tumeona hapa kwamba takwimu za Wilaya mbili tu Wete na Magharibi watoto ambao wana mazingira magumu ni zaidi ya watoto 7000 na wataalamu wanatwambia kwamba kwa Zanzibar watoto wenye mazingira magumu zaidi ni zaidi ya watoto 100,000. Kwa hivyo, hawa hatuwezi kuwafikia kwa bajeti ambayo wenzetu hawa wamepangiwa zaidi ni bajeti ya mshahara na *other charges***,** lakini bajeti ya maendeleo kwa kweli ni ndogo sana. Kwa hivyo, nasema kwamba kuna haja ya wizara hii chini ya idara zote kuweka msimamo kwa serikali kwamba bajeti hizi ziongezwe kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naendelea na msimamo wangu kwamba sioni haja ya mafungu ya Wizara ya Fedha kuwa na fungu kubwa zaidi kuliko mafungu ambayo yanawagusa watu moja kwa moja. Na hii ni hoja yangu nitaendelea nayo mpaka nione kwamba serikali inafahamu kuwa mafungu ambayo yanawagusa watu ndio mafungu ambayo yangeongezewa fedha zaidi kuliko yale mafungu ambayo zaidi yamekusanya safari na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee kuwapongeza serikali chini ya idara hii kwa uamuzi wao wa kuwatoa watoto pale Mazizini, masuala ya nyumba ya Forodhani naamini ni Wizara ya Fedha kwa hivyo hilo Mhe. Waziri atajibu, lakini uamuzi wa kuwapeleka watoto Mazizini kwa ajili ya kupata hifadhi nzuri. Kwa kweli ni uamuzi wa kupongezwa na mimi nachukua nafasi hii

binafsi nimpongeze Mhe. Shadya na *NGO's* yake jinsi alivyoamua kutusaidia kupata jengo lile pamoja na mambo mengine lakini limekidhi mahitaji ya watoto wale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama Mjumbe wa Kamati tumetembelea pale niseme kwamba mazingira ambayo watoto wale wanaishi vitanda ambavyo wanalala basi vinazidi hata ambavyo sisi wengine tunavilalia. Mhe. Mwenyekiti, ni vitanda vyenye viwango na mazingira mazuri na bahati nzuri wanafanya ibada ndani ya majengo yale, wanasoma kur-ani, wanasali mle mle ndani na wanaendelea kuishi kama wa Zanzibar wengine wenye maisha mazuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa niaba yangu binafsi nimelani sana kitendo ambacho juzi wamefanyiwa cha uvamizi wa nyumba ile kwa kweli mimi nakilaani sana na niiombe serikali kuanzia sasa waweke ulinzi pale wa askari wetu polisi. Mhe. Mwenyekiti, pale panahitajika kuwekwa ulinzi masaa 24 kama ambavyo tunaweka ulinzi sehemu nyengine na nyumba ile namuomba sana Mhe. Waziri aombe serikalini kuanzia leo aweze kuweka ulinzi pale kwa ajili ya kulinda maisha ya watoto wetu, na maisha ya wafanyakazi wetu pale.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ilivyo muhalifu haamini kama mle ndani hamna fedha, anaona ile nyumba ni nzuri bila shaka humu ndani mna masanduku ya fedha. Kwa hivyo, nadhani kuanzia sasa Mhe. Waziri nikuombe sana uiombe serikali kuu wakupatie ulinzi pale uwe ni wa kudumu masaa 24 kwa ajili ya kulinda maslahi ya watoto wale na kwa ajili ya kulinda maslahi ya wafanyakazi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningegusia kwenye Idara hii ya Ustawi wa Jamii mimi niwapongeze tu kwamba mbali na kutoa huduma za msingi za malazi na chakula, lakini idara hii pia imesimamia maslahi bora ya elimu kwa watoto wale. Mhe. Mwenyekiti, pale kuna watoto 45 hawa wanapatiwa elimu ya msingi na ya Chuo Kikuu, na mimi nichukue nafasi hii kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwamba kwa kupitia mazingira yale kuna mwanafunzi ambaye yuko Chuo Kikuu na niombe tu kwa heshima ya wizara hii akimaliza kusoma serikali huyu mtoto imuajiri haraka, tenda imuajiri ndani ya wizara hii kwa sababu yeye ndiye anayejua hasa matatizo na mazingira ya watoto ndani ya wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana wizara hii chini ya idara hii ambayo kwa kweli watoto wote pale wanapatiwa elimu tofauti kabisa na watoto wa mitaani ambao wanatembea bila ya kupatiwa elimu. Lakini ndani ya idara hii watoto wote wizara hii inahakikisha inawapatia elimu ya msingi na ya lazima kwa ajili ya maslahi ya watoto wote.

Mhe. Mwenyekiti, jengine lile ambalo ningelisema ni Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto. Mimi nataka nipongeze kwamba kwa kweli sheria tumeipitisha hapa ya mtoto na sheria sasa iko tayari Mhe. Rais anaitia saini. Kwa hivyo, tunaomba sana vyombo vinavyohusika viweze kusimamia sheria ile, lakini sambamba na hilo kama kawaida ofisi hii ya hifadhi ya mtoto kwa kweli haina ofisi ni kitengo ambacho ni muhimu lakini jengo lake ni dogo mno kama ambavyo ofisi nyengine kwenye wizara hii ilivyo. Lakini kamati yangu niwapongeze kwamba wameona haja ya kutoa mafunzo wameshirikiana na *Self the Children* wakatupatia mafunzo kamati nzima, na tumekuwa sasa wataalamu wakujua mazingira magumu ya watoto.

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wangu wa kamati wote wamepatiwa vyeti kwa ajili ya utunzaji wa watoto na hifadhi ya mtoto na hivi karibuni tulikuwa Nungwi siku mbili tumepatiwa mafunzo makubwa na leo nina ufahari kusema kwamba Katibu wangu wa Kamati yuko Kenya kwa wiki tatu kwa ajili ya kupata mafunzo. Mhe. Mwenyekiti, yote hii ni jitihada za wizara hii chini ya idara hizi kwa ajili ya kutoa uelewa kwa wananchi nini mtoto na nini maslahi yake mtoto wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niwaombe tu waendelee kutuelimisha kwa sababu elimu ni muhimu na wengine tunapata kujua kwa ajili ya kulinda maslahi ya mtoto. Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa niseme tu kwamba yote haya ambayo wizara hii inayafanya yangekuwa mazuri zaidi lakini tatizo ni fedha, fedha za wizara hii ni ndogo sana. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia bajeti kuu kati ya bilioni 613 za bajeti ya serikali wenzetu hawa wamepewa bilioni 2.7 ni sawa sawa na asilimia 0.4.

Mhe. Mwenyekiti, asilimia 0.4 ni bajeti ndogo sana kwa maendeleo ya wizara hii na mimi nimekuwa nikisema nimepekua hapa baadhi ya mafungu ya wizara nyengine nimeona kwa mfano Wizara ya Fedha kwenye Idara ya Huduma peke yake imetengewa shilingi bilioni 5, lakini wizara nzima ni bilioni 2 ni 0.4 asilimia ya bajeti nzima. Kwa hivyo, tunategeme wenzetu hawa wafanye nini kwa hivyo nikusema kwamba laiti kama si ujasiri wao kuandika na kuomba basi wangekuwa hawana kazi wanayoifanya zaidi ya kupata mshahara. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, bado narejea hoja yangu kwamba kuna haja ya wawakilishi sasa kuamua, kuwatetea wa Zanzibar kupitia wizara hii, hii ndio wizara ambayo ina watoto, walemavu na ina wazee ambao hawajiwezi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba tumeona kwenye Idara ya Maendeleo ya Vijana kuna mfuko kuwezesha vijana ambao utaendeshwa na *CRDB*, hapa ametwambia Mhe. Waziri kwamba milioni 300 zimetengwa. Nilipoangalia kwenye kiambatanisho hiki Nam. 11 ukurasa wa 39 sijaziona, na fedha ambayo inaingia kwenye serikali ni fedha ya ndani au ya wafadhili ni fedha ya

wananchi. Nadhani ingeandikwa vizuri zaidi ingeleta sura hapa tumeona kuna mishahara, kuna *fees* na kuna milioni 20 tu kwa ajili ya serikali. Lakini ile fedha ambayo pengine wametenga hatukuiona sambamba na hiyo milioni 149 kutoka *UN Habitat* pia hatujaiona kwenye uandishi. Nadhani ingeandikwa humu ingetoa sura halisi ya uandishi wa bajeti kama ni fedha za wahisani, lakini fedha za wananchi. Me. Mwenyekiti, nikuombe tu kwamba hizi Mhe. Waziri angeziingiza kwenye bajeti hii, kwa sababu pia nazo zinahitaji kuombwa ndani ya Baraza ili tuzipitishe.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa niwaombe sana Waumbe wenzangu kwamba hii bajeti tuipitishe na kwa kweli sioni haja ya kupiga buti, kwa sababu unataka kumzuia mtu ambaye hana uwezo, kama vile unakwenda kumkopa maiti sanda ni kumzidisha.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nia yake nzuri lakini fedha haijatengwa. Kwa hivyo hata tumzuie madhali fedha hajapewa atakuwa hana jibu. Mimi nimuombee sana Mhe. Waziri kwa waheshimiwa wenzangu na Mhe. Hamza Hassan sana kwa heshima ya kamanda wenu tuachieni tumsaidie ili aende mbele ahsanteni sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa naomba kwa sababu muda wetu leo tunatarajia kumaliza wizara hii na muda wetu kwa kweli ni mdogo wachangiaji ni wengi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba wakati tunachangia kwanza tusirudie rudie yale ambayo wenzetu tayari nyuma wameshayasema, lakini pia tuhakikishe kwamba muda tunaoutumia usizidi zaidi ya dakika 15 ili sote tupate nafasi ya kuzungumza. Nina hakika kwamba wengi wenu mtaka kuchangia na michango yenu ni thamani kubwa kwa wizara hii. Ahsanteni tunaendelea.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na imi kuchangia Wizara hii ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ambayo imetugusa kila sehemu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niaze kwa vijana. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wizara hii ina wanawake, vijana, wazee na watoto, naomba Mhe. Waziri aone sasa kwamba kuna haja ya kuwashajihisha na kuwapa elimu vijana wetu ili waweze kujiajiri kwa sababu ajira ni ndogo katika nchi yetu, aone sasa kuna kila haja ya kuwatafutia vijana wetu ajira ili kuepukana na matatizo ambayo yanatokea katika mitaa.

Sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, kutokana na nchi yetu ilivyo vijana wengi wanajishughulisha na madawa ya kulevya na kukaba watu ili kupora watu mali zao, yote haya yanatokana na vijana kukosa ajira na sasa kutokana na kuwa

hawana kazi za kufanya ndio wanafanya kazi zile ambazo ni potofu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aone kuwa kuna haja ya wizara yake kubuni mikakati ya kila mbinu ili kuwapatia vijana wetu ajira na kupunguza kasi hii mbaya.

Jengie Mhe. Mwenyekiti, wengi waliozungumza hapa walizungumza suala la ubakaji na mimi nalizungumza kuwa suala hili ni bay asana katika nchi yetu na limekithiri. Kwa hivyo, kuna haja ya kila njia kutafuta dawa ya kulikomesha suala hili.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri siku zote tukitunga sheria basi sheria ni msumeno unagusa pande zote sio upande mmoja tu. Kwa hivyo, wanawake hapa walikuwa wakali sana kwa sababu ya wanaume kuwa wanabaka, lakini na mimi nasema wanawake pia wanabaka na wao wanasababisha watu kubakwa. Kuna ubakaji wa watoto wadogo na wakubwa yote ni hatia, yote ni matatizo, matatizo sio kubaka wadogo tu, hata wakubwa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sheria ikitungwa itizame pande zote kwa sababu wanawake nao wanaweza wakabaka. Siajabu tuangalie huku nyuma yaliyomfika Nabii Yussuf .

Nabii Yussuf alibakwa, Zulekha alimbaka Nabii Yussuf, nabii Yussuf hataki na Zulekha akambaka. Kwa hivyo, lazima sheria ikitungwa itungwe huku na huku, hilo natoka Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ina jukumu la kusimamia wafanyakazi wanaopata ajali makazini. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema sijui niilaumu wizara kuwa haiwashughulikii watu hawa, kuna watu ambao walipata ajali kazini lakini mpaka leo hii hawajalipwa fedha zao, wanadai malipo yao ya fidia ya kupata ajali kazini. Pamoja na kuwa fedha hizi zinazotolewa ni ndogo na inapasa mpaka yule anayeumia kazini atoe tena fedha zake mfukoni kujihudumia, lakini tatizo kubwa ni kwamba umekuwa muda mkubwa walioumia makazini hawajalipwa fedha zao. Tokea mwaka 2007 mpaka leo hii hawajalipwa na mfano ni kwamba, Unguja kuna watu 42 ambao hawajalipwa fedha zao na Pemba kuna watu 20, jumla ni wafanyakazi 62. Sasa namuomba Mhe. Waziri atapokuja hapa anieleze kwa kina ili niridhike ni lini wafanyakazi hawa watalipwa fidia zao ambazo kwa kiasi ni zaidi ya shilingi 73 milioni ambazo zinadaiwa kwa wafanyakazi hawa.

Kila ikija bajeti fedha zinazoingizwa nafikiri kama sikosei ni shilingii milioni tano kwa kipindi hiki zilizotengwa kwa ajili ya watu kuwalipa. Sasa fedha hizo watu hawa tutakwenda mpaka lini ili wamalizwe kulipwa fedha hizo. Namuomba Mhe. Waziri anijibu niridhike na anambie kwamba ni lini bajeti hii ikimaliza kuwa fedha zao watalipwa watu hawa, hapo nitaridhika. Kwa hivyo,

namuomba Mhe. Waziri hili anitafutie jibu zuri si hivyo nitakuwa mkaidi sana kwa suala hili, kwa sababu ni muda mkubwa na fedha hizi zinatiwa kila mwaka shilingi milioni tano hawawezi kuzilipa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ili kulisimamia kw anguvu suala hili na kupatiwa ufumbuzi aje na maelezo ya kina. Kwa sababu toka mwaka 2007 mpaka leo ni muda mkubwa, hivyo Mhe. Waziri anitafutie hoja nzuri ya suala hili.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika kitabu chake amezungumza kwamba kuna wazee ambao wanapata huduma hii ambao wako Sebleni na Pemba Gombani. Pia akazungumza kwamba kuna wazee walioko Welezo. Sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri, jambo la kwanza wazee hawa wanaotunzwa katika nyumba zile za Sebleni wametajwa katika kitabu hiki kuwa ni watu 119, wanaume 65 na wanawake 54. kwanza nasema hawa watu bado ni wachache mno kwa nchi yetu ya Zanzibar kuwa ndio wazee waliomo katika nchi yetu watu 19 serikali kuwapatia huduma hii na kuwatunza ambao wanakaa katika majumba ni kidogo mno. Kwa hivyo, wizara yake ifanye jitihada ya kuwaangalia wale wazee ambao washakuwa wazee kweli na hali zao ni mbaya na waone kuwa kuna haja ya kuongeza huduma kwa wazee hao.

Lakini kitu chengine nataka kumuuliza Mhe. Waziri, hao wazee walioko Welezo amesema hawa wanasaidiwa kwa kupewa chakula, nguo, sabuni pamoja na malazi. Ni vizuri sana, lakini napenda nimuulize Mhe. Waziri kwa sababu wizara yake ina Idara ya Ustawi wa Jamii na inawaangalia wazee wetu, lakini mimi nauliza hivi wale wazee walioko kule Makumbeni ambao ni wagonjwa halafu ni wazee, hivi wizara yake imewaangalia kwa jicho gani la huruma wazee wale. Kwa sababu ni wazee ambao wametelekezwa kwa muda mrefu sana, sasa hivi apite Muisilamu anaye imani ende akawasaidie wazee wale, wazee ambao ukiwaangalia wewe mwenyewe kama una kitu mfukoni utakitoa kwa hiari yako, ni wazee hawajiwezi halafu ni wagonjwa Mwenyezi Mungu kawakirimu ugonjwa wanastahili kusaidiwa.

Kwa bahati mbaya wazee hawa walikuwa wakitunzwa, kulikuwa na hospitali yao, walikuwa na majengo yao, lakini kwa bahati mbaya majengo yale sasa hivi yameporomoka mengi na hospitali ile haipo, huduma hii serikali haiwasaidii tena. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze kama je wale wazee walioko Makumbeni wamejipanga vipi wizara yake kuwasaidia na je anawasaidia vipi wazee hawa, na wizara yake imejipanga kuwasaidia vipi wazee hawa? Kwa sababu ni wazee ambao walikuwa wakijulikana lakini sasa hivi wametelekezwa kwa muda mrefu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atapokuja na hili nalo anipe majibu.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, ni suala la ajira ya utotoni. Mhe. Mwenyekiti, kwanza Wilaya yangu ya Micheweni imetajwa kwamba nayo ni moja ambayo inatoa ajira kwa watoto wadogo. Suala hili mimi kwanza nikiri kuwa ni kweli, siwezi nikasema si kweli ni kweli, lakini Mhe. Mwenyekiti, watoto wanaofanya hivyo hawafanyi kwa makusudi au kwa hiari zao imebidi wafanye kwa lazima kutokana na hali za maisha ya wazee wao ilivyo. Kwa hivyo kutokana na wazee wao walivyo, watoto wanasababishwa kupata ajira wenyewe kwa sababu mtoto akiona kuna siku moja au mbili hajapata chakula basi lazima siku ya pili atoke aende akatafute cha kudaka mdomoni.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kuiangalia Wilaya ya Micheweni kuona kama kuna watoto wenye hali ngumu za maisha basi na hii kama tunavyosema kuwa Wilaya ya Micheweni ni moja katika sehemu ambayo ina hali ngumu ya kimaisha aone basi kuwa kuna haja ya kuimarisha kila msaada, kila kikundi cha hao vijana au watoto wa wazee kuwasaidia ajira ili watoto kuepukana na jaira za utotoni. Kwa sababu wanafanya ka ulazima si hiari yao.

Nimuombe Mhe. Waziri katika wizara yake hii ya Wanawake na Watoto kuona kuwa kuna kila haja ya kuwasaidia watoto walioko katika Wilaya ya Micheweni katika hali ngumu hii ya maisha.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine unaweza ukafanya kosa si kwa hiari yako inakuwa kama ni lazima. Kwa hivyo, ili kuwaepusha waoto wetu na ajira za utotoni namuomba Mhe. Waziri kwanza aiangalie hii wilaya na awasaidie wazee wao kwanza kwa elimu wapewe elimu pamoja na kwamba imeshatolewa, lakini aandae elimu ya kutoa kwa wazee, semina ili kuwaelimisha wazee kama kuna haja ya kuepukana na watoto hawa kuwapa ajira wakiwa watoto wadogo.

Jengine ni kutoa kipaumbele cha kuwasaidia wazee na vijana kubuni mbinu za kuwasaidia wazee ili waepukane na hizi ajira za watoto wao wadogo. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aone kwamba kuna haja ya kufanya hivyo ili kusaidia watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naomba nimalizie hapo kwa muda huu, namuomba Mhe. Waziri anitafutie majibu ya hoja zangu hizo na akishanipa majibu nikiridhika basi nitaunga mkono hotuba hii kwa asilimia zote, lakini baada ya kupata majibu ambayo yataniridhisha. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri. Kwanza kabisa

napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuchaguliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar kuwa waziri wa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kuwa nina masikitiko makubwa sana kwa ufinyu wa bajeti hii, bajeti hii ni finyu wakati bajeti yenyewe imebeba vijanam watoto pamoja na kinamama. Mimi nasema bajeti hii inategemea zaidi wahisani kuliko serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Kazi za Maendeleo kwa Vijana. Idara ya Vijana kazi za maendeleo wamepewa shilingi 20 milioni, hivi kweli Mhe. Mwenyekiti, milioni ishirini zinaweza zikaleta maendeleo kwa vijana?

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile sasa Zanzibar tumeshapata kituo maalum kinachushughulikia udhalilishaji wa watoto Zanzibar, mimi ushauri wangu niwaombe wananchi waache kufanya suluhu nyumbani. Kwa sababu watakapofanya suluhu nyumbani ushahidi wote huwa unapotea na hili tatizo la udhalilishaji huwa linaendelea siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hivi karibuni tulipitisha sheria zinazowadhalilisha watoto, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mwanasheria Mkuu sheria hizi azilinde na mswada huu tuliopitisha aulinde. Zinapotolewa huku na zinapopelekwa kesi kwenye kituo hiki cha mkono kwa mkono basi Mhe. Mwenyekiti, kesi hizi zifuatiliwe mpaka upatikane ufumbuzi.

Kwenye bajeti hii tumeona kuna Ofisi Kuu Pemba, Ofisi Kuu Pemba walisema wanataka kukodi jengo lakini kwenye bajeti hii hatukuona sisi pesa ambazo zitakodiwa hilo jengo. Siku zote huwa tunalalamika kina baba ndio wanaosababisha matatizo, lakini na sisi kinamama tunasababisha matatizo. Kwa sababu kinamama mtu anachukua ujauzito, ujauzito ule anailewa mamba mpaka anafikia miezi tisa, unapofika miezi tisa unakwenda kujifungua vichochotoni, unapojifungua vichochoroni mtoto yule aidha unamuua kwa kumtumbukiza kwenye choo au unamtupa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, na hawa kinamama ambao wanafanya mambo haya nimuombe Mhe. Waziri kama atathibitisha aliyefanya tatizo hili ni mama fulani akamatwe, apelekwe kwenye vyombo vya sheria baadae sheria ichukue hukumu nzito. Kwa sababu mtoto hana kosa mwenye kosa ni yule mzazi, kwa nini wewe mama huna shida ya kuzaa ukenda ukatafuta mwanamme akakupa ujauzito baadae mtoto yule ukamtupa? Inauma sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Vijana. Idara hii Mhe. Mwenyekiti, ina chumba kimoja cha wafanyakazi na wafanayakazi ni 17 nao vile vile wanahitaji kushughulikiwa vijana hao kwa sababu wanakwenda pale na matatizo yao.

Nataka niiombe serikali watafute jengo lka kuwaweka vijana hawa au kiwanja wawajengee wizara hii ya Ustawi wa Jamii, kwani wizara hii imekwenda kutupwa kule walikowekwa. Ni kwa nini hasa Mhe, Mwenyekiti, jengo lile la Ustawi wa Jamii likachukuliwa na tokea zamani jengo lile ni la Ustawi wa Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mkosefu wa fadhila kama nitakuwa sijawatetea vijana wangu. Hivi karibuni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipokuja kufungua Baraza lake hili tukufu aliahidi kuweka Baraza Kuu la Vijana Zanzibar. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi unakaribia mwaka mpaka leo hii hatujaona habari yoyote ya maandalizi. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atapokuja hapa anieleze ni kwa nini mpaka leo hii Baraza la Vijana Taifa linasuasua.

Mwisho naomba niishie hapo kwa niaba ya vijana wenzangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Vijana wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla naunga mkono hotuba hii.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Kwanza nitangulize shukurani zangu za dhati kumshukuru yeye Mhe. Waziri kwa kuwasilisha bajeti yake hapa mbele ya Baraza lako tukufu kwa vizuri sana. Pia niwashukuru watendaji wake kwa kumuandalia bajeti hii kuileta hapa mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nitoe mkono wa rambarambi kwa wazee na familia ya marehemu aliyekuwa Katibu Mkuu wa wizara hii Ndugu Rahma Mshangama. Vile vile nimpongeze Katibu Mkuu mpya sasa hivi Ndugu Fatma Moh'd Gharib. Kwa kweli lile pengo tungesema kwamba halitozibika ingawaje mwenzetu tumempoteza lakini tumepata mwanamke mwengine mwenye hisia na imani kabisa pamoja na uwezo wa kuendesha wizara hii. Nimpongeze Mheshimiwa kwa kupata nafasi hii.

Kama walivyoendelea wenzangu kuipongeza wizara hii lakini vile vile niseme kwamba kutokana na majukumu mengi ya wizara hii iliyokuwanayo na mipangilio yake mingi wizara hii ni kwamba bajeti yake bado haitoshelezi kama ilivyojiwekea malengo yake mengi katika kitabu hiki.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, umuhimu wa wazee, vijana pamoja na akinamama na malengo yetu ni kuwakwamua vijana na kinamama. Kuna mikakati mingi ambayo amejiwekea Mhe. Waziri lakini ikiwa bajeti hii ni ndogo kiasi hicho mambo mengi yatamuwia vigumu kuyafanya.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu walizungumzia kuhusu hii *One Stop Center*. Kwa kweli hiki kituo nakiomba kiwe endelevu kisiwe kwamba baada ya muda kikasambaratika, na yote haya ndio kama hayo niliyosema kwamba inazingatia bajeti. Kwa sababu hapa panatakiwa mambo mengi na hasa pale vinapotokea vile vitendo kutakuwa na ufuatiliaji wao wenyewe hawa kama kituo kitakuwa na mambo yake mengi ambayo kinataka kuyafanya. Kituo hiki ni kizuri kuwepo kwa pamoja, watu wanafanya kazi zao kwa pamoja linapotokea lile tendo ambalo la udhalilishaji wa watoto wetu.

Vile vile nichukue fursa hii kuwaambia wazee wenzangu kwamba sasa tubadilike haya matatizo yapo kwa wale ambao hawana hisia au ni upotofu kumchukua mtoto mdogo kabisa aliyekuwa hajawa na uwezo wa kufanya tendo lile ukamchukua kumfanyisha kitendo kile kwa nguvu na baadae kumletea maumivu makali. Kwa kweli lazima paandaliwe sheria ngumu na nzito, mtu atakapotokea kafanya jambo hili basi na yeye kama walivyosema wenzangu kama ni mwanamme na akili zake hasa basi afanyiwe uchunguzi kwanza na kujua kweli huyu na tendo lile alilolifanya ana akili timamu? Kama ana akili timamu basi na yeye kama alivyomuumiza mtoto yule na yeye apewe adhabu ya kuumiza.

Hivi sasa tubadilike kulea watoto wetu, kuna tabia ya kukaa na watoto wadogo na kusema maneno ya ovyo ovyo tu, hii kwa kweli sio utamaduni wetu. Watu wazima kukaa na watoto ni kweli unamharibu mtoto kisaikolojia, kutakuwa na maneno mengi unasema ya kijitukizima ambayo mtoto hayamfai. Kwa hivyo, lazima tubadilike na mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na wizara hii kama walivyosema wenzangu kwamba wizara hii pale ilipo sasa hivi hapastahiki hata kiafya. Kwa sababu watu 17, 21 au zaidi ya hapo ni kweli kwamba kiafya haikubaliki hasa ukizingatia kuwa walikuwa na jengo lao ambalo lilikuwa na nafasi tu, pana, zuri wenyewe walikuwa wanaenea, lakini leo kuchukuliwa jengo lile kwa kweli pana mapungufu tena makubwa sana na hasa tukizingatia pale walipokuwepo tutakuwa tumefadhiliwa, tumepata ufadhili, leo anakuja mfadhili wetu mahala pale anatafutwa Mhe. Waziri ambaye ni mama na ambaye kafadhiliwa sijui wafadhili wale watatuonaje. Tutafute wafadhili wengine kama hatuna ofisi basi watusaidie kwengine, lakini kuwaondoa kinamama wale pale walipokuwepo hili ni tatizo kubwa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea ni kwamba suala jengine ni la uhaba wa wafanyakazi. Uhaba wa wafanyakazi na hasa hawa wa ushauri nasaha, tunaomba wizara au serikali kutokana na *skills* za hawa watu kwa vile hapa pana ushauri nasaha panatakiwa watu ambao wana *skill* ile. Kwa hivyo, vile

vile tunaomba kwamba serikali kwa jitihada zote kupatikane hawa watu wenye elimu ya ushauri nasaha.

Pia maposho ya wafanyakazi kwa ajili ya usafiri. Hili ni tatizo na jana nililizungumza hapa kwamba ni jambo muhimu na unamjengea imani yule mfanyakazi, ikiwa hakuna posho la safari kusema kweli inakuwa ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu muda wako hauruhusu umeshatwambia kwamba kidogo turejeshe chini, basi Mhe. Mwenyekiti, na mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, kwa kweli wanawake ni mama zetu, wanawake ni wake zetu, wanawake ni watoto wetu, wanawake wana mzigo mzito sana kama ilivyoelezwa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, akinamama bado wataendelea kuwa na mzigo mzito na majukumu makubwa kwa watoto. Kwa sababu wao ndio walio karibu na watoto masaa 24 kuliko baba.

Mhe. Mwenyekiti, tukizungumzia habari ya mama na watoto hili ni jambo jema. Lakini pia akina mama tunaomba wasiwe dhaifu sana kwa watoto wetu kwa sababu wao ndio walezi, wasiwape fursa watoto zilizokuwa si nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, unyanyasaji wa watoto kijinsia ni jambo baya sana na mpaka leo hii linaendelea kwa nguvu zote juu ya kwamba linakemewa. Mhe. Mwenyekiti, unyanyasaji na ubakaji wa watoto ni jambo lililowekewa sheria lakini linatushangaza kila siku tunasikia katika vyombo vya habari mtoto wa umri wa miaka mitatu au minne wamebakwa au wamenajisiwa. Lakini hatuoni ni kesi ngapi zilizohukumiwa katika vitendo hivi, sijui kesi hizi zinaishia wapi ni jambo la kushangaza.

Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Waziri alichukulie hatua jambo hili kwa kina kwa sababu sio jambo la mchezo. Kila mtu amezaa na kila mtu mtoto wake hakubali kudhalilishwa, kama hakubali kudhalilishwa tunaomba jambo hili lisiendelee. Sheria zipo na tunaomba ziwe na usimamizi mzuri. Kwa sababu sheria kama haina usimamizi mzuri basi haiwezi kupita, lakini sheria kama itasimamiwa kwa kila mtu akajua kama mimi nikifanya kosa hili adhabu yangu ni hii atajikinga na mambo ya utovu wa nidhamu kama huo.

Mhe. Mwenyekiti, katika vijiji vyetu tunamuomba Mhe. Waziri navyo kuna matatizo makubwa. Kuna watoto ambao wametelekezwa na kuna wazee ambao hawajiwezi hawana huduma. Tunamuomba Mhe. Waziri asitembelee mijini tu aende na vijijini aangalie hali kuna watoto mayatima kule hawana wahudumu. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri siku moja ajaribu kuvuka kisiwa cha Kojani wapo walemavu, wapo wazee wasiojiweza na watoto walio katika mazingira magumu.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie Idara ya Maendeleo ya Vijana. Mhe. Mwenyekiti, idara hii imejipanga vizuri sana katika kuwaendeleza vijana katika mambo mema. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia mitaani kwetu huko vijana wetu wameathirika sana kwa mambo ya uvutaji bangi na uvutaji wa unga. Ni muhimu sana jambo hili lichukuliwe hatua za kisheria pamoja na kwamba sheria zipo lakini watu hawa wanakuwa wanarejea katika hali ya kawaida. Namuomba Mhe. Waziri aliangalie kwa kina suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, akina mama huwa wanawapa uhuru sana watoto, kwa hivyo tunaomba watoto wadhibitiwe sana kwa sababu wanatumika katika vitendo viovu. Kama tutawadhibiti na kuwaelekeza katika njia njema kama kuwashajihisha katika vyuo na kuwalea katika malezi mazuri basi tutaepukana na kufanyiwa vitendo vichafu. Lakini wakati mwengine tunawapa uhuru uliokuwa si haki yao hili ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, katika hali hii ya vijana wetu hawa imeandaliwa vizuri sana lakini bado vijana wanajitumbukiza katika wimbi la maovu. Kwa hivyo, tunaomba suala hili lizingatiwe na wapewe elimu ya kutosha, bila ya elimu itakuwa hawajui wanachokifanya. Tukiwapa elimu, tukiwapa vitendea kazi basi *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu majanga haya yatapungua.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wachangiaji ni wengi mchango wangu niishie hapo. Mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kojani naiunga mkono hotuba hii mia juu ya mia.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, kwa leo sina mchango mkubwa isipokuwa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha wakati huu kuweza kuchangia bajeti hii ili kutoa nafasi ya kuwachangia wazee, watoto, pamoja na vijana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa leo sina zaidi isipokuwa nichangie ukurasa wa 18 kuhusu wazee wetu ambao hivi sasa tunawatunza hapo Sebleni. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza serikali kwa mchango mkubwa wa kuwatunza wazee

wa Sebleni. Nashukuru sana kwamba wapo katika hatua nzuri na malezi bora ya kupigiwa mfano.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba kuwatunza wazee wa Mkoa wa Mjini Magharibi tu kwa kweli hatujafikia lengo zuri. Lengo zuri ni kuhakikisha kwamba kila mkoa na wilaya tunakuwa na majengo ya wazee na tunawatunza kama ipasavyo. Kama tutafikia lengo hili ni wazi kwamba tutawatunza wazee wetu.

Mhe. Mwenyekiti, malipo ya wazee kwa kiwango kilichotajwa katika kitabu hiki ni kidogo sana kwa hivi sasa kutokana na hali ya maisha. Ukitazama katika mikoa na wilaya zetu hivi sasa kuna wazee wanalipwa mshahara kama huu wa kuwatunza wazee lakini utasikitika sana kwamba mzee anakaa miezi mitatu hapati hata mchango mdogo. Akilipwa mchango wenyewe hauzidi kwenye shilingi elfu tano tofauti na kiwango ambacho kimetajwa katika bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba suala hili linazingatiwa na wazee wanatunzwa kiasi ambacho sawa sawa na Mkoa wa Mjini Magharibi. Isiwe kila kitu kinafikia Mkoa wa Mjini lakini Mikoa ya Kusini au Wilaya ya Kati na Majimbo yake wazee wanasikitika. Hivyo, tunapata dhambi sana serikali itakuta kwamba kila siku haifikii katika bajeti yake kutokana na kwamba haitunzi wazee wote kama ni sambamba inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie watoto walio katika mazingira magumu. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivi sasa watoto wanaotunzwa na serikali wapo katika Mkoa wa Mjini Magharibi tu lakini kwenye wilaya zetu ipo haja ya kujengewa majengo kama hayo ili vijana na watoto ambao wana mazingira magumu waweze kutunzwa isiwe katika Mkoa wa Mjini tu. Namuomba Mhe. Waziri ahakikishe maendeleo yanafika katika vijiji hasa katika wilaya na majimbo.

Mhe. Mwenyekiti, pia namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha atueleze kulikuwa na kituo kizuri katika Wilaya ya Kati, Jimbo la Koani pale Tunguu. Lakini kituo hiki kimekufa hatuelewi kwa mazingira gani na kwa kweli kilikuwa ni kituo cha kwanza katika wilaya za Unguja kilichokuwa kikitunza watoto waliokuwa wakipewa elimu kuhusiana na biashara au kimaendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, pia namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha atueleze kuhusu matangazo ya kupotea kwa watoto yanatutatanisha sana. Utaona katika televisheni tangazo la mtoto aliyepotea tena taahira, ama mtoto mwanamke mwenye umri wa miaka 15 amepotea, lakini husikii tena wala

huoni kwenye televisheni kama mtoto yule ameonekana vipi, au ameonekana wapi na katika mazingira gani.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atueleze je, Zanzibar hivi sasa wamerudi tena wale mumiani kwa sababu kama wamerudi ndio huwezi kusikia tangazo tena mtoto ameonekana.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema sitakuwa na mchango mkubwa kwa sababu yote wamemaliza kina mama. Mhe. Mwenyekiti, naiunga mkono bajeti hii mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Koani. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* ambaye ametujaalia mchana huu tukawa tuko katika Baraza lako hili tukufu katika hali ya uzima na afya. Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia machache katika bajeti hii.

Lakini tatu Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa juhudi yake yeye na watendaji wake kwa kuweza kutuletea kitabu chao hiki ambacho kina muelekeo mzuri wa kuweza kutukomboa wanawake, vijana, watoto, pamoja na wazee wetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia niungane na wenzangu ambao walimpa Mhe. Waziri pole kwa msiba ule ambao ulitokea wa Katibu Mkuu wetu wa Wizara hii Ndugu Rahma Mohammed Mshangama, Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri huko aliko, amuingize katika pepo yake na *inshaallah* na sisi ukifika muda wetu atupe *husni l-hatma.*

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika Idara ya Ustawi wa Jamii. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa juhudi zake ambazo amechukua za kuwaenzi wazee wetu pale Sebleni na pia akatutaka sisi Waheshimiwa Wawakilishi siku moja tuungane nae twende pale tukawaone wazazi wetu wale, pia tuweze kula nao chakula pale ili tuwape faraja wazee wetu wale. Hili tunampongeza Mhe. Waziri na tunaomba Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri ili kila wakati anapowezeshwa basi aweze kuwakumbuka wazee wetu hawa.

Lakini pia niungane nae katika suala hili kuwakumbusha wale wananchi wenzetu ambao wapo mitaani basi kujua wajibu wa kuwatunza wazee. Maana wazee si kama labda wapo Sebleni tu, wazee tunao majumbani, ndani ya mitaa yetu tunaona wazee wengine wanahangaika huku na huku wananyanyasika wanapita wakiomba ovyo na hali ya kuwa watoto wao wapo.

Hili tuweze kujua kama ni jukumu letu tunapaswa kuwashughulikia wazazi wetu ambapo hata Mwenyezi Mungu mtukufu ametuagiza katika hilo kuwafanyia hisani wazazi wetu ili tuweze kupata radhi zao na kupata radhi kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Huu ni wajibu wetu tuwaenzi wazazi wetu ili na sisi ni muda mfupi tu mbele yetu tutakuwa wazee nasi tuweze kuenziwa na watoto wetu kama tulivyoweza kuwaenzi wazazi wetu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie Idara ya Maendeleo ya Vijana. Mhe. Mwenyekiti, vijana ndio nguvu kazi yetu, ndio nguvu kazi ya taifa letu hili. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kama alivyojipanga katika kitabu chake hichi, basi tukifanikiwa kuwawezesha vijana wakaweza kuwa katika vikundi na wakaweza kupata mikopo mbali mbali ya kuweza kujiajiri, nadhani tutapunguza idadi kubwa ya wale wala unga au wanaokaa vijiweni na baadae vijana watawaeza kujiajiri ili waweze kujiendesha wao wenyewe hatimae na familia zao.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili nimuombe Mhe. Waziri kwa kuwa vijana tunao na vijana ndio wale ambao wengine tunawaandaa katika mbio za mwenge basi vijana wale wanapotoka huwa wamejifunza mambo mengi. Nimuombe Mhe. Waziri wanapomaliza harakati hizi za mbio za mwenge basi aweze kuwaita vijana wale na wakae pamoja kupanga ili waweze kutoa elimu kwa vijana wenzao katika wilaya na mikoa. Hili litawafanya vijana waweze kujielewa na kujitambua na waweze kuachana na mambo maovu.

Mhe. Mwenyekiti, hawa ni wenzetu ambao wamezunguka katika mkoa mzima wa Tanzania na wanakuwa wamejifunza mengi kupitia mzunguko wao huu. Mhe. Mwenyekiti, ni vizuri elimu ile ikawa inapatikana na kwa vijana wengine ili tukaweza kwenda vizuri katika taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa amejipanga katika kutekeleza malengo na lengo lake la mwanzo amesema anakusudia kutekeleza malengo ikiwemo kusimamia na kulinda haki za wanawake na watoto pamoja na kushajihisha jamii kuziheshimu.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri kwa hili na niombe sote kwa pamoja tuweze kuziona juhudi zake katika mpango huu na tuweze kushirikiana nae. Kwani haki za wanawake na watoto zikitambuliwa na zikiheshimiwa tunaweza tukafikia pahala pazuri na tunaweza tukamkomboa mwanamke na mtoto kwa kiasi kikubwa sana. Pia tunajua tukimuelimisha mwanamke tumeielimisha jamii.

Hivyo, niwaombe kinababa juu ya suala hili kuweza kutupa moyo wanawake hata ule wa kutusifu tu pale wanapoona wanawake wanafanya juhudi kubwa katika kuwaenzi wao na hatimae kuzienzi familia. Mtakapotupa moyo huu kuona wanawake tunajitahidi katika kuhakikisha tunafanya kazi mbali mbali za uzalishaji ili familia zetu ziweze kuwa bora, basi ni vizuri mkatuunga mkono ili tuweze na sisi kupata moyo wa kufanya vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika unyanyasaji wa kijinsia hasa unyanyasaji wa mwanamke. Mhe. Mwenyekiti, tatizo la udhalilishaji linaonekana kuongezeka siku hadi siku. Mhe. Mwenyekiti, udhalilishaji unaonekana majumbani mwetu, unaonekana katika mitaa yetu, unaonekana hata maofisini wanawake wanadhalilishwa sana. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe Mhe. Waziri kuliangalia sana suala hili kwani wanawake wana mchango mkubwa kwa taifa, wana mchango mkubwa katika jamii yao. Hivyo, kumdhalilisha mtoto wa kike au mwanamke basi uhakikishe kama umeidhalilisha jamii yote.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri juu ya hili kwamba ipo haja wizara kuweza kufanya kampeni maalum jinsi ya upingaji wa unyanyasaji wa wanawake kwa kutumia redio, magazeti na televisheni, ili kuweza kumkomboa mtoto mwanamke juu ya udhalilishaji huu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimuombe Mhe. Waziri kutokana na athari za wanawake jinsi zinavyozidi kutokea basi ahakikishe anatenga sehemu maalum, ili wanawake hawa waweze kuwa na fursa ya kupeleka malalamiko yao yale wanayofanyiwa ya udhalilishaji na waweze kupata ushauri nasaha.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ubakaji wa watoto. Mhe. Mwenyekiti, kitendo hichi sote kama wazazi ambao tunaujua uchungu wa mwana jambo hili linatutia unyonge, linatuchukiza au hatupendi hata kulisikia katika masikio yetu na tunalipinga kwa nguvu zote.

Mhe. Mwenyekiti, natoa wito hasa katika Mkoa wangu wa Kaskazini ambapo jambo hili linaonekana lipo kwa kiasi kikubwa. Mhe. Mwenyekiti, niwaombe wananchi wa Mkoa wa Kaskazini kuwa macho katika jambo hili na kupiga vita kuona kwamba tunaondokana na wimbi kubwa hili la ubakaji wa watoto wetu. Hivyo, niwaombe Masheha ndani ya Shehia zao wahakikishe linapotokea tukio hili basi wasimuachie kesi hii yule mama tu ambaye amekutwa na kadhia hii ya mtoto wake. Wahakikishe kujua hukumu imekwenda vipi na imeamuliwa vipi, wahakikishe tunamsaidia mtu ambaye anakumbwa na kadhia hii ili haki yake ya msingi iweze kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, niseme juu ya jambo hili ni kwa nini pengine linaongezeka kwa wingi. Jambo hili mimi nilikuwa *assessor* katika Mahakama ya Mkoa

Mfenesini, uendeshaji wa kesi zake unakuwa taratibu sana au hatimae hukumu hazilingani na yale matukio yenyewe yalivyokuwa.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mwengine tunawalaumu wazazi wanapokutwa na kadhia hii kwamba hawajitokezi au wanaficha lakini ule uendeshaji wa kesi pale unawakatisha tamaa na kuona ni bora nikae tu kwa sababu unapata adhabu mara mbili. Adhabu ya kwanza mwanao ameshafanyiwa tendo ambalo silo linakuumiza, lakini adhabu nyengine inakuwa nauli unayotupa kwa kufuatilia ile kesi yako ambayo hujui inaishia vipi na pengine inachukua muda mrefu sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipokuwepo pale kulikuwa na kesi pengine tangu mwaka 2003 mpaka naondoka pale bado ipo inaendelea ni kupangwa tarehe, ushahidi haujakamilika, daktari hajaja kuthibitisha, mpaka lini. Sasa haya ndio yanayowasababisha watu zinapotokea kadhia hizi basi kuona wao ni bora tu wakae majumbani. Hichi ni kitendo cha kusikitisha sana na kinawafanyia kiburi wale wanaofanya haya matendo. Kwa sababu wanaona si nimeshakwenda na bado kesi mpaka leo inakwenda pale inatiwa tarehe haoni uzito wowote uliochukuliwa, kwa maana hiyo anakuja mtaani anafanya tena tukio jengine.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Mhe. Waziri hapa katika kitabu chake amejipanga vizuri tunapata moyo. Tunakuomba haya yote ambayo umekusudia kuyafanya basi yafanye na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atakupa nguvu, atakupa uwezo, ili tuweze kukabiliana na mahasidi hawa. Maana hasidi humuhusudu hata aliyemtoa tumboni mwake. Kwa sababu mtoto yeyote wa miaka miwili au mitatu huwa na wewe ni mtoto wako tu yule.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu ni mdogo sana lakini niliona kwa kuwa mimi ni mwanamke, ni mzazi na haya yaliyosemwa hapa yote yanatugusa sisi. Lakini wenzetu wote ambao wamejaribu kuchangia basi walikuwa wameeleza haya na mimi nimeona niongezee nguvu.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri na namtakia kila la kheri. Hii ni wizara mama na kila ukijiuliza swali nani kama mama hakuna. Tuwawezeshe wanawake ili waweze kuchunga vizuri familia zao, tuweze kuwalinda vizuri baba zetu, tuweze kuwalinda watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, tunamuombea Mhe. Waziri awezeshwe katika wizara yake hii. Mafungu haya pamoja na kwamba tunayaona yamepangwa madogo lakini inawezekana siri ikawepo huko kila utakapomuendea Waziri wa Fedha basi akaweza kujua tatizo lako akakuingizia kifungu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia juu ya mia. Niwaombe Wawakilishi wenzangu wamuunge mkono sana mama yetu, bila ya mama hakuna maendeleo. Ahsante sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii fupi ya kueleza machache katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukrani za dhati kwa namna Mhe. Waziri alivyoweza kukisoma kitabu hichi kwa ufasaha kikafahamika na kikaeleweka vizuri. Nampongeza kwa uwasilishaji mzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, hii wizara ina majukumu makubwa sana, ustawi wa jamii una maana ndefu na maendeleo ya vijana, wanawake na watoto pia ina kazi kubwa. Kwa hivyo, namuomba Mwenyezi Mungu ampe uwezo Mhe. Waziri aweze kutekeleza malengo yake yote aliyojipangia kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika Program ya Mapambano dhidi ya UKIMWI. Mhe. Mwenyekiti, ukimwi ni maradhi mabaya sana na hayachagui jinsia wala umri, ni maradhi yakikuingia ndio moja kwa moja mpaka safari. Ni maradhi ambayo yakikuingia ndio moja kwa moja mpaka safari. Ni maradhi ambayo ni wajibu wetu kupambana nayo ili yasienee katika visiwa vyetu. Namshukuru Mhe. Waziri kwa juhudi yake katika kupambana na maradhi hayo ya UKIMWI.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ni vyema na sisi wenyewe tujiangalie chanzo kikubwa cha Ukimwi, chanzo kikubwa kinatokana labda tuseme na vitendo vya uasharati na tukiangalia Zanzibar ya leo ilivyo sio Zanzibar ya miaka yote iliyopita. Leo tumo katika mtandao wa kwenda na wakati. Kwa bahati mbaya sana pamoja na kujitetea sana na mimi sifarajiki kusema hivyo ni kuwa kijinsia Ukimwi niseme kuwa unaashiriwa zaidi kwa upande wa kukeni kuliko wa kiumeni.

Mhe. Mwenykiti, pamoja na juhudi yetu ya malezi yote tunayokwenda nayo kwa watoto wetu, lakini hili bila kupingwa mwenendo wa maisha wa watoto wetu wa kike ni tofauti na wakiume na kusema neno ambalo halifurahishi wanajisahau.

Mhe. Mwenyekiti, leo ukitizama ngoma yoyote iwe ni taarab, kuna taarab ya kisasa wanaita '*Modern Taarab',* ukienda kwenye *Bongo flavor* wale wavutiaji hasa wa taarabu zile ni wanawake kwa sababu ya kuvaa nguo ambazo hazistahiki wazivae. Wao ndio wanaotembea barabarani bila ya kujistahi na

hawa ni vijana na wanaume nao ni vijana tunajua ile ni *dangerous age* tunasema kwahivyo, utaona ukimwi unaongezeka siku hadi siku. Tutajitahidi kutoa mafunzo, maoni na ma-*aya* na kadhalika, lakini kama hatukuamua kurejesha utamaduni wetu wa zamani tukajiheshimu kikweli kweli sio kimasihara tukaacha kwenda na wakati, tatizo hili la kitaifa litakuwa likitusumbua kila siku.

Kwa hivyo, ushauri wangu naomba kwa kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atumie zaidi mashekhe kuona kuwa wanasaidia katika kupambana na ukimwi kwa kutoa taaluma kama alivyoeleza Mwenyezi Mungu katika Quran Tukufu na hadithi za Mtume (*SAW*).

Pili, sisi tuna vyombo vya habari nasikitika kusema kwamba ukifungua vyombo vya habari vyote vya Tanzania utaona namna ya silka zao wanavyokwenda. Lakini ukija ukifungua na sisi Wazanzibari tuna mpango wa kuigiza, hii kuigiza kwetu na vijana wakasoma pia kwa upande mwengine utaona kuwa ni njia moja ya kuona kuwa watoto hatukuelekeza zaidi katika kupambana na shughuli hii. Kwa hivyo, nakiomba hiki chombo chetu cha habari na hasa Televisheni Zanzibar sasa iende na wakati kwa kuutumia wakati wake wote badala ya kutia nyimbo kama za joti ‘mtoto husomeki’ na haitizamiki tuwe tunaelimisha jamii, ili watoto wetu wajijuwe majukumu yao hapa na hasa katika suala hili la UKIMWI.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo hili nataka nijuwe, tumeona katika ukurasa wa 54 kuna jadweli hapa ambalo linaonesha orodha ya vijana walioshiriki katika makambi kazi ya kitaifa Zanzibar kutoka nchi mbali mbali, vijana hawa walikuwa jumla 94. pia vijana wetu wametembea katika nchi mbali mbali kwa shughuli hii. Mimi binafsi sijaelewa, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri kwa kupitia kwako leo anielezee kikamilifu hasa pamoja na waheshimiwa wajumbe wengine tuje tufaidika, ni nini hasa maana ya UVIKIUTA. Umoja huu wa vijana ni upi, kwa sababu mimi mwenyewe sielewi lakini kwa hii hali ninavyoiona pengine sijui nifahamishwe unachangia vipi katika maadili yetu ya Mzanzibari, kuna athari gani na halafu unachangia kitu gani kiuchumi, je, tuendelee nao au laa. Naomba nipatiwe maelezo ili kuweza kuja kuamua kwa maslahi ya vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nafarijika nalo ni namna wizara inavyojitahidi sana kutoa fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali kazini. Tukitizama kitabu chetu hiki moja kwa moja katika ukurasa wa 20, Mhe. Mwenyekiti, utaona kuwa kifungu kitabu kimeeleza kuwa wizara inashughulikia kikamilifu fidia kwa wafanyakazi waliopatwa na ajali. Ukenda kwenye ukurasa wa 45 kuna jadweli linaonesha hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika jadweli hii kuna kesi zilizoripotiwa na kuna kesi ambazo zimebaki mpaka hivi sasa maana yake ni kwamba hazijaripotiwa na kuna kesi zilizofidiwa na kuna thamani ya pesa ambayo ni kwa hizo kesi zilizobaki. Suala langu la mwanzo hapa ni kuwa, kwa vile kesi mfano zilikuwa 40 kwa Unguja na zilizoripotiwa ni 22 tu, je, hizi nyengine ziko wapi, ina maana wanazo katika mikono yao wana pahala wanaripoti au wao wanangojewa kuripotiwa.

Hivyo hivyo kwenye kisiwa cha Pemba ambako kuna kesi 10 zilizoripotiwa, lakini 23 bado hazijaripotiwa. Hapa kidogo naomba nipate maelezo. Halafu Mhe. Mwenyekiti, tukienda katika fidia hii, kwa sababu wizara inahusika na mambo ya ustawi wa jamii na ustawi wa jamii zamani ilikuwa katika wizara ya afya, pia ilikuwa ikishughulikia watu waliokuwa wakipata ajali kazini, lakini hii ni kazi ya kuchuma mikarafuu. Kuna watu wengi walikuwa wakichuma mikarafuu na ni kazi ya kitaifa na wakianguka, zamani wakilipwa, lakini baadae ikawa kuna mirundikano tu wa idadi ya watu na hii kazi ikawachwa.

Kwa hivyo, sijui Mhe. Mwenyekiti, watu kama hawa ndio basi au kuna mpango mwengine mpya ambao umewekwa wa kutowashughulikia hawa wachumaji wa karafuu na ikiwa walikuwa katika sehemu ile, sasa sehemu ile ya wizara iko kwake. Je, ana mpango gani kwa watu hawa ambao kila siku wanaanguka na wako wengi na mpaka leo hawajalipwa na wengine kwa bahati wamepoteza hata maisha yao, na ajali walizopata ni za kila namna, wengine mpaka leo ni walemavu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine mimi nashukuru sana kwa namna wizara inavyowajali wazee na wazee kuna wale ambao wako hapa Unguja na kuna wale ambao wako Pemba. Tukifungua katika ukurasa wa 18 Mhe. Mwenyekiti, kuna maelezo ya kutosha kuhusu wazee. Kitu ninachotaka ufafanuzi hapa, ni kuwa katika kuwasaidia hawa wazee, kuna wale walioko katika nyumba ya wazee ya Welezo, wazee wale wanapatiwa chakula, matibabu, nguo, malazi, uangalizi wa pamoja na posho la Shs. 7,000 kwa mwezi. Lakini kuna wale wazee wengine walioko katika vile vituo vyengine, hawa wanapatiwa Shs. 25,000, ninataka nipate ufafanuzi je, kuna viwango vya wazee hawa yaani wazee zaidi wapatiwe hivi na wazee wengine wapatiwe hivi au kunakuwa na vigezo vya kitu gani, hapa kidogo sikufahamu.

Mhe. Mwenyekiti, pia ninataka nielewe wizara iko katika matayarisho ya kuongeza posho la hawa wazee mpaka kufikia Shs. 40,000 ni kwa wote au ni kwa wale waliolipwa Shs. 7,000.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kwa vile wanashughulika na wazee, tunajua kuwa kuna wazee ambao hawamo katika hizi nyumba, lakini wanalipwa pesa kwa

ufupi tunaita *welfare*, mpaka leo wazee wanalipwa Shs. 5,000 na pengine Shs. 5,000 zile atumie gari kuzifuatia kule kunakolipwa. Mhe. Mwenyekiti, Shs. 5,000 kwa mwezi zimeshapitwa na wakati sana tena sana. Kwa hivyo, ninaloomba Mhe. Mwenyekiti, hawa wazee ambao vigezo vyote vimeonekana kuwa wanahitaji kupatiwa msaada wapatiwe msaada ambao utaweza kuendesha maisha yao, kwa sababu hawa wazee wana mzigo mzito wao wenyewe wa kihali na familia wameshawaweka huko nyuma.

Vile vile kuna watu wa pensheni, wengine wanapata mpaka Shs. 20,000 kwa mwezi na Shs. 20,000 kwa mwezi Mhe. Mwenyekiti, ni kidogo sana. Kwa vile idara hii ya ustawi wa jamii inahusika na wazee, ningewaomba pia wizara ione kwa kushirikiana na huko kunakohusika ili wazee hawa wanaopatiwa *welfare* wameshatufanyia kazi kubwa sana na kutuwekea urithi katika nchi hii wasaidiwe zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika mbili za mwisho za kumalizia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Naam. Sawa. Mhe Mwenyekiti, nashukuru. La mwisho, napenda kuuliza wizara imeweka mpango gani kwa wale wanaume ambao wanadhalilishwa kijinsia na wanawake. Kwa sababu kitabu chote kimeeleza namna gani wanawake wanavyonyanyaswa na wanaume, lakini kuna wanawake ni wanyanyasaji wakubwa kuliko mtu yeyote na mifano iko. Kwa hivyo, wizara imewawekea mpango gani watu hawa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia juu ya mia.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nawaombeni tena kwa mara nyengine, muda hautatutosha kwa sote, kwa hivyo naomba kila yule ambaye anaweza kutoa mchango basi asirudie yale ambayo yamekwishasemwa na tutumie muda mchache sana. Anayefuata sasa hivi ni Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, anafuata Mhe. Mohammed Mbwana Hamad.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mchana huu na mimi nikaweza kuchangia bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri kwa juhudi zake za kufanya kazi kwa bidii. Pia nimpongeze katibu mkuu ndugu Fatma Bilal kwa kuteuliwa kuwa katibu. Vile vile nitowe pongezi kwa watendaji wa Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza bajeti kusema kweli Mhe. Waziri kaiwasilisha vizuri na kila kitu kimejitosheleza. Lakini nilichokiona ni kwamba bajeti hii imepangiwa fungu dogo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha,

Uchumi na Mipango ya Maendeleo basi awatizame tena kwa jicho la huruma, ili kuona bajeti hii inatekelezeka kwa kipindi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nije kwenye jengo. Kusema kweli wizara hii hawana ofisi, ofisi yao ni ndogo, haitoshi kuna baadhi ya kurugenzi ziko katika jengo jengine na waziri yuko katika jengo jengine. Kwa hivyo, inaonesha kuwa wanahitaji wapatiwe jengo. Wizara kukaa tofauti Mhe. Waziri na watendaji wake sio vizuri. Tukizingatia watendaji wengine waliokuwemo katika jengo lililokuwa halitoshi.

Mhe. Mwenyekiti, mfano kitengo cha hifadhi ya mtoto. Mule muna mambo mengi, lakini tukiangalia kuhusu kushughulikia watoto hakuna siri, kwa sababu ofisi ni ndogo. Wakiingia watu 10 kwa siku, kwa maana hiyo inabidi mule katika ofisi hawawezi kufanya kazi vizuri kutokana na ufinyu wa ofisi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, niipongeze wizara hii wakishirikiana na Shirika la *Save the Children* kutuletea kituo cha mkono kwa mkono *one stop centre.* Mhe. Mwenyekiti, sisi wanawake tumegomboka hapa, kwa sababu wamejipangia vizuri, naamini watafanyakazi kwa hakika ili kuona matatizo haya ya ubakaji yanamalizika. Pia Mhe Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kituo hiki basi waharakishe na kule Pemba ili waone kinafunguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nitowe shukrani zangu za dhati kwa wizara hii kwa kushughulikia jengo la wazee Sebleni. Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli wizara imejitahidi na Mwenyezi Mungu awajaalie waweze kuyakarabati majengo haya. Vile vile niipongeze wizara kwa kuona suala hili la wazee kutoka kwenye Shs. 25,000 na kufikia Shs.40,000. naamini hii ni jitihada ya wizara kutoka kiwango cha Shs. 25,000 na kufikia kiwango cha Shs. 40,000.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye jinsia. Kwenye jinsia sisi wanawake tuna kazi. Tukija kwenye kilimo sisi wanawake ndio wengi ambao tunajishirikisha na masuala haya, tukija kwenye familia sisi wanawake ndio tuko katika masuala haya. Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli tunapambana na kazi kubwa. Kwa hivyo, wizara hii ina kazi nzito ya kuweza kusimamia wanawake na kusema kweli wanaume pale tunapotengana nao, basi ule mzigo wote wa watoto huwa wanatuachia sisi wanawake tukizingatia uwezo wenyewe ni mdogowa kutunza watoto hawa. Matokeo yake watoto wanakosa elimu, wanakuwa wazururaji na hawapati yale malezi ya baba na mama.

Mhe. Mwenyekiti, nikiwa mimi ni mjumbe wa kamati hii, tumetembelea na tumeona kazi za wizara hii. Kwa kweli wanafanyakazi kwa mashirikiano makubwa, ikiwa wizara hii inaongozwa na mwanamke. Pia Mhe. Mwenyekiti, pale Sebleni, nilisahau kidogo naomba nitowe pongezi kwa kuweka uzio, kwa

sababu katika majumba yale ya wazee wezi walikuwa wanawaingilia kwenda kuwaibia wazee hawa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile watu wengi wameshachangia na ulituomba kuwa tusirejee. Basi na mimi niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia juu ya mia, ahsante.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwepo hapa katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na wajumbe wenzangu wa Baraza hili. Pia nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza angalau na mimi kutoa mchango wangu mdogo sana katika wizara hii muhimu ambayo iko mbele yetu. Jengine Mhe. Mwenyekiti, natoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Waziri juu ya kuiwasilisha hotuba yake hii ambayo imejaa nyama na matumaini kwa watoto wazee vijana na maendeleo yao. Zaidi ya hayo nampa pole Mhe. Waziri kwa kifo cha Katibu Mkuu, tunasema *Innalillah Wainna Ilahi Rajiun*, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema.

Pia nachukuwa nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu ambaye kateuliwa hivi juzi. Mwenyezi Mungu ampe ufanisi mkubwa na ayatekeleze majukumu yake kwa ufanisi wenye kukamilisha lengo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa idara ya Ustawi wa Jamii kuhusiana na suala zima la ulezi wa watoto. Kabla sijataja suala zima la ulezi wa watoto hawa wanaolelewa katika Kituo cha Mazizini pale, nataka niwatanabahishe wazazi wenzangu na kwa sababu humu kuna wataalamu basi nimuombe Mhe. Waziri afanye utafiti wa kutosha juu ya hili ambalo nitalisema hapa.

Waheshimiwa Wajumbe, wazazi hivi sasa tunapozaa watoto wetu huwa tunawavalisha nguo ambazo zinaitwa *pampers*. Kwa kweli mimi nina wasi wasi wa *pampers* kwamba zinawaumiza watoto wetu hasa wa kiume. Kwa hivyo, namuomba Mhe. waziri, suala hili alifanyie utafitiwa kina, kwa sababu *pampers* ni mpira ambao unawakaza vibaya sana watoto katika sehemu za nyonga na katika sehemu nyenginezo na watoto wanaume wanapokwenda haja tunajua wanakwenda haja kivipi. Kwa hivyo, naomba suala hili lifanyiwe utafiti wa kina, isijekuwa baada ya miaka labda 40 na badala ya mzee wa kiume kuzaa watoto 15 au 10 basi anazaa watoto wawili tu na wengine anawakosa. Mhe. Waziri naomba suala hili lifanyiwe utafiti wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende kwenye kituo cha kulelea watoto Mazizini. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza wizara hii kwa kuamua kulea watoto mayatima wa nchi hii ya Zanzibar. Lakini masikitiko yangu ni kwamba

mayatima wanaoishi hapa katika kisiwa hiki cha Unguja ni wengi. Lakini wizara mpaka kufikia mwaka 2010 ina watoto mayatima 49 tu katika kituo hiki. Kwa hivyo, nahisi kwamba watoto mayatima wanaoishi katika mazingira magumu kwenye shehia mbali mbali za Zanzibar ni wengi. Je, nimuulize Mhe. Waziri amefanya uchanganuo kwa kiasi gani katika wilaya zetu za hapa Unguja na akaona kwamba labda watoto hawa 49 ndio walio na mazingira magumu kuliko wengine. Kwa hivyo, naiomba wizara ijikite katika kulea watoto mayatima, kwa sababu kulea watoto mayatima ni moja katika fungu kubwa la kupata wema duniani na akhera *Inshaallah*.

Lakini pamoja na hilo Mhe. Mwenyekiti, labda nimuulize tena Mhe. Waziri juu ya matayarisho ya watoto hawa mayatima wanatayarishwa vipi, mbali ya kusoma skuli na kufikia vyuo vikuu. Wengine hawafikii vyuo vikuu, je amewaandaa katika mazingira gani watoto hawa ili watakapomaliza uyatima na kuachwa mkono kulelewa na serikali, je watajitegemea vipi katika maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, suala la tatu katika hili nimuombe Mhe. Waziri akitowa majumuisho anieleze au atueleze kwa kina kwamba watoto hawa wanalelewa mpaka mwisho wa umri gani ndio tena wanaachiwa huru.

Mhe. Mwenyekiti, nikiachilia mbali suala hilo la watoto niende katika suala la wazee. Naipongeza wizara na serikali kwa jumla kwa kuamua kwa makusudi kuwatunza wazee wa Kizanzibari. Kwa kweli wazee ni hazina na bila ya wazee hakuna mtoto. Lakini kwa hahapa nahisi Mhe. Waziri ameeleza katika kitabu chake kwamba kuna wazee wanaolelewa pale Sebleni na kuangaliwa vizuri pamoja na wanaoangaliwa katika kituo cha Welezo na kuna wazee wanaoangaliwa katika kituo cha Limbani kule Pemba na Gombani. Mhe. Mwenyekiti, inaelekea wazee wanaolelewa katika kituo cha Weleze wanapata huduma za matibabu, chakula, kupewa Shs. 7,000 kila mwezi na mengineyo. Lakini kuna wazee wengine ambao wanalelewa katika majumba haya wanapata posho la Shs. 25,000, serikali ina mpango wa kuwaongezea mpaka kufikia Shs. 40,000.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri akubaliane na mimi kwamba kuna baadhi ya wazee wanaoishi vijijini kwao wanalipwa Shs. 5,000 tu kwa mwezi. Mhe. Waziri ni vigezo gani ambavyo ulivyotumia mpaka hawa wapate matibabu, chakula, posho la Shs.7,000 na hawa wapate posho la Shs.25,000 na hawa wengine wapate posho la Shs.5,000.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuwatunza wazee itabidi wizara yako ijikiti iwaangalie wazee kwa mtizamo wa huruma sana. Kwa sababu wazee wetu wengi hasa wa vijijini wanaishi katika mazingira magumu, katika mazingira ya unyonge na katika mazingira ya umaskini sana. Kwa hivyo, wazee hawa wanahitaji

kuangaliwa ili na wao wajiskie kwamba wamepata matunda ya serikali yao hasa hii ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Mwenyekiti, Shs. 40,000 hizi basi zingewafaa wazee wa aina zote tatu ambao wanaendelea hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije kwenye sehemu ya vijana. Mhe. Mwenyekiti, vijana ni rasilimali kubwa ya nchi na ni nguvu kazi, pasi na vijana basi nafikiri nchi ingekosa nguvu kazi. Nashukuru katika hotuba ya Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein alipolizindua Baraza hili, alisema kwamba Baraza limebadilika. Miongoni mwa mabadiliko yake ni kwamba wawakilishi wengi ni vijana. Kwa hivyo, mimi nalipongeza sana hili kwamba kambi ya wawakilishi wengi ni vijana, ina maana kwamba vijana ndio nguvu kazi na ndio maana hivi sasa Baraza la Wawakilishi linatisha, watu wengi wanalisikiliza hivi sasa kwa sababu ya mchango mkubwa wa vijana. Sasa basi katika kuwawakilisha vijana wa Zanzibar, vijana wa Zanzibar wanahitaji kuwezeshwa, kutayarishwa na kuwekwa katika mazingira mazuri ambapo wao watalijenga taifa hili liwe taifa imara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kusaidiwa vijana hawa milioni 149, basi wasipewe tu vijana wakazivutia unga, watayarishiwe mazingira mazuri ya kuziendeleza fedha hizi na kuendeleza maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika vipindi vilivyopita tulikuwa na viwanja hivi vya kufurahishia watoto kama Kariakoo kwa hapa Unguja. Sasa hivi pale ukipita huku barabarani basi utakuta miti mingi imeota mule na inatokeza huko juu. Kwa nini sehemu ile haitayarishwi kwa vijana hawa wakakopeshwa mamilioni haya ya fedha wakahamia pale, kwa ajili ya kuendeleza biashara, kwa sababu pale ni *center* nzuri sana kibiashara.

Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri hili uliangalie kwa kina, ili vijana wetu wafaidike katika nchi yao na waepukane na madawa ya kulevya, bangi na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo kwenye suala la vijana kwa ajili ya kuokoa muda haraka, basi nizungumzie suala zima la wanawake na mavazi. Mhe. Mwenyekiti, wengi miongoni mwa Wajumbe waliozungumza hapa wamezungumzia kuhusu suala la kubakwa, kwa kweli kubakwa ni tatizo, lakini tatizo hili linasababishwa na mambo tofauti. *(Makofi)*

Kwa hivyo, miongoni mwa mambo yanayosababisha jamani baadhi ya wanawake wanakwenda vibaya. Kwa mfano, unamkuta mwanamke amevaa nguo imemganda kiasi ambacho mpaka alama za vyombo vya ndani vinaonekana, hivi kweli asibakwe angoje nini. Kwa upande wa watoto wadogo

wanabakwa kwa sababu mbali mbali kwanza kuna wanaume wana maradhi ya nyoyo zao kwa ajili ya hivi vitoto vidogo. Lakini kuna baadhi ya watoto hawavalishwi nguo za kutosha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, unaweza ukatembea katika eneo ukamkuta mtoto mwanamke amevaa kikanzu kifupi sana, yaani unaona mpaka maeneo mengine, sasa yule mwanamme mwenye maradhi afanye nini. *(Makofi)*

Sasa jambo la msingi wazee wanawake wawatunze watoto wa kike, ili waepukane na kubakwa kiholela. Hivyo, basi ndani ya suala hili la mavazi nakuomba Mhe. Waziri kuna changamoto kubwa hivi sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa walimu wanawake pamoja na maafisa wao. *(Makofi)*
Kwa kweli wanawake Mwenyezi Mungu amewapa sana na hata baadhi ya mavazi yao yamekuwa ni mengi zaidi kuliko wanaume, yaani hata mavazi ya kuvishwa siku ya kufa basi mwanamke nguo zake ni nyingi kuliko mwanamme. Mhe. Mwenyekiti, kwa nini maafisa wa elimu wanawapambua wanawake waliopambwa na Mwenyezi Mungu mwenyewe. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kutoa majumuisho basi atuekee wazi mavazi ya wanawake kazini na wala tusiwaache wanawake kazini wasisitirike. Kwa mfano, watoto wanaosoma skuli wanavaa mashungi, kwa nini walimu wao wasivae mashungi waambiwe wavue mashungi.

Hivyo, kama kuna mashungi yanababaisha au yanashawishi kuna aina fulani ya mashungi, basi ni vyema kuambiwa mashungi ya aina hii msivae na badala yake wavame mashungi ya aina fulani. Sasa kwa nini wanafunzi wanavaa mashungi ya sare zao na wasivae mashungi walimu wao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwamba walimu kuvaa nguo za kuwasitiri ni heshima kubwa zaidi kuliko kuwapambua walimu mavazi yale ambayo yanaletastara, kwa sababu wanafunzi wako ambao ni watundu

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakuomba umalizie.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa nataka niheshimu muda wako, kwa sababu kesho usijeukasema Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi ukimpa muda anaweza kuutumia ziada. Kwa hivyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, pia namuomba Mhe. Waziri wakati wa majumuisho anipe maelezo yangu. *(Makofi)*

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijaalia kusimama katika

Baraza lako hili tukufu kwa siku ya leo na mimi kuweza kutoa machango wangu huu kama mwanamke wa Wilaya ya Micheweni.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti kwanza nampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutuletea kitabu hiki kizuri cha bajeti. Kwa kweli lengo kuu ni kumkomboa mwanamke, mtoto pamoja na vijana kwa jumla kwa hilo nawashukuru sana. *(Makofi)*

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, umesema tusirudie mazungumzo yale kwa yale ni kweli na tutafanya hivyo. Lakini kuna suala moja ambalo ni lazima tuligusie na suala hilo linatuumiza zaidi sana kuhusu bajeti hii ya kima kinachoingizwa humu ni kidogo sana kwa wizara hii pamoja na majukumu aliyonayo Mhe. Waziri kwa ujumla. *(Makofi)*

Kwa kweli tukimuangalia Mhe. Waziri ana majukumu ya wanawake kuwasimamia haki zao, watoto ambayo ndio rasilimali na taifa la kesho pamoja na kusimamia vijana kwa jumla uende katika mwenendo mzuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, katika hili namuomba Mhe. Waziri wa Fedha alione sana, ili amjaalie fungu angalau kidogo liweze kumuwezesha. *(Makofi)*

Nikiondoka hapo sasa nije kwenye Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Katika utekelezaji wao wamesema miongoni mwa hayo ni kusimamia na kulinda haki za wanawake na watoto pamoja na kushajihisha jamii kuziheshimu. Mhe. Mwenyekiti, hili ni suala zuri sana, lakini kwa upande wa idara naona hawawezi kushajihisha jamii peke yao.

Kwa hiyo, kuna jumuia hizi zinazoundwa kwenye shehia ambazo ni Jumuia za Wanawake. Kwa mfano, katika Jimbo la Tumbe kuna shehia karibuni mbili na zote zina jumuia hizi, lakini jumuia hizi zinabakia katika kwenda wao kwenye semina na kurudi, sasa kwa upande wa jamii kwa kiasi fulani bado hawajatoa elimu kwa jamii hususan ya kike kwa wanawake wenzao.

Mhe. Mwenyekiti, idara itahamasisha kupitia vipindi kama vile vya redio na *television*, lakini ukimwangalia mwanamke na mazonge yake aliyonayo na mchana wa kutwa basi hana wakati wa kusikiliza redio wa kuangalia *television*.

Sasa namuomba Mhe. Waziri kupitia jumuia hizi basi yeye aanze kuzihamasisha hizi jumuia katika mafunzo yao wanayowapa, hivyo ni vyema kuwataka na wao wawashajihishe wanawake wenzao angalau kupita kijiji kimoja kimoja kwa ajili ya kutoa elimu ya kuwaelimisha wanawake kujua haki zao pamoja na kulea watoto wa majumbani. Kwa hiyo, suala hili isiwe kwa

jumuia tu kwenda kwenye semina na kurudi na tukaambiwa kuna jumuia za wanawake, lakini hatuoni kazi ambazo wanazifanya.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu idadi ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Mhe. Mwenyekiti ni kweli wako watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ni vyema kusaidiwa.

Lakini mimi naomba nitoe kilio changu Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli siku zote Baraza hili ni mashahidi wakati yanapotolewa maelezo ni Wilaya ya Micheweni ndio wilaya inayoishi katika mazingira magumu, pia ndio wilaya ambayo ina ajira nyingi za watoto, yaani ni wilaya ambayo ina kila aina ya matatizo. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nikitizame kwenye vitabu vya bajeti sioni msaada wake unaosaidiwa. Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti, kuna hii idadi ya watoto wanaishi katika mazingira magumu wanaotambuliwa Pemba sijaona Wilaya ya Micheweni kitongoji hata kimoja. *(Makofi)*

Lakini humu sijasikia hata siku moja tukiambiwa kwamba Wilaya ya Wete ndio wenye matatizo magumu. Kwa hivyo, wilaya hii yenye matatizo magumu nawatizama watoto wanaosaidiwa wako wapi na ajira mbaya ziko huko pamoja na mashaka yote yako katika wilaya hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje anieleze kwa nini hakuna watoto wanaoishi katika mazingira magumu Wilaya ya Micheweni au hawajajua utaratibu huu uko vipi na kuna nini? Ili na wao wapate kusaidia. Lakini nashangaa kuona kwamba Wilaya ya Wete kuna vijiji vingi ambavyo vimeorodhoshwa humu na wala sijaona Wilaya ya Micheweni sijaona. *(Makofi)*

Vile vile kwenye kiambatanisho Nam. 3 kuna aina za Kesi za Udhalilishaji wa Watoto na zimetajwa hapa kama vile kubakwa pamoja na mambo mengine mengi ambayo yameelezwa. Mhe. Mwenyekiti, suala hili naona wanatudanganya, kwa sababu katika masuala haya ambayo yamekithiti kwenye Visiwa hivi vya Zanzibar kwa takwimu hii sioni kuwa ni nzuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hapa pamoja na kwenye Jumuia za Wanawake ambazo zimeundwa basi kazi hii iwe moja ya kupeleka ripoti kule kunakohusika, kwa sababu hawa wao wanadhani takwimu hii ni wale tu wanaokwendakupeleka pale kesi zao, lakini walioko huku vijijini pengine hawajulikani na mambo yao watu wanayaficha.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri pia awashajihishe jumuia hizi kufanya utafiti na masuala haya, ili wawape elimu waweze kupeleka taarifa kunakohusika.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sikuwa na mchango mkubwa ni kuhusu hizi kesi zinazopelekwa, pengine mtu mtoto wake amebakwa au amebeba ujauzito labda atajifunga kibwebwe aende polisi ama Wizarani Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Lakini kesi hizi hatima yake huishia hapa njiani, sasa sijui ni wazazi au ufuatiliaji wa zile kesi unawapa usumbufu ama ni mambo yao ya kukubaliana huku na badala ya kwenda kwenye kesi siku moja, kwa sababu ana uchungu wakati ule na baadaye kushawishiwa pengine na kusamehe kesi ile.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba wizara iwe na mkakati maalum kwamba mtu yeyote atakayekwenda na kesi yake ikiwa wizarani au polisi, basi waweze kupewa masharti kwa sababu wasihangaishe watu, kama mtu mambo yake anayaweza basi abakie nayo nyumbani.

Kwa hivyo, ikiwa hayawezi anakwenda nayo Mahakamani au kwenye wizara hii, basi wizara ifuatilie masuala yake moja kwa moja. Lakini kesi nyingi huwa zinaishia na wala hatuzitii nguvu na hatimaye watu kuendelea na masuala haya, kuona kuwa ukeshakwenda kwenye kesi siku moja, mbili na ukiwa na shilingi 100,000/= tu ukeshampa mtu basi huwa hayana mpango maalum. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri ujitahidi sana na ufuatiliaji huu wa kesi na wala usiwakubalie watu hata kidogo na kuja pale wizarani, kwa sababu wana uchungu wakati ule, pengine yule mtoto hajashauriwa na kubakia kuridhia yale masuala mengine na kumuacha mtoto yule katika mipango ya udhalilishaji. *(Makofi)*

Suala jengine kuhusu kuwapa mimba wanafunzi ambao kuwa unafanywa na walimu ama mwalimu wa chuoni au skuli. Kwa kweli suala hili ni baya sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sisi wazazi lengo letu baada ya mtoto wetu kuondoka majumbani ni kupeleka chuoni kwa ajili pale unasaidiwa ulezi au unampeleka skuli kwa kuwa mwalimu naye pia ni mlezi wa mtoto yule. *(Makofi)*

Saa leo itakuwaje mwalimu afanye kinyume kwa mtoto yule na kuweza kumfanyia kitendo kama hicho. Kwa hivyo, tunaiomba wizara litakapotokea tukio kama hili basi mwalimu yule ni wakufukuzwa skuli hasa. *(Makofi)*

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wanawake wa Wilaya ya Micheweni naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa ya kueleza machache kuhusu hoja iliopo mbele yetu. Kwa kweli mimi si mzungumzajii sana katika mambo ya wanawake, lakini kwa kuwa na mimi nimo kwenye Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, nadhani haitokuwa vibaya kama nitatia nyalio kidogo kuhusiana na hili.

Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na baadaye nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ya kueleza machache juu ya hoja iliopo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kumteua huyu mama kuwa waziri wa wizara hii. Kwa kweli amesibu kwa sababu huyu mama katika masuala ya watoto na wanawake utafikiri amesomea hii fani, lakini anajitahidi sana huyu mama. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nitumie fursa hii kumpongeze huyu mama kwa ajili ya kuweza kufanikisha majukumu yake yeye pamoja na wataalamu wake katika kuhakikisha kwamba maendeleo ya nchi hii yanapatikana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika Idara ya Ustawi wa Jamii na nizungumzie watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Lakini kabla sijaenda kwenye hotuja naomba nitoe tanbihi kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli napenda niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kufanya utambuzi wa watoto wenyewe mazingira magumu tokea mwaka 1966. Kwa hivyo, katika miaka hiyo ilikuwa ikiongozwa na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume walifanya utambuzi wa kuwepo watoto wenye mazingira magumu na kutoa nyumba pale Forodhani. Kwa hivyo, bidii hii ya wazee wetu inabidi tuiendeleze sana, tuienzi pamoja na kuitunza pia. *(Makofi)*

Population density ya Zanzibar asilimia 40 ni watoto, Mhe. Mwenyekiti kwa hali hii wanahitaji kutunzwa, kuenziwa pamoja na kusaidiwa katika hali kusudi waweze kuwa katika mazingira mazuri. Kwa kweli watoto ni walipakodi watarajiwa wa nchi hii tena pia ni viongozi watarajiwa wa nchi hii. Sasa kwa vile mtu anayemdhalilisha mtoto au anayemdharau mtoto ni sawa na mkulima aliyedharau kitalu chake cha mbegu, sidhani kama atapata mazao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kuipongeza wizara, kwa kuweza kufanya utambuzi wa watoto wanaishi katika mazingira magumu katika wilaya mbili, yaani Wilaya ya Magharibi Unguja na Wilaya ya Wete Pemba kwa kuweza kufanya utambuzi wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Hivyo, wameweza kuatambua watoto 7,711 katika Wilaya ya Magharibi na watoto 4,742 katika Wilaya ya Wete na takribani hao ni watoto 12,453 katika wilaya mbili tu. Kwa hivyo, hali ni mbaya sana ikiwa wilaya mbili za Zanzibar tu, kwa sababu wilaya zote ni 10, sasa wilaya mbili za Zanzibar zina watoto 12,453 wana mazingira mabaya hivyo wilaya 10, nadhani hali ni mbaya sana. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, tunahitajika kuchukua hatua madhubuti katika kuhakikisha kwamba watoto hawa wanaondoka katika mazingira haya magumu. Vile vile tuangalie nini kinachosababisha watoto kuingia katika mazingira magumu. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, nadhani pamoja na mambo mengine ni suala zima la ndoa kukatika kienyeji, watoto kuwatelekeza pamoja na wawazi wao. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama viongozi wa nchi hii tunalo jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba hivi viashiria vinavyopelekea watoto kuwa katika mazingira magumu tuvidhibiti. *(Makofi)*

Kwa kweli nawaombeni sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza kwamba tujihitahidi sana kwa wale watoto waliofiliwa na wazazi wao, kuwashajihisha wenye uwezo wawasaidie. Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna Sadaka na Zaka na tunawaona watu wenye uwezo wanatoa Sadaka na Zaka, lakini hawa watoto inakuwa si rahisi kuwafika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba ni siis Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwashajihishe wenye uwezo waweze kupeleka sadaka zao kwa walengwa yaani hawa watoto wanaoishi katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Kwa mfano, siku nyengine ukipita pale *Azam Modern Bakery* karibu na Siku Kuu unakuja foleni za watu wazima wanasubiri Sadaka pale. Lakini watoto wanaoishi katika mazingira magumu walioko Matemwe, Wawi, Vitongoji hawafiki pale kwenda kukaa foleni kwa ajili ya kupata sadaka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tujitahidi kuwashajihisha hawa wenye uwezo waipeleke sadaka pale inapohitajika.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, niliombe Baraza lako tukufu tuwanasihi wenzetu, yaani wapiga kura wetu wadumishe ndoa zao, ili kuweza kuwatunza watoto wetu. Kwa kweli inaonekana wanaume ndio mstari wa mbele katika kutoa talaka, sasa pia na akinamama wanahusika sana. Kwa mfano, kuna akinamama wengi wanaodai talaka, pia kuna akinamama wanaowaachia watoto waume zao baada ya kupata ushawishi wa wanaume wengine. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nadhani sisi kama Wawakilishi wa wananchi basi tuhakikishe kwamba tunawanasihi wapiga kura wetu hasa hawa akinamama kwa sababu wanavyo vitimbi vingi, yaani wawanasihi wanawake wenzao wasitukatae na kutupia mizigo. Mhe. Mwenyekiti, sisi tutajitahidi sana kuwashajihisha akinababa hapa. *(Makofi)*

Kwa mfano, juzi nilikuwa nikitembelea Nyumba ya Watoto, kuna mtoto wa miaka miwili Mhe. Mwenyekiti mama yake amemuachia baba yake, yaani amemtupia tu na sijui amechukuliwa na nani yeye huko, sasa yule baba hajui kulea ndio amemleta pale, mtoto mzuri tena ana afya yake na analelewa pale. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, na nyinyi wanawake mjitahidi sana kuwashajihisha wanawake wenzanu wasidai talaka kiholela pamoja na kututupia mizigo wakeshaghilibiwa huko. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu Mradi wa Jinsia. Mhe. Mwenyekiti, ulimwengu mzima hivi sasa una-*advocate* mambo haya ya *gender*, unanadi kwamba unyanyasaji wa kijinsia usiwepo. Kwa kweli mara nyingi na mpaka hivi sasa wanadai akinamama kupatiwa uwiano sawa katika vyombo kadhaa vya serikali pamoja na hivi vya kutunga sheria.

Kwanza napenda niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kuweka karibu asilimia 40 ya Viti Maalum, kwa hilo napongeza sana. Kwa hivyo, ni vyema akinamama mjitahidi sana kwa sababu serikali hii inawaonea huruma na mnatakiwa muwe na uwiano sawa katika vyombo. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninachonasihi hapa katika suala la *gender balance*. Kwa hivyo, akinamama wasibweteke, kwa sababu wanao uwezo na Mwenyezi Mungu amewajaalia neema kubwa ya akili, maarifa na nguvu. Sasa neema anayokujaalia Mwenyezi Mungu lazima uitumie na usipoitumia neema hiyo, basi inaondoka kwa sababu hukumtukuza Mwenyezi Mungu kwa neema hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mweyekiti, kuna nadharia inayosema “wanawake wakiwezeshwa wanaweza”. Kwa kweli wanawake bila ya kuwezeshwa wanaweza hawa, yaani

wanaweza na wala wasibweteke wakasubiri mpka wawezeshwe, kwa sababu wanaweza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano kidogo ilioko ndani na nje ya nchi kuhusu kuwa wanawake wanaweza. Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa hivi sasa ni mwanamke anatoka Tanzania na anava mkashtada kama hawa wetu wa humu Barazani. Kwa kweli amehangaina kwa kusoma na kuweza na kuchukua *PhD* yake pia amehangaika katika masuala ya kimataifa na kuweza kuwa Naibu Katibu Mkuu. Kwa hivyo, hakuna haja ya kuwezesha wanaweza. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wanawake wana *creative mind*, yaani wana akili tambuzi tena zenye kujenga. Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti pale Liberia mama mmoja anaitwa Balson Serdif ndio Rais wao tena amewashinda wanaume kwa kuwauunganisha Waliberia pale. Kwa kweli wakati wa Rais Samuel Doh na Thomas Sankara ilikuwa vita haviishi, lakini bada ya kupewa yule mama basi Liberia imenyooka, jamani dogo hilo, mwanamke mweusi kama nyie. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wakisema wanawasubiri kuwezeshwa na kuletewa viti maaluma hapa, basi mtakuwa katika hali ngumu. Kwa hiyo, watumie akili zao ili wawe sawa na wanaume. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ni mama mmoja anayeitwa Anna Makinda *black skin* kama nyie hivyo na tangu Bunge la Jamhuri ya Muungano liasisiwe mama yule Bunge analiendesha vizuri sana. *(Makofi)*

Sasa nadhani kuna haja ya kutumia, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo ikiwa hawa hawakutumia vipawa walivyopewa na Mwenyezi Mungu, kuna nadharia nyingi sana zinazoonesha kuwa kuna tatizo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu ninukuu nadharia moja ya *psychologist* mmoja anasema hivi "*The organ which is used will develop better and the organ which is not used will be generate*." Kwa hivyo, maana ni kwamba kiungo ukikitumia kinakuwa hadhiri na kinaweza kufanyakazi, lakini kama hukikitumia basi kinaondoka. *(Makofi)*

Kwa mfano, wachezaji mpira kwa sababu misuli wanaitumia hii, basi misuli yao ni migumu sana, hali kadhalika nyoko alikuwa jeuri hatumii miguu yake katika kwenda basi miguu imeondoka, vile vile jongoo alikuwa jeuri hafumbui macho yake yameondoka. Sasa na nyie akinamama ikiwa mtakaa hapa na kusema kwamba tunasubiri Viti Maalum, *gender balance*, basi mtapoteza akili pamoja na nguvu zenu. *(Kicheko/Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, naomba sasa mjitahidi kuweka *gender balance* kwa kuweza kutumia hivi vipawa alivyowajaalia Mwenyezi Mungu, ili visije kuondoka kama ilivyoondoka miguu ya nyoka na macho ya jongoo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu suala la mapambano dhidi ya UKIMWI. Kwa kweli bado kabisa Mhe. Mwenyekiti, yaani UKIMWI ni tatizo katika nchi hii, tena kwa bahati umesibu katika *engine* kama tuseme hii *population* yetu ni *machine*, basi tungesema UKIMWI umedhibiti *engine*, yaani vijana, kwa sababu vijana ndio *engine* ya maendeleo katika nchi, kwa kiasi kikubwa umesibu pale. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nadhani katika hili serikali ina kazi kubwa ya kufanya, tunaomba muwawezeshe hawa, serikali iwawezeshe wizara hii. Kwa sababu bajeti mnayowapa ni ndogo na hawa ndio wenye vijana, leo mnawapa bajeti ambayo hata hao vijana kwenda kuwafanyia kazi kushirikiana na vyombo husika kuweza kuwapa taaluma ya kujikinga na huo Ukimwi inakuwa pesa ni ndogo. Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, tulione hilo, kwamba wizara hii ina-*engine* ya nchi yaani vijana, wizara hii inalea watoto, kwa hivyo wanahitaji bajeti yao iwe kubwa itanuliwe.

Lakini vile vile niungane na Mheshimiwa wa Chambani pale, kwamba hili suala la UKIMWI na udhalilishwaji wa jinsia wanawake wenyewe wanachangia sana, mambo ya mavazi haya Mheshimiwa. Mimi huwa naangalia wakati mwengine kwa bahati mbaya tu nikipita ukumbini pangu, kwa sababu mimi mambo yake vijana huwa wanaangalia tena mimi huwa siangalii sana. Wanawake katika kulisakata rumba basi wanaume wanavaa suti na tai, lakini wanawake viguo viko mapajani. Ni tatizo Mhe. Mwenyekiti, na UKIMWI hauwezi kukimbia kama wizara hii na serikali haikuwa makini.

Sisi hapa katika miaka ya 1960 tulikuwa na *Presidential Decree* ukitembea na nguo fupi unapigwa mikwaju pale pale, kabisa kabisa, wakaanza kuvaa nguo refu zenye kuwabana (chupa) ikawa wanakula mikwaju pale pale, lakini inaonekana serikali yetu imeachia mambo tu hivi. Kwa hivyo, ili UKIMWI tuuweze kwanza tujitahidini sana kutuletea sheria yenye meno hapa iweze kuwatafuna wale wote wanaotembea nusu uchi.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, si mimi nachangia hapa lazima Mhe. Mwenyekiti, ujue kwamba mwanamke akitembea nusu uchi macho yanaona, hata shehe akifumbua macho hivi anaweza kumuona. Tendo hili Waheshimiwa ni *scientific action* kwa sababu *optic norve* ikishaona sehemu ya siri ya mwanamke inasafirisha mpaka *hypos lamas of the brain*, sasa ikeshafika huko kuna *homones* wanaitwa *testosterone* anatolewa, baada ya kutolewa anasababisha *reaction* ya *reproductive organs*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ikianza kutokea hivyo na wala sitaki niende sana kwa sababu sitaki kutumia lugha mbaya kwenye Baraza, basi kichwa cha mtu kinapotea akili, ndipo unapoona mtu amejiingiza kwenye janga ambalo hakulitegemea kwa uzembe wao wanawake wa kutokuvaa nguo vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Kutokana na mambo haya mashehe wengi wameshaganda kwa kupitiwa na nguo fupi na wao wakababaika mpaka yakawatokezea hayo na kufanya mambo hayo. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tuletewe sheria ya nguvu sasa, yaani mtuletee Sheria ya Kudhibiti Mavazi katika nchi hii, kwa nini Marehemu Mzee Abeid Amani Karume pamoja na waasisi wengie walifanikiwa kwamba watu wasiende ovyo hapa. Kwa kweli sisi ni *intellectuals*, yaani watu na taaluma zetu tushindwe jamani, ni aibu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, malizia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kuunga mkono kwamba kwanza nalaani sana suala la udhalilishaji wa akinamama. Kwa hivyo, naunga mkono hoja ya akinababa wanaobaka watoto, walemavu wahasiwe. *(Makofi)*

Sasa kwa wale waliokuwa hawajui kuhasiwa Mhe. Mwenyekiti, maana yake ni *medical removal reproductive organs*, baada ya kuondosha inakuwa mambo haya hayapatikani tena. *(Makofi)*

Kwa hiyo, utungwe Sheria ya kudbibiti mambo hayo na iletwe Barazani na tutaipitisha kwa wingi Mhe. Mwenyekiti, ili kuweka heshima na maadili mema ya nchi hii pamoja na kujikinga na huo UKIMWI. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, funga hotuba yako maliza.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu sana, naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri kama ingekuwa unaruhusika kuunga mkono kwa asilimia 200 chini ya 100 basi ningeunga mkono hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, bado tunao wachangiaji watatu kutoka *backbencher*, halafu tutakuwa na wachangiaji wanne. Kwa hivyo, hawa wa *backbencher* atakuwa Mhe. Ali Salum, Mhe. Salmin Awadh Salmin na Mhe. Hamza Hassan Juma na baadaye atachangia Mhe. Mwanasheria Mkuu,

akifuatiwa na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Waheshimiwa wajumbe natarajia leo tutamaliza shughuli yetu, ili kesho tuanze na wizara nyengine.

Baada ya hayo, nakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa utulivu na michango yenu mizuri na *Inshaallah* tutaonana tena jioni leo saa 11:00. *(Makofi)*

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii ya leo kutufikisha hapa tukiwa wazima na wenye afya njema, pili nikushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikachangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Wizara ya Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti kwanza nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa kazi ngumu ambayo tumemtwika ya kuweza kuwahudumia wananchi wote wa Zanzibari isipokuwa watu wazima wanaume, nadhani jina la wizara yetu tungaliangalia utaratibu wa kulirekebisha kidogo badala ya wanawake na watoto angalau ikawa jinsia na watoto, kwa sababu kuna Mheshimiwa mmoja siku moja hapa alisema tuanzishe jumuiya ya wanaume sasa hivi, kwa sababu wanawake kile siku wanaongezeka nguvu zao.

Mhe. Mwenyekiti mimi nataka nianze moja kwa moja kwenye Idara ya Mipango na Uendeshaji, mimi niwapongeze kwa kazi nzuri lakini vile vile kuna jambo kidogo hili nilikuwa nataka nilizungumze na wenzangu walizungumza Mhe. Subeit Khamis Faki saula zima la kwenye kiambatanisho namba nne, ilikuwa inazungumza kuhusu suala lamadeni ya wafanyakazi walioumia kazini zinadaiwa karibu Shs. 65,000,0000 nilivyoona kwenye kitabu ingawa Mhe. Subeti alizungumza milioni 73,000,000.

Sasa hili nadhani sijui fungu hili katika bajeti hii ya Wizara ya mwaka huu sijui fedha hizi zilitengwa kwa ajili ya malipo haya kama hazikutengwa basi Mhe. Waziri aje atusaidie maelezo ili inapofika bajeti ya Wizara ya Fedha, kwa sababu tumejaribu kuchungulia katika buku la Wizara ya Fedha kuna

maburungutu ya pesa kule yamehifadhiwa kwa ajili ya mambo kama haya ya dharura. Mhe. Mwenyekiti tutamsaidia sana Mhe. Waziri kuzitafuta pesa hizi kwa sababu sasa hivi serikali yetu imo katika suala zima la utawala bora na imeundwa Wizara ya Utumishi wa Umma, sasa hawa haya maendeleo yanayopatikana kama si watumishi wa serikali tungeliyapata kwa njia gani.

Sasa kama kuna fedha hizi karibu Shs. 65,000,000 ameeleza Mhe. Waziri kwamba wanatudai wafanyakazi ambao wameumia wengine tunaambiwa tokea mwaka 2007 tusimjali mtu anapokuwa mzima tu, lakini tunatakiwa tumjali zaidi pale anapokuwa mgonjwa kwa sababu hata zile nguvu za kutafuta rizki kwa upande mwengine zinakuwa hazipatikani. Sasa Mhe. Waziri aje atujibu hapa Je, hili fungu limo ndani ya bajeti yake au anategemea fedha kutoka serikalini katika mfuko mkuu wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nimuonee huruma Mhe. Waziri wangu kwa kuhamishwa katika jengo kwa sababu hii Wizara sio mpya, hii wizara ni kongwe mimi nadhani ile wizara iliyohamia pale ya rafikia yangu mpendwa mpezi wangu Maalim Haroun Ali Suleiman Wizara ya Kazi na Uwezeshaji wa Wananchi yeye ndio alikuwa atafutiwe pahala pa kukaa, lakini hii wizara ina vitengo vyake na shughuli zake wamehamishwa wamepelekwa hukoo wanajibana bana Mhe. Waziri wangu wanambana bana mimi nadhani ilikuwa sio jambo la busara sana sasa hili tutaiomba serikali katika mipango yake ijaribu kuangalia katika yale maeneo ambayo tunaweza kuyaboresha kidogo basi na jengo hili la wizara apatiwe eneo lake afanye kazi kwa vizuri hasa kwa kazi ngumu ambayo tumemtwika.

Mhe. Mwenyekiti, bado niko katika Idara ya Mipango na Uendeshaji kwa sababu shughuli zote ndio ziko hapa na kama nitaamua kupiga buti basi nitapiga buti katika kifungu hichi cha mipango na uendeshaji, mimi nazungumzia suala la nyumba ya Forodhani nakubali kwamba mimi niliwahi kuwa Waziri huko nyuma, lakini serikali yetu maisha yote ilikuwa inahimiza suala zima la utawala bora. Kwa hivyo inaonyesha wizara inapoulizwa swali likisha maliza kujibiwa hapa inaonyesha linakuwa limeshamaliza. Sasa sisi hapa barazani ajira kubwa ya wabunge na wawakilishi ni kusema hatuji na jembe hapa wala panga wala mndu ajira yetu sisi kusema, kwa hivyo maneno yetu tunataka serikali iyasikilize kwa sababu sisi tunasema halafu tunalipwa ukenda marikiti kule watu wanapiga mnada mpaka saa 10.00 kama huna ndizi mkononi hupewi pesa na mtu uuze, sisi tunauza maneno.

Kwa hivyo tunapozungumza sio kwamba tunakusudia kubabaisha babaisha tunaposema serikali itusikilize Mhe. Mwenyekiti suala la nyumba ya Forodhani leo kama hatujapata jawabu iliyokuwa sahihi Mhe. Mwenyekiti hii bajeti inaweza kupata tabu, kwa sababu gani katika kikao kilichopita Mhe. Salmin

Awadh Salmin ambae sasa hivi ni mnadhim wa CCM hongera kwanza aliuliza, tunataka mkataba kwa sababu tunajua watoto wetu wako katika jengo la *ZAYADESA* leo kama ingekuwa ruhusa kuchangia ningekwambia changia hapo hapo na wewe maana yake na wewe *ZAYADESA* unaijua vizuri, lakini nimefanya kazi nzuri nimefanya kazi nzuri sana. Mhe. Salehe hajaja mwana mapinduzi na mimi nikiwa mwanamapinduzi mwenzake *ZAYADESA* imetekeleza yale mawazo na fikra za waasisi wa taifa hili ambao ni Mzee Karume ndio aliyeanzisha nyumba ile ya Forodhani, leo limejengwa jengo zuri tunakubali. Lakini lile jengo bado tunasema la *ZAYADESA* sasa ndio maana waheshimiwa wakataka tupate mkataba wa kuhakikisha kwamba wale katika eneo lile wataendelea kuwepo bila ya matatizo yoyote.

Sasa watu wanachanganya mambo wanasema hawa watu wana ushabiki sio ushabiki sisi hapa tunapozungumzia suala hili ukiangalia katika sera yetu na ilani yetu ya uchaguzi ambao ndio inayoongoza serikali, katika utekelezaji wa ilani tunafuata mkuza ukija katika mkuza kuna klasta tatu moja katika hizo ni utawala bora, utawala bora vile vile umegawanyika katika maeneo mengi *transparence* uwazi. Mhe. Mwenyekiti kama tunataka demokrasi hakuna cha kuficha Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Moh'd Shein katika ziara zake anahimiza anawaambia watendaji elezeeni mafanikio mliyoyafanya, penye matatizo pia elezeeni. Sasa leo kitu kidogo tu mkataba mpaka leo sasa Mhe. Waziri mimi nakuonea huruma sana na nakuonea huruma kwa sababu utakuwa huna jawabu ya kutosha tutakupatisha tabu.

Lakini sisi nia yetu wananchi kama wana hofu kwa sababu maneno tunayosema sisi ni maneno ya wananchi na ndio waliotuleta hapa majimbo hamsini, kama watu wana wasi wasi wa kitu kwa nini yasitolewe maelezo ambayo mimi najua kuna nia njema, mimi siku iliyofunguliwa bustani ya Forodhani nilikuwepo kwa bahati nzuri Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambae amestaafu alitoa maelezo fasaha kabisa, kuhusu jengo lile la watoto Forodhani kwa sababu watu wana hoji je lile jengo sasa hivi kapewa nani na linatumika kwa shughuli gani, kuna na mambo gani alitoa maelezo mazuri pale.

Alisema kwamba watu pale walikuwa wanafikiria labda kuna hivi na hivi mpaka ile bustani ilitiwa maneno, lakini alipotoa ufafanuzi Mhe. Rais maneno yote yakawa yamemaliza kwa sababu kuna wengine walisema labda bustani ile ni ya yule mwenye nyumba ya Forodhani kumbe bustani ya kila mwananchi kila mtu anakwenda kugaragara sasa hivi, je leo ameondoka tufuate nyayo za viongozi wetu kutamka yale mambo hadharani ukishatamka hadharani mambo yanakuwa yameshamaliza, sasa inapokuwa viongozi wetu wanaonyesha mfano

mzuri. Sisi tunaogopa ogopa kusema ina maana sisi ndio tutasababisha majungu na wananchi waseme mambo yaliyokuwa siyo.

Sasa siku ile Mhe. Rais mstaafu alizungumza kwamba lile jengo la Forodhani ambalo wamehama watoto anashauri tuangalie taratibu za kuweza kuweka eneo liwe kama jengo la kuweka kumbukumbu ya wale mabaharia, kule hakuna hansard lakini kumbu kumbu kwa sababu Rais anapokwenda katika ziara ndio maana anafuatana na watu wengi ili kila mmoja achukue yale maagizo. Sasa ile nyumba ya Forodhani yale maagizo ya Mhe. Rais mstaafu yanatekelezwa au vipi ile *future* ya eneo lile la juu linakuwaje je ile kuweka kumbu kumbu itakuwepo si hivyo itakuwa viongozi wetu wanasema maneno halafu yanapotea hewani.

Mhe. Mwenyekiti jengo lile la Watoto wa Forodhani sasa hivi wa Mazizini lipo *very classic* yaani kwa mtu wa kawaida basi si rahisi kujenga nyumba au akapata watoto wakalala pahala pazuri, tunapongeza sana lakini sasa Mheshimiwa mali inapokuwa ina wenyewe inabidi ipate maelezo ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, samahani maana naona unanitizama kutokana na muda lakini nataka nizungumze suala zima la watoto, Mhe. Mwenyekiti tumeangalia takwimu Mhe. Waziri mimi nataka kusema kutuletea takwimu kwenye kitabu bado hujafanya kazi, Zanzibar mabasha wamekuwa wengi sasa hivi tena wala hawana aibu. Juzi nilikuwa katika semina na hili nilisema nitalizungumza kuna tafiti zimefanywa Zanzibar kuna mabasha wengi kweli kweli na orodha ipo, hii taasisi bado haijamaliza kazi. Lakini ningewaambia hebu nileteeni orodha ningeitaja hapa, leo una hofu mtoto wako anakwenda skuli akirudi msachi sachi Mhe. Mtumwa Kheri Mbarouk alisema hapa, kwamba leo unapokosha watoto uwasachi hii hawa watoto kila siku watakuwa wanasachiwa.

Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kustahamili mabasha wawekwe hadharani katika kesi hizi hatujaambiwa wangapi wamefungwa asilimia hata ziro waliofungwa, nampongeza sana Mhe. Asha Bakari Makame wakati alipokuwa waziri akishughulikia wanawake kuna mtu alikufa jela jina tu lilikuwa linahifadhiwa kitaki ni basha sio kitangi, tunataka Mhe. Waziri nitakutafuta baadae hawa watafiti wakupe orodha ya hao mabasha wapigwe picha watangazwe na wawekwe hadharani. Mheshimiwa Zanzibar tunafuga mabasha kwa nini watoto waharibiwe kwa sababu watu washazoea mimi nawapongeza sana *ZENJ FM*. Wana kipindi chao kile harakati za wanawake ukisikiliza kipindi kile utalia unasema kweli tuna Mahakimu sisi, tuna wanasheria sisi, tuna Polisi sisi watu wanadhalilishwa.

Kuna kesi moja kuna mtoto niliwahi kumzungumza kuna mtoto wa kike sio mtoto mdogo wa miaka mitatu ni mtoto wa skuli anachukuliwa na baba yake

anapakiwa kwenye vespa anampeleka skulie, akifika njiani anampeleka gesti yule mama alikuwa anasema anapelekwa gesti ya Bububu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan muda wako umebakia dakika mbili.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nitamaliza sasa hivi matokeo yake mtoto yule anatamka mwenyewe kwenye *ZENJ FM* mama yake analia yaani anafanya kote kote, imekuwa sawa sawa kama unakwenda Mahonda ukipitia Donge sawa sawa, ukipitia Mkwajuni sawa sawa. Lao hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa Mheshimiwa tunataka Mhe. Waziri katika miaka inayokuja kwa sababu sasa hivi bajeti ndio tunaipitisha hii ingawa kwa tabu lakini tutaipitisha, lakini mwakani tunataka tuhakikishe wangapi wamefungwa kwa ajili ya kuwadhalilisha watoto, leo hawa alizungumza vizuri Mhe. Mtumwa Kheri Mbarouk leo kama mtu anamdhalilisha mwanawe aliyemzaa huyo ni sawa sawa na mnyama sisi tunamuonea haya kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti kutokana na muda kulikuwa kuna baadhi ya mambo nilikuwa niyaseme lakini sasa nataka nimalizie moja la *SACCOS* hizi kazi hebu tuweke wazi haya mambo, kama masuala ya mikopo tunamuachia mwalimu Haroun Ali Suleiman Waziri wa Kazi hebu yale mambo yote yanayohusu fedha hizo tumuwekee yeye, leo kuna fedha ziko Wanawake na Watoto kuna nyengine ziko huku tunakwenda wapi Mheshimiwa, hebu tufanyeni kitu tunapoamua jambo tufanyeni vyenginevyo tutakuwa tunamshughulisha Mhe. Waziri, mimi nazani katika suala la *SACCOS* hizi hasa ndio za kupewa mikopo Mhe. Mwenyekiti nakuheshimu sasa hivi nitakaa, lakini kitu ambacho nakiomba Mheshimiwa sasa hivi mikopo mingi imetoka na tumeona mingi haijarejeshwa tatizo kwamba inapelekwa kwa watu ambao hawajaanza biashara.

Lao ukenda majimboni kuna vijana wanachonga, kuna vijana wanauza chips, kuna vijana wanauza maseredani, kuna vijana wa gereji hawa tunawasahau katika mikopo tunawapa watu wengine lazima pesa zitapotea. Mhe. Mwenyekiti baada ya hayo machache kutokana na muda najua umenionea huruma sana, lakini ingawa nafasi yangu ipo nitakuja kuzungumza tena siku nyengine lakini kwa kweli Mhe. Waziri namuonea huruma sana lakini ndio tuko kazini tutafanya nini.

Mhe. Mwenyekiti, nina asilimia karibu sabini au thalathini tu kama ana maelezo mazuri tutapitisha bajeti haina matatizo nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti mimi sina maelezo mengi isipokuwa naona na mimi nichangie nipate japo nusu saa hivi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ni dakika kumi tu tunatoa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsane sana Mhe. Mwenyekiti, basi naomba kumi na tano, kwanza nimpongeze Mhe. Rais kwa kuanzisha Wizara hii maalum kwa ajili ya ustawi wa jamii, kwa sababu hii Idara ya Ustawi wa jamii hii mara nyingi huwa inawekwa katika wizara nyengine kwa hivyo ule ufanisi unakuwa hauwezi kupatikana, safari hii tunamshukuru sana Mhe. Rais kwamba ameona afanye idara ya ustawi wa jamii kwa makusudi. Kwa sababu idara hii ina umuhimu wa pekee.

Mhe. Mwenyekiti lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Wizara hii kwa kitabu chake na maelezo yake aliyoyatoa humu kwa kweli tumefarajika na maelezo yake, sasa nije moja kwa moja katika suala zima la bajeti yenyewe kwa kweli bajeti hii au fungu hili la bajeti ya ustawi wa jamii halikidhi haja kulingana na uzito wa wizara yenyewe na shughuli zenyewe. Kwa kuwa tumeanzisha wizara hiyo kwa makusudi haiwezekani kwamba kiwango hiki cha bajeti inayotengewa kinaweza kukidhi hata robo ya shughuli zake, kwa kwali bajeti hii imetengewa bajeti ndogo sana na niiombe sana bajeti ijayo iweke fedha za kutosha, kwa sababu fedha zilizotengwa katika wizara hii hata ile asilimia moja ya bajeti haitimii.

Mhe. Mwenyekiti, juu ya uziato wa wizara yenyewe sisi tunaona mambo wanayoyafanya ni madogo madogo lakini mambo muhimu ambayo yanahitaji kuwa na fedha za kutosha ili tuweze kupata ufanisi unaostahiki, kwa hivyo niiombe sana serikali Waziri wa Fedha hayupo lakini bajeti ijayo mwakani hii ndio imeshakwenda tunataka patengwe fungu la kutosha vyenginevyo tutakuwa hatuelewani vizuri hapa. Tiweke bajeti ya kutosha kuona wizara hii inaweza kukidhi mahitaji ya wananchi kwa sababu hii tunapozungumzia suala la jamii maana yake ni watu, tunapozungumzia ustawi wa jamii maana yake tunazungumzia ustawi wa watu haiwezekani watu wanatengewa pesa ndogo halafu mambo yao hayendi fedha tunazipeleka katika maeneo mengine. Kwa hivyo mwakani tukijaaliwa ishaala tutakuja kukumbusha kwamba tulisema hili kwamba litekelezwe na tunaomba litekelezwe kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika Idara ya Ustawi wa Jamii mimi nimpongeze Mhe. Waziri wa Ustawi wa jamii kwa kujenga uzio pale katika nyumba za wazee wetu pale Sebleni, kwa kweli hichi ni kilio cha muda mrefu ambacho wazee wetu wale ambao tumewaweka pale kwa makusudi wamekuwa wakidhalilika na katika bajeti iliyopita nilikuwa nazungumza sana juu ya jambo hili. Lakini tunamshukuru sana Mhe. Waziri kwa muda mfupi ameweza kuondosha tatizo hili, haidhuru uzio ule haujakamilika lakini umeshafika katika hatua nzuri tunaamini kwamba katika bajeti hii utamalizika na wazee wale watapata stara ya kutosha. Kwa sababu mle mlikuwa mnaingia wezi, majambazi, wala unga,

mifugo ya Ng'ombe, mbuzi wote walikuwa ndio eneo lao lile. Kwa hivyo tunashukuru pale alhamdulillahi uzio Mhwe. Waziri ameujenga na ishaala tunajua utamalizika.

Isipokuwa moja ambalo bado namuomba Mhe. Waziri azidi kulipa nguvu ni juu ya matengenezo ya majengo yale, majengo yale yanahitaji kufanyiwa ukarabati wa kutosha kwa sababu hayako katika hali nzuri, kwa hivyo katika kipindi hiki cha bajeti kuna fedha hapa Shs. Milioni 100 zimetengwa kwa ajili ya maendeleo katika Idara ya stawi wa Jamii sielewi zimeelekezwa wapi moja kwa moja lakini mimi naamini fedha hizi pengine zimelengwa katika kuzifanyia ukarabati yale majengo si lazima yafanyiwe ukarabati yote kwa jumla kwa pamoja. Lakini tunaweza kulikamata jengo moja moja hatimae majengo yale yakakamilika na yakarejea katika hali yao ya kawaida ili wale wazee wanaoishi mle na wao waweze kuishi kama vile watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa ametueleza kwamba ana mpango katika maelezo yake katika Idara ya Ustawi wa jamii amesema kuna mpango wa kuongeza Shs. 40,000 baada ya bajeti hii, haya maelezo kidogo yamenishutua kwamba bado serikali ina mpango naomba kidogo ninukuu nimkumbushe pengine wamekosea, amesema serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango wa kuongezea wazee posho kufikia shs. 40,000 baada ya bajeti hii. Sasa haya mambo mawili yamenishughulisha kwamba bado mpaka leo ina mpango huu mpango bado haujakamilika. Sasa nataka atwambie Mhe. Waziri je bado ana mpango au amepanga katika bajeti hii watawapa wale wazee shs. 40,000 badala ya shs. 25,000 kwa sababu hii *statement* imenishughulisha kidogo, lakini amesema baada ya bajeti hii. Ina maana baada ya bajeti hii ni bajeti ijayo sasa hapa hebu atupe ufafanuzi kwamba tumetenga shs. 40,000 kwa ajili ya wale wazee wa pale katika bajeti hii au bajeti ijayo. Hilo nataka ufafanuzi,

Mhe. Mwenyekiti, jengine nizungumze kwa haraka haraka muda wako hautoshi kuna Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba kuna maslahi hapa ya wale wazikaji, kwa sababu idara hii ya Ustawi wa Jamii huwa inafanya mazishi kwa wale watu waliokufa ambao hawana jamaa zao. Kwa mujibu wa table iliyokuwepo hapa imeeleza kwamba kuna gharama za mazishi, gharama za mazishi inasema Unguja 55,000 Pemba 50,000 idadi ya maiti Unguja 25,000 Idadi ya Pemba 25,000 pamewekwa mahisabu mahisabu kidogo hapa totali imeonesha hapa.

Lakini mimi nataka kuzungumzia jambo moja mimi nimepata malalamiko juu ya hawa watu wanaoshughulikia na kuzika kwa kweli mara nyingi maiti zile zinakuwa haziko katika hali ya kawaida wamenionyesha mpaka picha zinatisha, mtua asipokuwa jasiri atashindwa hata kwenda kuzizika kule lakini kwa bahati mbaya sana wale wanaoshughulika na maiti zile wanalipwa shilingi

elfu tano kwa maiti mmoja. Pamoja na ufinyu wako Mhe. waziri lakini shilingi elfu tano kumpa mtu kwenda kuzika maiti wa aina ile ni kiwango kidogo ambacho hakilingani na hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti ukionyeshwa hizo picha ambazo hao wenzetu wanaoshughulika na kuzika zile maiti wewe mwenyewe utashtuka na ndio kwenye picha, wakati wao ndio wanaoshughulika katika hali halisi kwa hivyo nimuombee sana Mhe. Waziri kiwango cha shilingi elfu tano kwa maiti mmoja kuwapa wale wanaoshughulika na maiti ni kiwango kidogo pamoja na ufinyu wako wa bajeti lakini kiwango kile kinahitaji kiongezwe ili kiendane na wakati.

Mhe. Mwenyekiti jengine nizungumzie suala la udhalilishaji wa kijinsia wenzangu hapa wamezungumza sana katika jambo hili, na mimi nitumie nafasi kama mzazi nilizungumze kwa kweli jambo hili la udhalilishaji wa watoto kwa kweli limekuwa janga la taifa, tunahisi bado serikali haijatoa uzito. Hapa Mhe. Waziri ametueleza kwamba ameunda kamati ambayo inawahusishwa Wizara yenyewe ya Ustawi wa Jamii, inahusisha Polisi, inahusisha watu wa Afya, inahusisha Mahakama, inahusisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Katiba na Utawala Bora na washirika wa maendeleo.

Lengo la kamati hii kushughulikia masuala haya ya udhalilishaji ukweli kamati hii nadhani Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atueleze hawa wanaohusika na hili, huyo polisi ni yupi, Mahakama ni Hakimu gani anayehusika na hawa wengine wote ambao wametajwa kwa sababu tuna wasi wasi juu ya kamati hii, kamati hii haifanye kazi zake vizuri. Kwa sababu masuala ya udhalilishaji wa watoto unaendelea mimi katika jimbo langu katika shehia ya kwa wazee kuna mwalimu mmoja wa madrasa ana kazi ya kudhalilisha wanafunzi wake, juzi juzi amekamatwa akimdhalilisha mtoto wa kiume.

Lakini matokeo yake kesi yake imekwenda anaambiwa eti ana mashetani anafanya shughuli hizi kwa sababu ya mashetani, hivi kama ana mashetani kwa nini asiwafanye watoto wake waliokuwemo mle ndani ya nyumba yake anakwenda kufanya watoto wa wenziwe, matokeo yake mtu yule ameachiwa huru. Sasa kamati hii inafanya kazi gani leo mwenye mtoto anaranda na panga anasema nikimkuta nitamkata kichwa kweli tuko *serious* katika kuzuia jambo hili, kweli hii Idara ya Mahakama inafanya kazi zake vizuri, je hawa Polisi wanafanya kazi vizuri, Je, Wizara yako inafanya kazi vizuri na inasimamia vizuri katika jambo hili. Sisi tunaona jambo hili halijapewa uzito unaostahili na ndio maana jambo hili linaendelea kila siku tunaiomba sana Mhe. Waziri wizara yako kupitia hata hii kamati mliyokuwa mmeiunda kama iko *serious* katika kufanya kazi zake tuone kwamba jambo hili linakoma kabisa.

Leo watoto wa miaka miwili, watoto wa miaka mitatu wanadhalilishwa serikali ipo hakuna hatua kali zinazochukuliwa mwenzangu hapa Mhe. Salehe alisema kwamba hawa wanaofanya shughuli hii wahasiwe na mimi nakubaliana na yeye moja kwa moja, nakubaliana naye mia juu ya mia na kama kuna sheria ambayo inatakiwa ifanyiwe marekebisho ile sheria iliyopitishwa juzi basi irejeshwe tena hapa Barazani kwa sababu tunaona hizi sheria zilizokuwepo hazitoshi. Haiwezekani mtu mzima mwenye akili yake timamu akenda kumbaka mtoto mdogo wa miaka mitatu, miaka minne, miaka mitano wakati sasa hivi kuna wanawake tele humo nje imejaa. Mhe. Mwenyekiti hili jambo linahitaji kufanyiwa kazi vya kutosha vyenginevyo watoto wetu wataendelea kudhalilika.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, juu ya watoto hawa wanaoishi katika mazingira magumu kuna idadi kubwa ya watoto wetu ambao wanaishi katika mazingira magumu, ambapo idara hii ya Ustawi wa Jamii inahitaji kuwashughulikia kwa sababu hawa watoto ndio taifa letu la kesho. Leo kuna asilimia kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira magumu mitaani. Leo serikali badala ya kutenga bajeti ya kutosha kushughulikia jambo hili, matokeo yake wanaweka bajeti ambayo hata haiingii akilini. Je, suala hili la kuondosha watoto wa mitaani wanaoishi katika mazingira magumu kweli litaweza kufanikiwa.

Kwa nini serikali haitengi bajeti ya kutosha katika kuondosha jambo hili, tunawaachia wafadhili watusaidie kuondosha matatizo yetu. Hili kweli ni halali? Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninalosema narejea kusema tena bajeti hii ishapita na kwa mujibu wa Kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi hakuna fungu litakaloongezwa isipokuwa kupunguzwa. Lakini bajeti ya mwakani tukijaaliwe penye uhai tuaiangalia sana bajeti ya Ustawi wa Jamii. Kwa sababu bajeti hii ndio itakayotuwezesha sisi kuondokana na matatizo haya ya watu wetu na vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja. Namuomba Mhe. Waziri kwa yale ambayo nimetaka ufafanuzi basi anipe ufafanuzi ili niweze kuunga mkono zaidi. Sasa hivi naunga mkono kwa asilimia 95.9. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa dhati kabisa kuweza kunipa nafasi hii jioni hii ya leo. Pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri sana ambayo inaonekana haina mashaka hata kidogo. Huyu mama yetu ni lazima tumuenge enge.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba mawili matatu ambayo nitayazungumza kwa ufupi ili kuweza kufupisha muda wako ili kuweza kuwapa nafasi na wengine. Kwanza nilikuwa naomba niogelee zaidi katika

Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mimi hapa nilikuwa naomba nimuulize Mhe. Waziri ili baadaye aje anijibu suala moja dogo sana.

Katika kitabu chake kimetaja takwimu ya watoto wanaoishi katika nyumba ya kulelewa, imetajwa watoto mayatima. Miongoni mwao kuna mtoto wa Chuo Kikuu kwa mahesabu yangu ya haraka haraka. Chuo Kikuu anayejiunga anatakiwa ni mtu ambaye ana umri usio chini wa miaka 21. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kuja kufanya majumuisho anijubu huyu mtu wa miaka 21 ni mtoto yatima au kijana yatima. Kwa sababu umri wa mtoto unajulikana na kama hichi kijiji kinalea vijana yatima basi sisi tunao wengi.

Jengine ambalo Mhe. Waziri atakapokuja atanisaidia miongoni mwa hao watoto mayatima. Kwa sababu ndani ya maeneo yetu tuna watoto ambao wanaishi katika mazingira magumu. Mimi nina wasi wasi hao waliopelekwa wanaishi katika mazingira ya raha zaidi. Nataka anisaidie kama Kwahani angalau kama kuna kijana mmoja ambaye analelewa kule.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya suala langu hilo dogo amalo nategemea Mhe. Waziri atakuja kunielezea jinsi ya umri ambao mtoto anastahiki kulelewa na mimi niguse guse tu kidogo pale ambapo wenzangu wengi wemegusia juu ya mkataba wa jumba la kulelea watoto.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi naungana na wenzangu kuna haja na namsubiri Mhe. Waziri kwa hamukubwa sana aje atuletee mkataba wa jumba lile kumjua nani mmiliki halisi kwa faida ya wananchi wa nchi hii. Kwa sababu masikitiko makubwa kwa watu wetu wanasikitika mpaka wakati mwengine tunapata kigugumizi, wananchi wanatusimbulia mitaani Mhe. Mwenyekiti. Tunaambiwa watoto mmewahamisha mpaka njia mmetufungia ndio mnatupeleka wapi waheshimiwa, mnaturudisha mnakotaka. Yaani huju mnyonge apite, huku tajiri akae afanye starehe zake.

Mheshimiwa hili ni tatizo. Kama alivyozungumza Mhe. Hamza, tunapouliza masuala basi imani yetu ni kwamba serikali itasaidia na itarekebisha. Suala la njia nimelizungumza muda mrefu na tukachukuliwa ahadi hapa Mhe. Mwenyekiti, kwamba njia itafunguliwa, lakini mpaka leo bado. Hilo si lake, lakini nagusia ili kuonesha onyanyasaji wa wananchi wa nchi hii katika kutumia haki zao za busara na za msingi katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie ukurasa wa 23 Maendeleo ya Vijana. Mimi hapa napata kigugumizi kikubwa sana, kwa sababu umri wangu bado najihesabu ni kijana. Baada ya kukiangalia kitabu hiki cha Mhe. Waziri ameelezea jinsi ya wizara ilivyopanga mikakati na uharikishaji wakuunda Baraza la Vijana. Hofu yangu au masikitiko ambayo naelezea kwa wizara hii ni jinsi ya haraka hizi au

mbio wanazokwenda kwa mbio zao hatuzielewi zinaishia wapi au zitamalizika lini. Mimi nina wasi wasi Mhe. Waziri kwamba maofisa wake hawamuelezi ipasavyo ajajua undani wa hii hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili limeanza kuzungumzwa tangu mwaka 2005 wakati ilipoanzishwa sera hii ya vijana. Kitabu hiki huwa najaribu kukaa nacho sana na kukiangalia sana, kama Mhe. Waziri kama anacho akiangalia hii nembo iliyokuwepo mbele ya kitabu chake, basi hawa ni vijana wa jimbo la Kwahani na hii ni *NGO,s* ya jimbo langu. Hawa ni vijana wa *MAIDO* yaani Mikunguni *Development Organization*, Jumuiya ya Maendeleo ya Vijana wa Mikunguni, ndio walioanzisha sera ya sera hii. Ndiyo ilioainisha mikakati na katika mkakati wa mwanzo kabisa ni mkakati wa kuunda Baraza la Vijana. Sera ambayo imetumia gharama kubwa sana ya pesa za wananchi wavuja jasho, masikini wa nchi hii sio chini mioni 50 zimetumika katika kuandaa sera hii. Zilikuwa pesa za wafuja jasho na misaada ya ndugu zetu wa *UNICEF* pamoja na *UNESCO*.

Mhe. Mwneyekiti, hawa wafadhili itafikia pahala tutawakatisha tamaa, tutawarudisha nyuma na baadaye watukimbie. Wanatumia gharama lakini matokeo yake gharama zile hatuzifanyii kazi. Katika sera hii ina mikakati minane, hakuna mkakati hata mmoja ambao tayari umeshaanza kufanyiwa kazi, zaidi ya mkakati ambao sasa hivi wanaanza kuufanyia kazi ule tu wa upembezi wa sera hii kwa sababu inatakiwa kufanyiwa uyakinifu kila baada ya miaka mitano na miaka mitano tayari. Sasa huku Baraza linataka kuundwa halijafikia pahala, huku sera haijafanyiwa kazi, watu wanatafuta. Mheshimiwa hii ni hatari kubwa sana.

Nimuombe Mhe. Waziri kuwa makini katika hili ili kusaidia vijana wetu. Sera imezungumza mambo mazuri kuna mikakati mizuri ya kuwawezesha vijana kuwaanzishia mambo ya masomo, kuweza kujiajiri, kuwaondoshea umasikini, kuwapa elimu, yaani mambo yote yameelezwa, lakini hakuna hata moja, zaidi ya kutumia pesa za vikao na kuharibu pesa za nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa mchangiaji mkubwa sana kwa sababu ya muda lakini nina imani mambo haya aniarifu. Namuomba sana akirudi katika taasisi yake akayavute ayaangalie ili aweze kuyafanyia kazi. Leo na kesho kama walivyozungumza wenzangu bajeti ya mwakani basi tuje tumuulize kafikia vipi na amefanya vipi na kuna mafanikio gani kwa vijana. Vijana wa nchi hii wananyanyasika Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, naheshimu muda wako, lakini vijana wananyanyasika, hawana pa kwenda, hawana ajira, kila unapokwenda wageni wamezidi, ajira ya nchi hii mashaka matupu. Mheshimiwa nimalizie kwa kusema na mimi kwa

niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani naunga mkono kwa asilimia 90, asilimia 10 na mimi nasubiri kama wenzangu baada yakupata ufafanuzi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, baada ya kukushukuru kwa kunipa na mimi fursa hii naomba na mimi niungane na wenzangu kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake. Nampongeza kwa sababu ya kuaminiwa kupewa wizara hii ambayo ni muhimu sana inayotugusa tokea wakati ule mtu unatembea kwa miguu minne mpaka unapomalizia ukatembea kwa miguu mitatu. Bado wizara hii ipo pamoja na wewe yaani watoto mpaka wazee.

Hii ni wizara moja ambayo Katiba yetu inasisitiza majukumu yake kutekelezwa na Serikali, yaani huduma au haki za kijamii. Kwa hivyo nawaelewa sana waheshimiwa wajumbe wanaposisitiza sana kwamba fungu la wizara hii au bajeti ya wizara hii kwamba iongezwe kwa sababu majukumu yao kwa kweli ni muhimu sana.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nichangie kwenye maeneo mawili tu. Eneo la kwanza hili limezungumzwa na wengi na mimi naomba niungane nao katika uzoefu ambao nimeupata nikiwa kwenye bahati ya mambo haya ya kusimamia masuala ya uhalifu kwa miaka tisa nimefanya kazi kama mkurugenzi wa mashtaka. Nashukuru kwamba miaka hii sita imenipa uzoefu wa kumjua binaadamu.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la ubakaji na udhalilisha wa kijinsia kwa kweli ni kubwa sana kuliko hivi linavyoelezwa humu ndani na wajumbe. Wajumbea wanapotoa rai ya kwamba wahalifu au wakosaji wa wahasiwe. Mimi huwa najiuliza wahasiwe wapi. Maana tatizo lipo kwenye kichwa hichi, ndio linapoanzia. Ikiwa kichwa hiki kina matatizo basi hata ukihasi kwengine mikono ipo anayetaka kudhalilisha atadhalilisha vile vile. Kwa hivyo waheshimiwa wale wanaotoa rai ya kuhasi watueleze vizuri na mikono pia. Aliyekwisha kuharibikiwa kichwa basi hata ukimkata mikono na miguu pia. Aliyeharibika kabisa si anatumia macho mpiga bodi. Yote ni kudhalilisha (*Vicheko*).

Mhe. Mwenyekiti, tatizo sio jepesi kama hivyo watu wanavyolieleza, kusema labda *solution* ya kuhasi kwa kweli ni kulifanya hili tatizo ni dogo sana kuliko lilivyo. Mimi kwa uzoefu wangu kwenye eneo hili kwanza tujue kwamba kuna watu wengi wambo ni wagonjwa lakini hatuwatii katika hesabu ya ugonjwa. Katika eneo hili kwa mfano hapa kwetu bahati nzuri ugonjwa huo haupo. Lakini ukisoma katika *literature* za mambo haya ya ugonjwa unaopelekea watu kufanya vitu vya ajabu kuliko hata mnyama. Maana yake kusema watu wanafanya kitendo cha kinyama mimi nasema ni kuwaonea wanyama. Maana

yake mnyama hamchukui mtoto wa mwaka mmoja akamfanyia hivi ambavyo binaadamu anamfanyia. Sasa leo mtu huyu ukimwita mnyama kwa kweli unamuonea yule mnyama kwa sababu mnyama hafanyi hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tatizo hili ingawa tunaliona kama limeanza sasa hivi. Lakini kwa kweli ukisoma kwenye historia ya nchi yetu katika uhalifu hili tatizo lipo mda mrefu. Hawa aliowataja Mhe. Hamza mimi siwezi kuwataja, basi ukisoma wapo wengi tokea miaka ya nyuma tatizo hili lilikuwepo. Lakini sasa hivi kwa sababu tunalizungumza sana linachangia kuonekana kwamba tatizo ni kubwa zaidi.

Tatizo jengine la pili ni kwamba sasa hivi alilieleza vizuri Mhe. Mtumwa alipokuwa anachangia kwamba kuna mambo mengi, kuna suala la malezi. Lakini suala pia la ulimwengu wa sasa hivi. Kwa sababu sasa hivi ukisoma gazeti mpaka la serikali kuna siku maalum huamua kati kati ya gazeti utakuta picha za warembo, lakini ukijiuliza urembo ni kitu gani? Ni hivi walivyovaa? Gazeti linakushinda kuchukua nyumbani. Ukilichukua nyumbani basi inabidi labda ile kurasa ya kati kati uitoe. Kwa sababu ukianza kuwa vijana wa miaka 13, 14 ambao wameanza kushtuka shtuka akiliona lile hana pa kukimbilia basi atakimbilia kwa watoto wenzake.

Mhe, Mwenyekiti, sasa hivi inasikitisha sasa hivi kesi ni nyingi zinatokea za watoto kwa watoto wenzao. Hili tulione ni moja katika tatizo na si tatizo ambalo tunaweza kulishughulikia kwa kupitia njia ya sheria peke yake, lakini ni kwa ujumla wake. Kwa hivyo tunaweza tukamlaumu waziri, tukailaumu Kamati.

Jengine mimi nataka kuungana nalo ni kwamba tunapolipeleka katika vyombo vya sheria, niungane na waheshimiwa wajumbe kwa sababu nikisema kwenye vyombo vya sheria kunauwadilifu nitakuwa nalidanganya Baraza hili na nitakuwa nawadanganya wananchi. Kwa kweli tatizo la kukosa uwadilifu katika vyombo vya sheria nalo linachangia kwa kiasi fulani katika tatizo hili vile vile.

Lakini kwa upande mwengine hata katika vyombo vya sheria wapo wengine waadilifu na kesi nyengine nzuri, zinakwenda na watu wanatiwa hatiani. Lakini ikifika katika ngazi ya sheria pia kuna sababu nyingi zinachangia kesi hizi kuharibika. Moja katika mambo yanayochangia ni tabia yetu sisi wenyewe katika jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni pahala peke yake ambapo mtu anaweza akaja, akakufata, akakuomba kesi ya mtu kabaka mtoto mdogo. Analalamika

anaomba kwamba kesi ile kwa sababu tu aliyefanya kitendo kile ni jamaa yake wala haoni haya kuja kuomba kwamba yamalize.

Vile vile mambo haya yanatokea ndani ya jamii. Kesi nyingi za udhalilishaji za ubakaji zinakuwa ndani ya jamaa, ndani ya famili au ndani ya ndugu wa karibu. Hivyo inachangia kwamba watu wanazifanyia suluhu wenyewe katika ngazi ya kifamilia.

Binafsi yangu nina maafisa wengi katika Afisi niliyokuwepo zamani wameshagombana na watu wengi kwa sababu ya kukataa kesi hizi kuzifuta, lakini mtu anafika pahala anakwambia hatuji Mahakamani. Na kweli hawaji na akija Mahakamani kweli kesi hiyo ataiharibu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla kwenye tatizo hili mimi naomba na ninachoomba zaidi kwamba tushirikiane zaidi katika nyanja zote kupambana na tatizo hili. Kwa kweli tatizo hili ni kubwa hakuna njia ya mkato katika hili.

Mimi katika hili niseme tu zile baadhi ya juhudi za serikali Mhe. Waziri alilieleza. Moja tulikuwa tuna tatizo la ukosefu wa utaalamu katika kuzishughulikia hizi. Kwa mfano unapopeleka kesi hii kwa daktari au kwenda kufanyiwa uchunguzi wa kidaktari mara nyingi au huko tunakotokea akifika kwa sababu hili ni jambo linalohitaji utaalamu maalum wa kufundishwa. Mara nyingi ni madaktari wetu wengi kwa sababu hawakuwa na mafunzo maalum ya kushughulikia hili akifika mtu anaingia mvunguni kuanza kutafuta tatizo lipo pahala gani.

Kwa taratibu za kitaalamu kwanza ni kumuhoji na kumuangalia sehemu mbali mbali kabla hujenda huko sehemu ambako kumeathirika. Kwa sababu uchunguziukifanywa vizuri unatoa ushahidi mzuri zaidi wa kuunganisha kuliko ushahidi wa kuangaliwa huko ambako kunadhaniwa kwamba kumeathirika. Hilo kwa kweli lilikuwa halifanyiki.

Kwa sababu ya kuliimarisha hili ndio maana ofisi niliyokuwepo tulifanya juhudi maalum ya kutayarisha kitu tunakiita *standard operate procedure* ya kushughulikia mambo haya. Tukatafuta mtaalamu, akatuandalia muongozo yaani *manual* maalum ya kutumika na madaktari, polisi, *prosecutor*, pamoja na Mahakimu katika suala hili. Muongozo ule najua sasa hivi iko. Baadaye madaktari takribani wengi wanaoshughulika na suala hili wakaitwa, wakafunzwa na wakaelekezwa na sasa hivi muongozo ule upo katika hatua ya kuchapishwa ili ugaiwe kwa wahusika. Ni sehemu ya juhudi ambazo mimi naamini kwamba zitaweza kusaidia katika kupambana na suala hili. Mimi wito wangu ni kwamba jamani kwenye hili hakuna njia ya mkato, si ya kuhasi, si ya

kukata kichwa, wala si ya kitu chengine. Dawa ni lazima hivi ni vita tupambane katika sehemu mbali mbali.

Jambo la pili ambalo lilizungumzwa na ambalo nikiri sina taarifa ya kutosha sana, lakini ninayo taarifa kidogo, kuhusiana na nyumba ya watoto yatima. Sijui wasi wasi inawezekana wa waheshimiwa wajumbe ni wa msingi sana, kwa sababu wameona limechelewa labda. Mimi ninavyofahamu ni kwamba halijachelewa kwa sababu kuna tatizo. ama la *foul play*, ama kufichwa kitu, ama kudanganywa, ama kupendelewa. Kwa kadri ninavyofahamu suala hili kwa maelezo niliyoyapata ofisini kwangu ambapo sio bado sio mwenyeji sana ni mpya mpya.

Mhe. Mwenyekiti, *ZAYEDESA* walijenga nyumba ile sio kwa pesa zao isipokuwa na wao kwa kutumia wafadhili mbali mbali wamejenga jengo lile. Unapokuwa ufadhili kunakuwa na masharti yake ya namna gani ya kutunza kile unachopewa. Unapotaka kumpa mwengine akitumie pia kunakuwa na masharti yake. Jengo lile sasa linapotaka kupewa Serikalini, kukabidhiana ni kwa mkataba maalum, ambayo kuna baadhi ya masharti ambayo yatalinda wale waliotoa pesa kuchangia katika ujenzi ule, kuona kwamba yale malengo yao yanaendelea kutimizwa.

Kwa sababu hiyo ililetwa rasimu ya mkataba na Ofisi yetu kwa kuzingatia maelewano au nia ya makubaliano yale ndio imetoa maelekezo ni vyema Wizara na *ZAYEDESA* au ushauri tunaita. Wakae baadhi ya mambo wakubaliane ili yawekwe wazi katika mkataba ule baadaye isije ikawa tatizo. Mimi sioni kama hilo limechukua mda, mimi nadhani ni jambo la kutupa mda kulimaliza. Lakini halijafika pahala pa kutiliana mashaka wala pa kutiliana wasi wasi. Mhe. Mshimba nadhani anasikia. Kwa kawaida ananiamini maana mimi na yeye tuna mpango nimuombee uwakili. Kwa hiyo mimi naomba nimuhakikishie kwamba haijafika pahala pa kutiliana wasi wasi wala pa kudaiyana nyaraka wala mikataba. Ni utaratibu wa kawaida na naomba mimi aniamini kwamba tutakapoukamilisha basi atakuja kuona, kama atapiga *photocopy* anatachukua. Mimi nimuhakikishie na niwahakikishie wajube wote ambao wana wasi wasi juu hili. Kwamba ni kwa sababu ya *back ground* hiyo.

Hili si jambo ambalo mimi nadhani tumkwamishe Mheshimiwa mama yetu kwenye bajeti yake kwa sababu ya hili. Kwa sababu hawajibiki yeye peke yake katika hili na katika kulinda maslahi ya upande wa serikali. Lakini na maslahi ya hawa ambao waliyofanya jambo hili kwa nia njema na wao pia kuwalinda kwa sababu waliaminiwa wakati wa pesa za watu mpaka ndio nyumba ile tukaiyona leo ipo vile ilivyo. Kwa hivyo ni vizuri haya masharti yakawekwa bahati, yakawekwa wazi, ili hawa watoto wetu mnaowaweka pale wasiishi kwa

wasi wasi, wala siishi kwa kuuliza, kwani hii nyumba ya nani? Nani mwenye dhamana? Mimi labda kwa hili niseme hilo tu.

Kwa kweli niipongeze kwa dhati kabisa *ZAYEDESA* kwa sababu mazingira ya pale Forodhani yaliyokuwepo, kwa sababu sasa hivi utalii umehamia pale. *ZIFF* ni pale siku hizi kuna *ZIFF* kubwa na ndogo na watu wanatoka dunia nzima kuja pale. Hakuna nadhani mtu yeyote angependa mtoto wake aishi katika maeneo yale pale kwamba ndio makaazi yake. Kwa hivyo, juhudi ile iliyochukuliwa mimi nadhani ni ya kuithamini sana na kwa kweli tuipongeze na tuishukuru sana *ZAYEDESA* kwa kufanya hili. Naomba kwa hili basi mtuamini kwamba tutalizimamia, tutalishughulikia kuhakikisha linakuwa vizuri na litakapokuwa tayari, litakapokamilika basi tutakuwa na fursa ya kuliangalia na kuweza kujua kama kuna makosa. Kwa sababu si mkataba ya mauziyano kwanza ni mkataba wa kukabidhiana. Kwa hivyo, mnaweza ukarekebisha chochote, mnaweza mkatoa maoni, mnaweza mkatoa fikra wakati utakapofika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja na niwaombe sana wenzangu kwamba tumfanyie wepesi mama yetu hizi pesa azipate kwa haraka ili aende akafanye kazi. Sote tunamjua *spirity* yake ya kazi na ari yake ya kufanya kazi. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nitajaribu kwa kiasi fulani kujibu baadhi ya hoja za waheshimiwa kusaidia inaweza ikawa nisiwe na jawabu la moja kwa moja. Lakini na mimi nitangulie kushirikiana na wenzangu wote kumpongeza bi Zainab sana na kumpa pole kwa kuondokewa na Katibu Mkuu wake. Lakini pia nimpongeze kwa kupata Katibu Mkuu mwengine na timu yake ni nzuri kwa ujumla. Naamini kwamba masuala yanayohusiana na vijana, watoto na wanawake yamefika ndipo.

Mhe. Nikipongeze sana kitabu cha Bajeti ya Mheshimiwa. Nataka nizungumzie kidogo baadhi ya masuala ambao yamejitokeza na labda nianzie na hili alilolizungumza Mwanasheria Mkuu, kuhusiana na jengo lile. Bahati nzuri na mimi ninaelewa kwa kiasi Fulani naamini ndiye ambaye niliyeombwa kile kiwanja cha pale Mazizini nikitoe, nikiwa Waziri wa Elimu kwa wakati ule. Lakini kwa lengo la kuwaondosha pale penye eneo lile ambalo kwa kweli maadili na mazingira ya pale yasingeweza kabisa kukidhi mahitaji ya vijana wetu kuwepo pale.

Mhe. Mwenyekiti, wakati natoa kiwanja kile niliwahi hata kutania nikasema basi mimi nitaoa kiwanja kile halafu lile jengo nitalitumia kwa ajili ya *library*

ya Wilaya ya Mjini. Lakini baadae kwa vile tulikuwa tuna maandalizi ya kujenga jengo letu jipya la maktaba pale Eacrotanal nashukuru tukajenga *library* yetu na imekamilika na inatumika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni makubwa ilikuwa jengo lile nakumbuka na Mhe. Hamza nae amelizungumza pale kwamba Mhe. Rais Karume alilizungumza hadharani pale, baada ya maneno mengi na mazungumzo mengi. Akasema leo nimefurahi sana kwamba leo nalizungumza jambo hili kwa sababu kulikuwa na maneno mengi yakizungumza. Pia akatoa ushauri akataka Mamlaka ya Mji Mkongwe wafanye utaratibu za kuweza kulitumia jengo lile la Forodhani ili litumike kwa ajili ya *medical museum*. Alitaka taratibu hizo ziendelee sasa siwezi kusema mpaka sasa hivi taratibu hizo zimefika wapi. Lakini hayo ndio maelekezo ambayo yalitolewa wakati ule na sidhani kama kuna mengine sikumbuki kama kwenye kikao chochote kama tulizungumza masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, jengo lile ambalo limejengwa pale lilisimamiwa na *ZAYEDESA* na michango waliotoa ni wengi kweli sio wale tu ambao tunawafikiria labda walitoa pengine kwa sababu fulani au kwa madhumuni fulani. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba makampuni mbali mbali yalisaidia na jengo lile liko chini ya Mamlaka ya *ZAYEDESA* sasa hivi ndio waliopewa walisimamie. Kwa hivyo, kama kuna maamuzi mengine ambayo tunatarajia yatafanywa basi hayo yatakuja baada lakini kwa sasa hivi ninavyojua kwamba jengo hilo liko chini ya Mamlaka ya *ZAYEDESA*. Kwa sababu na waliochangia walikuwa ni wengi hatuwezi kukidhi mahitaji ya mtu mmoja tukasema huyu kachingia basi badala yake apewe hili hapana, isipokuwa kila mmoja aliyepeleka mchango wake pale amesaidia kwa njia mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, la pili limezungumzwa sana suala la udhzalilishaji wa watoto na Mhe. Hamza amelizungumza kwa hamasa kubwa sana, na hakuna sababu ya kumzuia na Mwenyezi Mungu amemjaalia ana kifua cha kuzungumza. Lakini turudi nyuma Mhe. Mwenyekiti, kwamba maadili, mitaani, vijijini na majumbani kwetu vile vile. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa mimi nilipokuwa Waziri wa Elimu nilipiga marufuku matumizi ya simu za mkononi kwa wanafunzi wa skuli, lakini pia nikapiga marufuku wanafunzi mwisho saa mbili za usiku kutembea au kwenda *tuition*.

Mhe. Mwenyekiti, wazazi nilitegemea wangetupa mashirikiano makubwa sana katika jambo hili, lakini mtoto anarudi nyumbani saa tatu au saa nne au tano kisingizio eti anakwenda *tuition*. Ni kwamba maelekezo ya serikali yalikuwa yameshatolewa kwamba mwisho saa mbili. Kwa hivyo, katika jambo hili katika ulinzi wa maadili yetu kuna kila sababu ya kulinda maadili yetu na sisi wazazi vile vile tulipozikamata simu zile baadhi ya simu tulizikamata tukazifungua

simu zile kwenye maeneo yanayohusika, Mhe. Mwenyekiti, mambo ambayo tuliyaona ndani yake huwezi kuamini kwamba mtoto wa darasa la saba au la tisa anaweza kuwa nayo.

Ndio kwanza mengine tuliyaona humo, lakini kuna mheshimiwa mmoja alisema mzee alijifunga taulo yake alikaa ukumbini anatizama picha ambazo sio nzuri basi maji moto yalikuwa yanachemka akaona akajitie maji. Mhe. Mwenyekiti, watoto walipoingia wakaona picha zile wakaa kitako kilichofanyika ni nini? Baba anatoka bafuni na ile taula akasema nyinyi watoto mnatizama nyinyi akavua ile taula akaweka juu ya TV. Kwa hivyo, hapo yakawa mengine basi ikiwa na sisi wazazi hatuko waangalifu tukasaidiana katika malezi haya ya watoto bado Mhe. Zainab tutampa jukumu kubwa sana peke yake haliwezi ni jambo la jumuiya nzima, kila mmoja alee kwa upande wake. Mhe. Mwenyekiti, mambo haya sasa hivi yameingia katika kiwango kikubwa sana tena yanatisha haya.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2001 nilikuwa Waziri dhamana wa michezo na nilikuwa na dhamana ya utamaduni, tukenda kwenye sherehe za Mapinduzi Bwawani kwenye taarab Waziri Kiongozi Mstaafu ndiye mgeni rasmi, mimi ndiye Waziri wa Utamaduni nimekaa naye pembeni nangoja taarab iimbwe pale, nyimbi ya kwanza ikenda vizuri, ya pili wakaanza kuingia kina mama nguo zimepasuliwa mpaka huku. Mhe. Mwenyekiti, badala ya kutizama waimbaji tunatizama wale wanaocheza pale, amini Mhe. Mwenyekiti, lakini tokea siku ile sijenda tena kwenye taarab mpaka hii leo.

Niliposema kwamba ni marufuku kwa kina mama kwenda kwenye taarab za viongozi wakuu wa kitaifa wakiwa wamevalia nguo kama zile hatutoruhusu aina yoyote ya nguo kama zile kwenda mbele ya viongozi kama wale na kucheza pale mbele. Nikaambiwa kwamba nimekuja Mjini kwa kufuata mwenge maana yake mshamba. Kwa hivyo, sikuwajibika tena kuyaendelea kuyasemea.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ndio maadili yenyewe yalivyo hali imefika kama hiyo watoto wanavaa nguo hizo, wazee pia wanavaa. Mhe. Mwenyekiti, zamani ndugu zetu wale wa Kibaniani wanavaa zile sari na matumbo yanakuwa wazi, lakini sasa hivi wamekuwa wengi zinavaliwa mpaka hapa chini kunakuwa wazi na jamii tunaiona.

Kwa hivyo, hili jukumu ni letu sote na naomba nimpongeze sana Dk. Ali Mohammed Shein ameunda kamati maalum kwenye Baraza la Mapinduzi kumsaidia Mhe. Zainab na katika kamati hiyo Mhe. Abubakar Khamis Bakary yumo, Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban yumo, Mhe. Juma Duni Haji yumo, Mhe. Haji Faki Shaali yumo, Mhe. Machano Othman Said yumo na Mhe.

Haroun Ali Suleiman yumo. Sote kwa lengo la kuangalia njia gani tunaweza tukafika tukaweza kuzuia wimbi hili la udhalilishaji wa watoto. Kwa hivyo, serikali imejidhatiti na imefanya kazi yake kwa upande wake na tunaendelea. Lakini kama alivyosema serikali imejidhatiti na imefanya kazi yake kwa upande wake na tunaendelea. Lakini kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu hapa hili jambo hakuna *magic formula* ambayo tunaweza tukaitumia tukasema leo litamalizika. Tunahitajia kutumia busara na hekima ili kuelimisha jamii mpaka tufike mahali ambapo ni muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, jengine mimi sitaki kuzungumzia suala la jengo kwamba Mhe. Zainab tumemuhamisha pale, hayo ni maamuzi ya serikali wala sijatoa kauli hiyo mimi tulikuwa tunashirikiana, tunafahamiana, tunazungumza vizuri na Mhe. Waziri. Siku hiyo akaja kunambia Mhe. Haroun mimi nahama nakwenda zangu kwenye jengo jengine, mimi nikamuuliza wapi? Akaniambia nitashirikiana na Mhe. Haji Omar Kheir nikamwambia hongera na kweli *furniture* za kule ni nzuri, amepumzika pazuri na upepo wa pwani mzuri. Kwa hivyo, ndio maamuzi ya serikali wala hakuna haja ya kuyahoji kwa sababu hayana ubaya yalikuwa yana nia nzuri tu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la ajira kwa vijana na mikopo ya vijana. Mhe. Hamza anasema ni vizuri masuala haya yakawa *centralize* mahali. Mimi nadhani ni suala la *coordination* tu lakini hakuna matatizo, ni suala zuri popote pale lilipo la muhimu ni kuweza kushirikiana na wenzetu katika njia mbali mbali. Mhe. Mwenyekti, wao wanawawezesha vijana kwa upande wao lakini wizara yetu inawawezesha wa rika zote, wawe vijana, wanawake na watoto wa aina zote popote pale walipo, hilo ndio jukumu la wizara yetu kwa kushirikiana na Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu afya na usalama kazini tumelizungumza wapo waliomia ambao wanahitajia kupata pengine fidia ya kuumia kwao, hili itabidi serikali ilifanyie kazi kwa sababu hii ni idara mpya sheria yake ilipitishwa tokea mwaka 2005. Kwa hivyo, tumeanza kuitumia sasa hivi kwa sababu Rais Dk. Ali Mohammed Shein ndio ameanzisha idara hii mpya na tunaifanyia kazi sasa hivi. Kwa hivyo, yale ambayo yatatokeza katika kipindi hiki ndio yale ambayo tutashirikiana kwa pamoja kuhakikisha wale ambao wanaumia kazini kwa kushirikiana na wenzetu na wizara zinazohusika kwamba wanapata haki zao pale.

Ndio maana yake tukahimizana sote pamoja na sisi tuliokuwemo humu ndani zana za kuweka usalama wa afya za wafanyakazi wetu ni muhimu sana popote pale walipo. Mhe. Mwenyekiti, wanapopata matatizo wakidai kwamba hawakupewa zana zile tutakuja kujiingiza kwenye matatizo. Kwa hivyo, naomba sana tulione hili na linashughulikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi pamoja na kumsaidia Mhe. Waziri lakini pia nikiwa Mwakilishi wa jimbo lile nampongeza sana Mhe. Waziri na kuunga mkono hoja ya Mhe. Waziri na sote naomba sana tumuunge mkono Mhe. Waziri kwani ni mama yetu, mzoefu wa kazi tusimuwekee vile viatu vya raba leo hata tusive viatu wala tusimuhangaishe sana. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimpongeze Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Nampongeza kwa sababu ya kazi yake nzuri aliyoifanya yeye pamoja na watendaji wake na kutupa mwelekeo ambao unatupa matumaini hasa sisi wanawake kwa mifano mingi tu iliyoko hapa. Nimenukuu mifano miwili mitatu ambayo ninaiona kwamba hii kwa kweli kama tutaisimamia vizuri kweli wanawake wanaweza wakapata maendeleo. Pia kuna mifano ambayo ni ya vijana iliyotolewa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na mifano pamoja na pongezi zake, nimeangalia mafunzo kwa kweli Mhe. Zainab kwenye takwimu zake kuna wanawake wengi waliosomeshwa ukilinganisha na wanaume. Kwa hivyo, hii nafikiri ni mfano mzuri kwa wizara ambayo ya wanawake anapotambua ule umuhimu wa kuwapa wanawake nafasi ya kusoma. Mimi ningependa na wizara nyengine sote tuige hivyo angalau kwa uwiano ulio sawa ikiwezekana.

Mhe. Mwenyekiti, ningependa nimpongeze kwa kuliangalia suala la vikundi vya wanawake vilivyopo kwenye Mawilaya na kuvikusanya ili aweze kujua wapi aelekeze misaada yake. Hili naliona ni la msingi na kwa zile Wilaya ambazo ziko nyuma nafikiri wajitahidi kwa sababu fursa iko hapo na ndipo itakapotokea kwa hiyo kama watakuwa hawahamasishi wanawake hao kufanya vikundi wajue kwamba wanawanyima fursa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, chengine ambacho nimekiona kizuri kwa vijana wa Mjini Magharibi kwani Mjini ndio Mjini ni kwamba wamepima ukimwi wengi, wanaume lakini ndio wengi kuliko wanawake. Mimi nafikiri wanawake na sisi tujitokeze maana tukiangalia takwimu za ukimwi za nyuma wanawake ndio walikuwa wengi, ingawa hapa hakupatikana hata mmoja. Lakini pia ningependa na wilaya nyengine nazo ziige mfano huu kwa sababu nafasi ya kutibiwa ipo na tuitumie fursa hii kuliko kukaa na matatizo tuliyonayo. Kwa hiyo kwa hilo pia napenda nimpongeze.

Pia napenda nimpongeze kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuelimisha jamii ni vipindi vingi vimetolewa kwenye redio na kwenye magazeti. Kwa hivyo, hayo ndio yanayonifanya nimpongeze Mhe. Zainab.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka nitoe ufafanuzi wa suala moja tu ambalo Mwanasheria Mkuu wa Serikali amelizungumzia kuhusu suala la uzalilishaji na jinsi gani kuna baadhi yetu sisi tulilaumu kwamba hatutendi vizuri labda tunasababisha matatizo. Lakini nafikiri yeye alisema vizuri tu kwamba kule sasa hivi kilichoanzishwa ni *One Stop Centre* ambayo iko Mnazi Mmoja Hospitali. Hiki ni kituo cha mwanzo cha mfano ambacho kimeanzishwa baina ya wizara yake, Wizara yetu ya Afya, Askari Polisi na Wanasheria.

Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma malalamiko mengi yamekuwepo ya kesi kama tulivyokwisha kuzisikia na udhalilishaji na mambo yalivyokwenda. Lakini ni tegemeo letu kwamba *One Stop Centre* itakuwa ni moja ya utatuzi wa tatizo hili, kwa sababu walioko pale ni wanawake ambao wanaumwa na haya ambayo yanayofanyika. Mhe. Mwenyekiti, tuna daktari mmoja mahiri kweli kweli na ukenda pale ukianza kuzungumza anachachatika kuhusu hili, anaumwa na ameapa kwamba atalifanyia kazi na atahakikisha.

Mhe. Mwenyekiti, watu wengine ambao kwa kiasi kikubwa wanalifanyia kazi tatizo hili ni *ZAFELA* tuna wanasheria wanawake ambao wamejitolea kwa hili, kuna na wanawake polisi wana na umoja wao nao hawakubali kudhalilishwa. Kwa hivyo, kuna na watu wa kuhamasisha pale, kuna na watu wa kutoa ushauri nasaha wote hao ni wanawake. Kwa hivyo, kama hao ni wanawake ambao wenye dhamana tofauti imani yetu kwamba sasa hivi labda hili linaweza likaleta ufumbuzi. Mhe. Mwenyekiti, lilokuwa linakosekana kama alivyosema Mhe. Mwanasheria hata mimi hilo ndilo niloliona ni uelewa kwa sababu mafunzo ya hawa watu hayakuangalia hilo.

Kwa hiyo wanapopelekewa matatizo kama haya uamuzi waliokuwa wakiusema ndio huo. Lakii kama alivyosema kwamba kuna *standard operating procedure* kwa hiyo hilo tutachukua jukumu kuhakikisha kwamba wote tunawafundisha ili waweze kuzifanya kazi hizo kwa ufanisi na hili tatizo liweze kupungua au kumalizika kabisa ikiwezekana. Lakini katika watu waliokuwa wametajwa jana hapa *NGO's* nataka nijipongeze mimi mwenyewe kwanza kwa sababu mimi ni mwenyekiti pale. Lakini nataka nijipongeze kwa sababu gani? Kwa sababu tumeshafanya kazi na Wizara ya Wanawake na Watoto kuhusu suala la kuwatoa watoto katika kazi zenye ajira mbaya na ni watoto wengi tumewatoa watoto wasiopungua 200 tumewarejesha skuli, tumewasaidia, wazee wao tumewapa uelewa, tumewapa vitendea kazi. Na hiyo kazi tuliifanya kwa pamoja na wao.

Kwa hivyo, nafikiri hatuko pabaya, kitu ambacho nilikihisi tangu jana tukifanye kwa kusaidiana kwa hili ni hili suala la uzalilishaji wa watoto kwa sababu mimi huwa najiuliza nimejaribu kuangalia hizi takwimu za juzi kwenye ripoti tuliyopewa hili suala linaonekana kwenye takwimu hizi Kaskazini, mimi

najiuliza huko Kaskazini kuna nini? Mnataka kuniambia huko hakuna tatizo maana hata ukiangalia mjini basi njia ile inayotokea Kaskazini ndio kwenye matatizo makubwa, hivyo najiuliza ni watu wa Kaskazini ni watu walioko Kaskazini.

Mimi nikiliangalia tulipokuwa tunatafuta tatizo la watoto wenye mazingira magumu kweli kule kuna watoto wengi walikuwa kwenye ajira hatarishi, na kama watoto wanahangaika kutafuta ajira na wenye dhamira mbaya ni hiyo hiyo nafasi wanaweza wakaichukulia. Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia takwimu nakuta hata uzazi wa mpango kule kidogo bado ni tatizo, kwa hiyo kunazaliwa watoto wengi na wazee wanashindwa kuwamudu.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kule kulikuja kukaingia tatizo Nungwi watu waliokuwa wanatoka Tanzania Bara kule kuna watu waliachwa kwa sababu ya wanawake wa Bara. Kwa hivyo, wanawake wakaachiwa shughuli na watoto wadogo. Kwa hivyo, tatizo lipo kinachotakiwa ni kufanya utafiti, sisi kama Wizara ya Afya tuko tayari kushirikiana na wizara hii kwani uwezo tunao, nia tunayo tutasaidiana na mama kuhakikisha kulifanyia utafiti hili suala ili tujue wapi tutalipatia ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda niunge hoja hii mama Zaynab hatuna tatizo na mimi sina wasi wasi kwa sababu mimi sijaliona hapo la kukwamisha nakuombeni Waheshimiwa Wawakilishi tusaidiane ili tumpitishie mama yetu na tukafanye kazi nae pamoja. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia nafasi ya kusema katika wizara hii muhimu, Wizara ya Ustawi Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri, naiunga mkono Mhe. Mwenyekiti, kwa asilimia mia moja. Mhe. Mwenyekiti, nimesema kama sitosema chochote itakuwa sijaitendea haki wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunatambua umuhimu wa wizara hii na kazi muhimu na kubwa ambayo imepewa. Mimi nataka niishukuru sana katika jitihada anazozichukua za kuhamasisha uundwaji wa vikundi kwani kuna vikundi vingi sana katika Jimbo la Fuoni. Namshukuru Mhe. Waziri kwamba miongoni mwa vikundi hivyo wengi ni wanawake, na tumekuwa tukishirikiana vizuri na wizara hii Mhe. Mwenyekiti, na hatimae tulipokwenda katika mabanda ya maonesho ya sabasaba basi banda lile lilifurika wanawake. Nampongeza sana kwa jitihada hizo kwa kuhamasisha na kwa kweli wamehamasika.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 26 kifungu cha 57 nimshukuru tena Mhe. Waziri kwamba katika kipindi hiki kifupi cha miezi sita lakini ameweza

kuandaa ziara ya Mhe. Rais kuja kutembelea kikundi cha uzalishaji na uhifadhi wa maziwa ya ng'ombe kikundi hiki kiko Fuoni. Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa jitihada anazochukua na hatimae kikundi hiki kimeweza kuimarika. Najua ameshirikiana na taasisi nyingi zikiwemo taasisi ya *PADEP* ya Wizara ya Kilimo na kupitia kwake Mhe. Waziri wa wizara hii basi salamu pia zifike kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, pesa zilizotumika sio kidogo lakini na elimu aliyowapatia vijana wetu pia sio ndogo ni elimu kubwa, tukifika pale mheshimiwa tukiangalie jitihada ambazo zijana wetu wameweza kuelimika na wanazalisha maziwa katika hali ya usafi kabisa. Kwa hivyo, nilisema nisimame kumpongeza Mhe. Waziri na kumshukuru sana kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kiambatisho Nam. 9 (a) nimejaribu kupitia sana nikakuta Mhe. Waziri amefanya kutembelea vikundi vingi sana Unguja na Pemba. Lakini sijaona kama wametembelea katika Wilaya Mjini wala Wilaya ya Magharibi kwa hiyo nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kama bado hajatembelea vikundi hivi kwa sababu sijaona kuoredheshwa hapa zimeorodheshwa tu Wilaya ya Kaskazini "A" na "B", kuna Wilaya ya Kusini na Wilaya ya Kati na Pemba pia ni Wilaya zote. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri katika kipindi hiki wafanye kuvitembelea vikundi hivi kwani pamoja na kuhamasika lakini bado kuna changamoto nyingi tungependa tuweze kushauriana na kushirikiana ili hatimae vijana wetu hawa waweze kufikia malengo ambayo tumeyakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema sitokuwa na mengi labda nikazie tu pale ambapo masikitiko mengi ndani ya Baraza hili limekuwa katika suala zima la unyanyasaji wa watoto. Wakati mjadala huu unaendelea jana nimepata ugeni kuja kulalamikiwa kwamba tuzungumzie kwa nguvu zote suala hili la huyu Ustadh ambaye amemnyanyasa mtoto mdogo ambaye ni mwanafunzi wake mwenyewe. Lakini walikuwa wanaomba kwamba pamoja na kwamba wamekata rufaa waelekezwe utaratibu wa kupita ili isiwe kwamba imetupiliwa mbali kama ambavyo yule Hakimu amesema kwa sababu ushahidi wote upo na kila kitu kilionekana bayana, japokuwa ilifanywa *delay tactics* Mhe. Mwenyekiti, kwamba suala hili limechukua karibu miezi mitano, lakini hatimae wakajawakaambiwa kwamba hakuna ushahidi na kama mambo mengine tulivyoyasikia ndani ya Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba kesi hii ni moja lakini ziko nyingi za aina hii, sasa watu kama hawa mimi nilikuwa nafikiria kwa upeo wangu mdogo wa masuala ya kisheria. Hivi akishaamua Jaji iwe ndio basi tu uhuru wa Mahakama hata kama kuna ushahidi tosha, hivyo watufikishe pahali basi na hii Mahakama nayo iwekewe chombo cha kukiangalia. Kwa sababu haiwezekani

Jaji mmoja akasema kwamba hakuna ushahidi basi sote tuseme ndio hakuna ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa wanaonyanyaswa kijinsia kwa kweli wanapata taasira ya kiakili katika ukuaji wao, inawaharibia maisha yao moja kwa moja, inawapunguzia ukuaji kwa kiasi fulani, lakini pia na ile haiba ambayo kama wangekuwa nayo pia inapungua kwa kiasi kikubwa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Waziri tumsaidie ili tuweze kubadilishana nae mawazo katika hili tufanye nini, maamuzi kama hayo yanapopita yasiishie hapa lakini tuone jinsi ambavyo hatimae wazazi wa watoto wa aina hii wanaweza wakatendewa haki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina zaidi lakini kwa kulinda muda wako na kwa kuwa unataka tujumuishe leo basi na mimi nirudie tena kusema kwamba kwa niaba yangu mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Fuoni ambao wameniamini na kunichagua kwa kura nyingi sana basi tunaunga mkono hoja hii kwa asilimi mia moja na naomba pasiwe na buti tumpitishie mama yetu huyu, lakini tumsaidie.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipatia tena nafasi hii, lakini pia naomba niseme kwamba Baraza lako tukufu limeonesha kwamba lina imani na mimi sana, imani hiyo imejionesha katika michango yao kila anayesimama anaunga mkono hoja hii. Kwa hivyo, mimi nashukuru sana kwa hilo, sana kabisa na nina imani kwamba ndugu yangu pale ambaye tulikuwa kwenye Baraza hili kipindi kirefu Mhe. Hamza Hassan Juma atakubaliana na mimi juu ya hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nikianza nataka niseme kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, napenda kukushukuru tena sana wewe mwenyewe na Baraza lako tukufu na wote waliochangia hotuba hii ya Bajeti ya wizara yangu moja kwa moja au kwa maandishi. Michango yao kwa njia moja au nyengine itaweza kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wizara. Miongoni mwa wajumbe waliochangia katika hotuba hii ya wizara yangu naomba niwataje ni:

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii
2. Mhe. Asha Bakari Makame
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
5. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
6. Mhe. Hija Hassan Hija

7. Mhe. Subeit Khamis Faki
8. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
9. Mhe. Fatma Mbarouk Said
10. Mhe. Hassan Hamad Omar
11. Mhe. Mussa Ali Hassan
12. Mhe. Panya Ali Abdalla
13. Mhe. Salim Abdalla Hamad
14. Mhe. Moh'd Mbwana Hamad
15. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
16. Mhe. Saleh Nassor Juma
17. Mhe. Hamza Hassan Juma
18. Mhe. Ali Salum Haji
19. Mhe. Salmin Awadh Salmin
20. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika
21. Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
22. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
23. Mhe. Mwanasheria Mkuu na kadhalika.

Kwa bahati Mhe. Mwenyekiti, kuna na waliochangia kwa maandishi naomba pia nao niwataje.

1. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
2. Mhe. Nassor Salim Ali
3. Mhe. Mussa Khamis Silima
4. Mhe. Nassor Salim Ali
5. Mhe. Mgeni Hassan Juma
6. Mhe. Mohammed Said Mohammed na
7. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze kwa kuwashukuru ten asana na hasa nataka nianze kuishukuru Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wajumbe wake wote kwa ushauri na miongozo yao mizuri yakiwemo kutangaza kituo cha Mkono kwa Mkono (*One Stop Centre*) ili wanajamii wakielewe vizuri.

Kufanya utafiti wa masuala ya ubakaji katika Mkoa wa Kaskazini ambako tatizo hili ni kubwa, kufuatilia utekelezaji wa haki ya watoto walio katika magereza kuhakikisha watoto wanatenganishwa na watu wazima katika Magereza, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupewa fursa ya kuyatambua Mabaraza ya Watoto, Sera ya Hifadhi ya Jamii iharakishwe kwa utekelezaji na kinamama wahamasishwe kuanzisha benki zao hasa kinamama wa ukanda wa pwani wanaozalisha mwani kama kina mama wa *SACCOS* ya Tujuane Pemba.

Yote haya Mhe. Mwenyekiti, tutayafanyia kazi tumeyapokea kwa heshima zote na Mweneyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake kwa bahati nzuri tunashirikiana naye vizuri anajuwa utendaji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea naomba nitoe kuhusu taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Kuwa kamati haikuridhishwa na Hali ya Makaazi ya Wazee wa Limbani Pemba.
Naomba nieleze kamati yako tukufu kuwa hali waliyoikuta katika ziara yao ya Kamati sasa kunamabadiliko makubwa na ya kutia moyo.

Uongozi wa Wizara Pemba kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii imefanya ukarabati mdogo sehemu ya jiko, sehemu ya hodhi ambapo maji kwa sasa yamehifadhiwa vizuri. Pia wazee hao wamenunuliwa vifaa kama ndoo mpya, makopo, mashuka ya kutandika na vitanda ili kuweka mazingira mazuri na Ustawi wa Wazee. Lakini pamoja na hayo tuna tanatakiwa tuwalee wazee wetu, sio serikali tu, na sisi tuanze.

Mhe. Mwenyekiti, wizara pia inamshukuru Mhe. Asha Bakari Makame kwa mchango wake mzuri na kuipongeza wizara. Tumepokea pongezi zake na pia alisisitiza umuhimu wa kuwepo wizara na kushauri wizara karibu na Wizara ya Uwezeshaji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Uvuvi na Biashara katika kuwaendeleza wanawake na Vijana, yaani tushirikianre nao. Tuna mashirikiano makubwa hivi sasa na kwa hivi alivyotwambia kwamba tushirikiane nao tutazidi kushirikiana nao kwa hali na mali.

Aidha, alisisitiza mashirikiano baina ya Mama na Baba katika malezi, kwa upande wa watoto alitahadharisha wale wanaotelekeza watoto wachukuliwe hatua zinazofaa. Jamani msituache ache watoto wanataabika.

Mhe. Asha Bakari alitoa pongezi kwa serikali kuongeza posho ya wazee kutoka shilingi 25,000/= mpaka shilingi 40,000/=. Mhe. Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mhe Asha Bakari kuwa ushauri wake tunauchukua na sasa hivi tumeshaufanyia kazi. Wazee bajeti hii watalipwa shilingi 40,000/-.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makame Mshimba aliuliza Nyumba ya Forodhani imefanywa nini baada ya kuondoshwa watoto kupelekwa Mazizini?

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mshimba kwamba nyumba iliyokuwa ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imelikabidhi rasmi Jumba la Kulelea Watoto Forodhani kwa iliyokuwa Wizara ya Maji kwa barua rasmi kwa ajili ya kufanya makumbusho ya bahari. Nadhani tunaona sasa hivi pale na barua hapa ninazo kama nilivyoambiwa nilete hati, nilete nini, mambo yote yako hapa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Salmin Awadh kuhusu suala lake la posho jipya la wazee, naomba asiwe na wasiwasi katika bajeti hii sio ya mwakani shilingi 40,000/- watapatiwa wazee wetu. Tunategemea posho hilo wataanza kulipwa baada ya kumaliza bajeti tunaweza kusema Oktoba, Novemba, lakini ni katika bajeti hii hii.

Mhe. Mwenyekiti Mhe. Makame Mshimba ametaka kupatiwa mafunzo vijana kabla ya kupewa fedha. Nakubaliana na Mhe. Mshimba kwamba suala la mafunzo kabla ya kutoa fedha ni la muhimu sana. Sera ya wizara yangu ni kuhakikisha mafunzo yanatolewa kwanza ndio fedha zifuatie ili zisije zikapotea ovyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba tayari wizara imekubaliana na Benki ya *CRDB* na *UN HABITAT*, kuwapatia vijana mafunzo ya uanzishaji na uendelezaji wa *SACCOS*, ujasiriamali, utunzaji wa hesabu na uongozi bora wa kuendesha vikundi vyao vya uzalishaji kabla ya kupewa mikopo na hiyo tunaifanyia kazi. Kwa sababu kupewa mikopo watu wanasema kukopa harusi kulipa matanga. Kwa hivyo, lazima tuwe na utaratibu wa kuhakikisha mikopo ni endelevu, yaani anapata huyu anafanyia kazi na baadae anapata mtu mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak alizungumzia suala la uhaba wa nafasi katika majengo ya wizara ya Shangani na Vuga. Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, napenda kulieleza Baraza lako tukufu kuwa serikali imeamua kujenga majengo ya ofisi na tumeambia kwamba wizara yetu itapewa kipaumbele. Kwa hivyo, tunasubiri jumba kubwa la ghorofa tutakalojengewa, msiwe na wasiwasi wa kuhama kwetu hiyo ni mipango ya kiserikali.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mtumwa pia alizungumzia haja ya kuongeza watendaji (wataalamu) katika wizara**.** Napenda kumjuulisha Mheshimiwa kuwa wizara imejipanga katika kujiimarisha kiutendaji. Kwa kuanzia wizara itafanya tathmini ili kujua uwezo wake halisi wa kutendaji. Aidha, wizara itatayarisha mpango mzuri wa mafunzo ili kuwapa uwezo wafanyakazi wake wote kiutendaji.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Subeti suala lake linalohusu fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali kazini kwa kumpa maelezo yafuatayo: Wizara haipendi kukaa na madeni ya watu muda wote huo, isipokuwa kutokana na Bajeti finyu tunayoipata na majukumu mengi tuliyokuwanayo tunalazimika kulipa fidia kutokana na uwezo wa kifedha tuliokuwanao. Kwa mfano, wizara kwa mwaka ina bajeti finyu sana ya kutekeleza majukumu yake. Lakini usiwe na wasiwasi ndugu yangu Subeit zikipatikana pesa watu watalipwa pesa zao.

Mhe. Mwenyekiti, tuna kazi ya:-

- Kuwahudumia wazee walioko Sebleni, Limbani na Welezo
- Kuwahudumia Watoto wa Nyumba ya kulelea Watoto Mazizini na wale wa binafsi
- Kuwahudumia Watoto wanaoishi katika mazingira magumu
- Kuhudumia Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto pamoja na *"One Stop Centre"*
- Kutoa fidia
- Kuzika maiti wasiokuwa na watu
- Na shughuli zote za utendaji wa ofisi kwa idara na tumeambiwa hapa kwamba wale wanaozika tunawapa pesa ndogo, lakini inategemea na fungu tulilowekewa ambalo ni shilingi 438 milioni kwa kazi za mishahara na matumizi mengineyo. Kati ya hizo shilingi 180 milioni ni matumizi mengineyo ambazo zinahitajika kutumiwa kwa shughuli kama hizo nilizozitaja.

Kwa hivyo, jamani tutakwenda kwa kadiri ya tulichonacho.

Mhe. Mwenyekiti, katika ufinyu wa bajeti nilionao namuomba Mhe. Subeit anisaidie kunipigia debe kuongezewa bajeti yangu ili niweze kulipa fidia kama inavyotakiwa, bila ya hivyo nitaendelea kutoa fidia kwa kadiri ya bajeti yangu itakavyoniruhusu. Kwa kweli hali halisi ya bajeti niliyonayo ni hiyo naomba mnielewe Waheshimiwa Wajumbe nyote.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu ina nia nzuri ya kuwalipa wote wanaohitaji fidia mfano mzuri katika bajeti ya mwaka jana 2010/2011, wizara ililipa fidia kwa wafanyakazi kumi na tisa (19) iliyogharimu shilingi 16,050,000/= Unguja na Pemba. Deni ambalo wizara yangu imelirithi tokea iliposita kulipwa mwaka 2007. Kwa hivyo, sisi tulipokuja tumejitahidi inafaa mtupongeze Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi tuliyoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Subeti alieleza kuhusu wazee 119 tunaowalipa katika makaazi ni kidogo kulingana na wazee waliopo wilayani. Ni kweli, lakini napenda kumfahamisha Mhe. Subeti na Baraza lako tukufu kuwa wazee wengine wengi wanalipwa kupitia Afisi za Wilaya chini ya Wizara ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hata hivyo, Waheshimiwa, wizara yangu inalipa wazee hao 119 kutokana na uwezo wa bajeti tuliyonayo.
Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Subeit amekiri kuwa Wilaya ya Micheweni kuna ajira nyingi za watoto na akataka kujua, jee, wizara ina mkakati gani kupunguza ajira hizo?

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu ni kweli kusema kuwa Wilaya ya Micheweni bado inalo tatizo la ajira za watoto. Wizara yangu pamoja na wizara nyenginezo za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika wa Maendeleo mbali mbali tayari tumechukuwa hatua mbali mbali za kuwawezesha wanawake na wananchi wa Micheweni katika kujiongezea kipato na kupunguza umaskini, wakati huo huo kupiga vita ajira za watoto na hatimae kuondosha ajira hizo. Kuna vikundi vingi vya wanawake ambavyo vinapatiwa mafunzo ya kubuni miradi mbali mbali. Vikundi hivyo tayari wameshasaidiwa miradi ya sabuni, kutengeneza chaki, kulima vitunguu na ukulima wa mboga mboga. Tayari vikundi hivyo vinaweza kuendeleza miradi yao na watoto wakaweza kuendelea na skuli.

Mhe. Subeit usikubali watoto wa Micheweni kukaa wakawa hawasomi, wakisukumia kwamba hali ngumu ya maisha, hatuna chakula, hatuna hivi, hatuna vile. Lakini kinachojitokeza ajira za watoto kwa Wilaya ya Micheweni ni tabia inayoendekezwa na wazazi, hivyo hatuna budi tubadili tabia na viongozi hasa wa Micheweni wasimamie. Mhe. Bikame Yussuf Hamad naomba usimamie sana juu ya suala hili ili tuweze kuwakomboa watoto kutokana na ajira mbaya za watoto ambazo zinawakosesha haki zao za msingi za kusoma, kutunzwa na kuendelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Subeit pia alizungumzia na akataka kujua suala la *SACCOS* ya Kikundi cha Tujuwane Konde ambao wameweza kuwa na *SACCOS* kubwa, ambapo na wao ni miongoni mwa vikundi tulovipatia mafunzo na misaada mbali mbali.

Naomba kumjibu Mhe. Subeit kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Jimbo la Micheweni, namuomba Mheshimiwa ashirikiane nasi katika kuwaendeleza wananchi wa Micheweni wapate maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile napenda kumuhakikishia Mhe. Subeit kuwa wizara yangu imeandaa mikakati ya kuwasaidia Wanawake, Vijana, Watoto na Wazee wa Wilaya zote ili hali zao ziweze kuwa nzuri na hasa ikiwemo Micheweni. Micheweni mbona siisahau, mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya Micheweni karibu miaka miwili. Watu wa Micheweni wananifahamu vizuri msimamo wangu, uwezo wangu, huruma zangu kwao. Kwa hivyo, naomba tushirikiane tufanye kazi zetu kwa pamoja.

Mhe. Menyekiti, naomba kuwajibu Mhe. Mtumwa Kheri Mbaraka, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) na Mhe. Viwe ambao wametaka kujuwa Baraza la Vijana litaundwa lini na sababu gani zilizochelewesha?

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Salim naye vile vile alielezea kuhusu Baraza la Vijana linaendelea na mchakato wake wa kuanzishwa. Wizara imepata mshauri mwelekezi na kuandaa mikutano ya vijana Unguja na Pemba. Mawazo ya vijana hao yaliratibiwa na Mshauri Mwelekezi na kuandaliwa Rasimu ya Katiba ya Awali ya Baraza, kwa sababu hatuwezi kuunda Baraza la Vijana bila ya kuwa na katiba ya Baraza hilo, ambayo ilirejeshwa tena kwa vijana wenyewe na sasa Katiba ya Baraza hilo imekamilika. Sera zile za zamani naomba niwaambie kwamba zimepiotwa na wakati sasa katika serikali hii ya kitaifa lazima tuandae sera madhubuti ambazo tutazisimamia vizuri na tutazifanyia kazi. Hatua zinazofuata ni kuwasilisha Katiba ya Baraza la Vijana katika ngazi za Makatibu Wakuu na Baraza la Mapinduzi, uchache wa fedha ndio uliosababisha kuchelewa kuanzishwa kwa Baraza hilo.

Naomba kuliarifu Baraza lako tukufu, wizara itakamilisha uundaji wa Baraza la Vijana katika mwaka huu wa fedha 2011/2012 kama lengo la Idara ya Vijana namba 2 ilivyoelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Mhe. Hija la kwamba fedha za *CRDB* na *UN HABITAT* kwamba hazijaingizwa katika hotuba ya bajeti ni kwamba fedha za *CRDB* ni fedha zilizoingizwa tokea bajeti ya mwaka 2010/2011. Hivyo hazikuweza kuonekana katika bajeti hii. Na kuhusu fedha za *UN HABITAT* shilingi 149,000,000/ hizi ni fedha ambazo zipo *UN HABITAT* hatujaletewa Wizarani. Sisi kazi yetu kuwahamasisha Vijana kujaza fomu na kuzituma *UN HABITAT* kwa wale waliotimiza masharti watapewa fedha hizo kupitia *UN HABITAT*. Kazi hii tumeifanya Pemba na Unguja, tumewakagua vijana vizuri tukifuatana na watu wa *UN* na waliokubalika ndio waliochukuliwa na majina yao kuingizwa katika intaneti na sasa hivi yanafanyiwa kazi. Tusubiri kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Kesi za Ubakaji, suala hili limezungumzwa sana takriban ukumbi mzima kila anayesimama anasema jamani ubakaji umekithiri. Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Mtumwa Kheri, Mhe. Subeit, Mhe Mtando, Mhe. Fatma Mbarouk, Mhe. Panya, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe Viwe, Mhe. Hassan Hamad na Mhe. Bikame Yussuf Hamad. Wote hao wamezungumzia suala la ubakaji na udhalilishwaji wa watoto wetu.

Wizara yangu mpaka sasa imepokea malalamiko, kuna malalamiko na kesi ni mambo tofauti, tusichanganye kesi na malalamiko. Malalamiko ni yale yanayokwenda wazee kwa wazee yakaja zake wizarani hawakupitia popote, hawakupita polisi wala wapi. Malalamiko yaliyoletwa kwa kubakwa watoto ni 74 ambapo kesi 5 tu ndio zilizotolewa hukumu. Ni malalamiko, kesi nyengine bado ziko polisi zinaendelea katika hatua ya upelelezi na nyingine zinaendelea kusikilizwa Mahakamani. Lakini kwa sababu ya sheria ya mtoto sasa itafanya

kazi kesi zitakwenda zake polisi kupitia vitengo vyetu tulivyovitayarisha mkono kwa mkono katika Mikoa, Wilaya pamoja na hapa Mjini Unguja.

- Katika juhudi za kupambana na vitendo vya udhalilishaji wizara imeanzisha Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto, Kituo cha Mkono kwa Mkono "*One Stop Centre*". Imetoa mafunzo ya Hifadhi ya Mtoto kwa wadau mbali mbali kutoka katika Shehia za Unguja na Pemba wakiwemo Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayohusiana na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na *Save the Children* katika Chuo Kikuu cha Zanzibar kiliopo Tunguu. Pia kuandaa mpango wa utekelezaji wa Sheria ya Mtoto.
- Hatua nyingine imeanzisha kamati za Hifadhi ya Mtoto Unguja na Pemba na Kamati za Kupinga Udhalilishaji Kijinsia (*GBV*). Yaani kuna kamati, kuna na vituo, polisi na *One Stop Centre* na kadhalika. Hizi zote ni jitihada za kutaka kwamba udhalilishaji, ubakaji wa watoto uondoke, haidhuru na sisi wanawake tunaambiwa tunawabaka watoto, lakini mili hilo sikubaliani nalo.
- Kutoa taaluma kwa jamii juu ya nini kifanyike pindipo mtoto atabakwa.
- Kuimarisha utendaji wa Kamati ya Kitaifa ya Hifadhi ya Mtoto kwa kuipatia elimu ya ushughulikiaji masuala ya udhalilishaji.
- Kusambaza miongozo ya Kitaifa ya Hifadhi ya Ustawi wa Watoto Zanzibar kwa wadau mbali mbali ili kuwafanya wawajibike katika kupambana na vitendo hivi.
- Kuitumia Sheria ya Mtoto na Muongozo wake mzima katika kulinda na kutetea maslahi yao.
- Watekelezaji wote wakiwemo Mahakimu, Maafisa Ustawi, Waendesha Mashtaka, Polisi, Wapelelezi na Wanasheria, wote watapatiwa mafunzo maalumu kwa ajili ya kushughulikia utekelezaji wa sheria hiyo.
- Sheria hiyo itawekwa katika lugha nyepesi ili wananchi wote waweze kuifahamu vizuri na kuitekeleza. Kazi kubwa nyengine tutakayokuwanayo katika sheria hii ni kupita tukiwahamasisha wananchi kwamba wasikubali ushauri wa pembeni pembeni kusema fulani namuonea huruma, jirani yangu, ndugu yangu, tuko ukoo mmoja, kwa hivyo tusaidiane tumuozeshe mtoto, yatamalizika haya.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salum Abdalla ametaka kujua juu ya suala la fidia kwa walioanguka katika mikarafuu. Napenda kumfahamisha Mhe. Mjumbe kwamba suala la fidia kwa wanaoanguka na mikarafuu malipo yake yanashughulikiwa na Shirika la *ZSTC* ambalo liko chini ya Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko, nadhani kesho atasoma hotuba yake. Wizara yangu

kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii hufanya tathmini tu, na hatimae kuiwasilisha kunakohusika.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Viwe Khamis Abdalla alieleza mpango wa kukodi jengo kwa ajili ya Ofisi ya Wizara Pemba, lakini hatujaonesha fedha za malipo ya jengo hili. Mhe. Viwe naomba kumjibu kwamba, ni kweli wizara imeshaanza kutafuta jengo la kukodi kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Wizara Pemba. Tayari jengo limeshapatikana na Wizara ya Fedha imo mbioni kutiliana mkataba na mwenye jengo hilo ili malipo yaweze kufanyika na hatimae tuweze kuhamia katika jengo hilo. Mhe. Viwe hatutoi sisi fedha, wenzetu hawa wa Wizara ya Fedha ndio watakaotukodia hilo jengo na ndio watakaolipa. Naipongeza sana Wizara ya Fedha kwa uamuzi wake huu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe, Mtumwa Kheri kuwa kweli Wazee wa Sebleni hivi sasa hawana daktari, kutokana na daktari aliyekuwepo kustaafu mwaka jana. Tumeomba Daktari mwengine kutoka Wizara ya Afya bado hatujapatiwa kutokana na upungufu wa madaktari. Hata hivyo, Wazee wa Sebleni bado wanafursa nzuri ya kutumia hospitali iliyopo ndani ya fensi yao katika Nyumba ya Sebleni ambayo ina daktari na manesi na huduma za dawa na uwezo utakaporuhusu tutahakikisha angalau tunapata gari moja kwa ajili ya usafiri wa wazee, lakini sasa hivi bado hatujaweza kuwa na gari.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala lililozungumzwa na Mhe. Mshimba, Mhe. Mtando, Mhe. Saleh Nassor Juma na Mhe, Hamza Hassan Juma. Mimi kwanza nataka niipongeze *ZAYEDESA*. Maana zipo *NGO's* nyingi hapa Zanzibar, lakini hazikushughulika wala kuhangaika, lakini wao walishajihisha kwa nia nzuri tu kuwajengea watoto yatima waliokuwa wananishi katika Jumba la Forodhani kwa kuwa jengo lao ambalo lilikuwa ni bovu na halistahiki kuishi watoto wetu kwa usalama wao. Hati miliki ya Jengo hilo hii hapa ninayo, mambo yote ninayo hapa, si mmenambia niwaletee jamani Waheshimiwa Wajumbe. Kuna makabidhiano hapa ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi walivyokabidhiwa ile nyumba ya Forodhani. Kuna mikataba hapa nitazungumzia baadaye habari ya mikataba ya nyumba ya Mazizini. Kuna hati ya kiwanja hapa, mmoja alisema anataka ajue mambo ya hati ya kiwanja. Hati hii hapa walipewa *ZAYEDESA* ndipo wakaanza kujenga.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme nilianza na kuwapongeza *ZAYEDESA* kwa kazi nzuri waliyofanya na kwa kweli mara ya kwanza mimi nilipozungumzia jambo hili wenzangu hapa walisema mimi nazungumzia mambo ya kisiasa. Lakini baada ya kwenda kuona hali za watoto zilivyo wao wenyewe wamehakikisha kwamba watoto sasa hivi wapo katika hali nzuri ya usalama na amani.

Ni kweli juzi kulipita majambazi pale lakini kwa bahati nzuri sasa hivi ulinzi upo. Nawaambia hao majambazi kwamba wakifika tena mara hii tumeshawaambia hakuna kumuuliza wala nini, mpige risasi za miguu halafu tena ndio utashughulika na mengine. Kwa nini watu watoke waende kuwaadhibu watoto wetu, hatutaki habari hiyo.

Sasa jambo kubwa najua mnalolipenda kulisikia hapa ni kwamba vipi hatima ya jengo lile. Sisi hatima ya jengo lile tunawapigania watoto. Mikataba ipo na kwa utaratibu wetu mpaka leo hatujatiliana saini kwa sababu mambo haya lazima yaende kwa utaratibu unaotakiwa kiserikali. Hatuwezi tu tukaruka tukachukua mikataba tukakaa sisi na *ZAYEDESA* tukatiliana masaini. Lazima ipite hatua kwa hatua na ikimalizika hatua kazi hiyo itafanyika sisi tutakuwa wazi, serikali itatuelekeza tufanye nini, hatuwezi kuyachukua mambo kifua kifua tu.

Hata hivyo, Wizara inaendelea kufanya majadiliano ya suala la makaazi ya watoto, pia tutahakikisha haki ya watoto inatendeka. Umiliki wa asili wa kiwanja kilikuwa ni cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Namshukuru sana Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ambaye alikuwa waziri wa zamani wa wizara hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sitakuwa na majibu mengine zaidi kuhusu mambo ya mikataba. Naomba mlipokee hilo, atakayenipigia buti anipigie tu kwa kunionea. *(Kicheko)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) Wizara inaendesha Kambi Kazi za Vijana ya Kimataifa kila mwaka Unguja na Pemba. Lengo la kambi kazi hizi ni kuimarisha mahusiano kati ya vijana wa Zanzibar na wale wa nje ya nchi. Aidha, kuwapatia vijana wa Zanzibar fursa ya kubadilishana mawazo na vijana wenzao wa nchi mbali mbali za dunia juu ya mambo yanayowahusu. Vile vile kuwaelimisha vijana kwa vitendo juu ya dhana ya kujitolea kwamba suala la vijana kujitolea sio la Zanzibar peke yake bali ni suala la dunia nzima. Aidha, kambi hizi zinaendelea Maungani, Bambi na Bwejuu ambapo vijana wa Zanzibar na wale waliotoka nchi 12 za dunia wanafanya kazi za ujenzi wa taifa katika vituo vya Afya kwa kupaka rangi na kujifunza Kiswahili na wao kufundisha Kiingereza.

Mhe. Mwenyekiti**,** Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) alitaka kujua sababu za kuhama katika jengo la Mwanakwerekwe. Napenda kumjuulisha Mhe. Mjumbe kwamba majengo yanayotumiwa na taasisi za Serikali ziko chini ya usimamizi wa Serikali ya Awamu ya Saba ilipoundwa ilikabiliwa na uchache wa majengo ya Serikali, Serikali ililazimika kuzigawa Ofisi zake ili Wizara zote zipate nafasi. Ndio maana sisi Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya

Vijana, Wanawake na Watoto ikalazimika kuhama na kutafutiwa jengo jengine Shangani.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando). Mkakati wa Wizara katika kushughulikia suala la udhalilishaji wa watoto ni kuunda Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Sheria mpya ya Mtoto ambapo kanuni za kurahisisha utekelezaji wa sheria hii zitaundwa katika utekelezaji wa sheria hii watapatiwa mafunzo (mahakimu, maafisa hifadhi, waendesha mashtaka, maafisa ustawi wa jamii, polisi na wapelelezi). Sheria hii pia itawekwa katika lugha nyepesi/rahisi *(popular version)* kama nilivyosema awali ili isomwe na ieleweke kwa jamii yote ya Kizanzibari na uhamasishaji mkubwa utafanyika kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) linalohusu *SACCOS* za Pemba, takwimu za *SACCOS* Pemba kuna *SACCOS* 11, Kusini 5 na Kaskazini 6. Vikundi vyote ni vya kuweka na kukopa. Wanaume ni 137, wanawake ni 155 na jumla ni 292. Wajasiriamali Pemba ni 132, wanaume 285, wanawake 279, jumla ni 560 ambao wanajishughulisha na kushona, kuchonga, kulima, uvuvi, ufugaji nyuki, kusuka vikapu na mikoba.

Mhe. Mwenyekiti, nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba kazi hii haijasimama hapo, tutaendelea kuhamasisha, kuwafundisha, kuwaimarisha vijana wetu ili waweze kujituma wenyewe kwa sababu si kweli katika nchi hii kwamba tutaweza kuajiri vijana wote waliopo hapa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Salum Haji anataka kujua kuhusu Sera ya Maendeleo ya Vijana. Sera hii ni ya zamani ya mwaka 2001 na hivi sasa inafanyiwa kazi ya kupitiwa upya ili kufanya iende na wakati na inayotekelezeka. Ni kweli ina mapungufu mengi jambo lililofanya wizara iifanyie mapitio.

Mhe. Salmin Awadh Salmin alitaka ufafanuzi wa Wajumbe wa Kamati ya Kitaifa inayohusika na kuzuia vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia lakini alitupongeza sana. Mhe. Mwenyekiti, vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia vipo tena vingi vikubwa. Udhalilishaji huu sio kamati tu lakini hata sisi Baraza zima tufanye kazi hiyo kwa shauri moja, tuupige vita udhalilishaji katika nchi yetu. Hayo mambo ya kuhasi sisi hatuyataki, tunataka watu wafahamu nini tunachokitaka. Hivi kweli sio aibu baba kahangaika mpaka akampata mtoto wake akisha aende akambake ndani ya nyumba jamani.

Tunaambiwa sisi wanawake tunasababisha ubakaji kwa sababu tunavaa nguo zisizostahiki kwa hivyo wizara ichukue hatua. Lakini nisikilizeni mtoto wa miaka mitatu je, nae anavaa nguo isiyostahiki, kwa nini abakwe na yeye pia kakuvutia mapaja yake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu swali lake Mhe Salmin Awadh Salmin kwa kumpa ufafanuzi kwamba naomba kukuelewesha kuwa kuna kamati moja ambayo wajumbe wake waliteuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein.

Kamati ya pili ya Kitaifa imeundwa kutokana na taasisi mbali mbali kama zilivyoonesha katika kitabu chetu ambapo Mwenyekiti wa Kamati ni Kamishna wa Polisi Ndg. Mussa Ali, Katibu wa Kamati ni Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Afisa Mdhamini Pemba kutoka Wizara ya Ustawi wa Jamii, Polisi kutoka Mtandao wa Polisi Wanawake, Wizara ya Afya Afisa Jinsia, Wanasheria Wanawake *(ZAFELA)*, Mwanasheria na Mwendesha Mashtaka na pia ni Kaimu Mwanasheria dhamana kutoka Pemba pamoja na Afisa kutoka Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, yote haya tutaunda makamati tutafanyaje lakini kama hatukukubaliana kuondosha vitendo hivi hawa wenzetu watashindwa. Jambo kubwa ni kushikana kwa pamoja serikali tuone kwamba hili jambo ni *very sensitive*, ni jambo baya halituwekei heshima katika nchi yetu. Zanzibar ni nchi ya heshima kubwa bwana au vipi jamani. Zanzibar ni nchi ya heshima, watu wake ni watu wa kuheshimiana, kwa hivyo kwa nini tusiheshimiane tubakane haiwezekani jambo hilo tuliache mara moja.

Kamati hii lengo lake ni kuratibu shughuli zote za udhalilishaji wa wanawake na Watoto Unguja na Pemba. Mhe. Mwenyekiti, kamati hii ni *change* bado tunaendelea kuujadili muundo wake, majukumu pamoja na kupatiwa nguvu ya kisheria ili iweze kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru sana Mawaziri wote waliochangia katika bajeti yangu pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwa kweli mmenisaidia sana, mmetoa mchango mzuri. Mimi nawashukuru na nategemea sasa tutapitisha vifungu bila ya matatizo yoyote. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hoja imeshatolewa wanaokubali, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama

Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

Fungu 28 Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto

Kifungu 0301 – Ofisi Kuu Pemba 302,000,000
Kifungu 0401 – Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri amenijibu vya kutosha. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba amejitahidi kunijibu lakini majibu yake bado naomba nipate maelekezo zaidi.

Kwa sababu nilimwambia Mhe. Waziri kwamba fedha hizi za wafanyakazi ambao walipewa fidia zina muda mkubwa sana. Pamoja na hivyo nilimwambia yeye kama msimamizi mkuu wa fedha hizi nilimtaka asimamie na atupe ahadi fedha hizi watazipata lini. Kwa hivyo, namuomba bado anipe majibu ya kuwa wafanyakazi hawa yeye sasa kama msimamizi mkuu wa kusimamia Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ili atoe pesa za kuwalipa hawa watu. Anambie ni lini atafanya jitihada ya kupatiwa watu hawa fedha zao.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, hapo mwanzo nilimueleza Mhe. Mwakilishi kwamba pesa tangu mwaka 2007 zilikuwa hazijatolewa. Lakini baada ya wizara yetu hii kuanzishwa tumehangaika tumetoa tulichokitoa. Kwa hivyo, kumwambia kama lini tutazitoa pesa si kweli nitakuwa nasema uongo hapa. Kwa hivyo, naomba Mhe. Subeit Khamis Faki ajenge imani kwamba pesa zikipatikana na sisi tutazipeleka kwa walengwa. Ahsante.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, yule mama yangu mimi namheshimu sana na sitaki nimuhangaishe sana lakini Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo yupo anasikia. Kwa hivyo, nimuombe Waziri wa Fedha atie kauli yake kwa sababu hili suala limeshakuwa la muda mrefu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba Mhe. Subeit Khamis Faki akubali na wenzake wote wenye suala hili wakubali kwamba tutaiangalia hii hali halisi tutasoma ripoti zao za tathmini halafu tuweze kuharakisha upatikanaji wa fedha ili watu hawa waweze kulipwa fidia kwa mujibu wa taarifa zinavyosema.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kaka yangu, rafiki yangu Mhe. Waziri anambie tu kwamba bajeti inayokuja japo kama hii ameshaifanya vibaya aiache, lakini alete ahadi kama bajeti inayokuja hiyo anihakikishie kwamba watu hawa watamaliziwa pesa zao. Kwa hivyo, bajeti inayokuja amuongezee mama fungu ili watu hawa walipwe pesa zao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Subeit Khamis Faki kwamba *concern* ya wajumbe wengi juu ya wizara yetu hii kwamba bajeti yake mwaka huu ni ndogo. Wajumbe wengi wameomba kwamba tuiongezee bajeti mwaka kesho ili waweze kufanya vizuri zaidi katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, moja ya jukumu ni hili. Nataka nimhakikishie Mhe. Subeit Khamis Faki kwamba hilo tutalifanya ili hii wizara iweze kupata bajeti nzuri zaidi na iweze kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi ikiwa pamoja na hili la fidia. Atustahamilie tuisome fidia tuweze kuona kama tutaweza mwaka huu au kama mwaka kesho basi tutafanya kazi hiyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naomba nieleweke kupiga buti maana yake sio kuzuia Mhe. Waziri asifanye kazi zake. Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia suala la udhalilishwaji wa watoto. Nashukuru tumepata jawabu kwa Mwanasheria Mkuu, wamezungumza na waheshimiwa wengine, Mhe. Haroun Ali Suleiman kazungumza kamati iliyoundwa na Mhe. Rais. Lakini bado Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada zote hizo takwimu za kesi tulizopewa zilizotolewa hukumu ni kesi tano.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nimechangia angalau ningejibiwa, basi hiyo orodha ya hao uliokuwa nao tuletee. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hili suala kama tulivyozungumza kwamba hapa sisi tunazungumza na tunalipwa kwa ajili ya kuwatetea wananchi. Tunazungumza hoja hizi kwa majibu ya Waheshimiwa Mawaziri na Mwanasheria Mkuu hawa wafanyaji hawajashtuka. Sisi tunataka angalau tunapoondoka katika kikao hichi hawa watendaji wa vitendo hivi wajue hasa kwamba kuanzia sasa hivi tuko hatarini.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana maelezo je, wataweza kufanya vipi kwa sababu kuna utafiti umeshafanywa na ushahidi upo. Watawekwa hadharani lini hawa watu.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nadhani nimejitahidi kujibu kuhusu udhalilishaji. Sasa kama unataka mwenzangu nijibu kauli nyengine sijui nitaipata wapi.

Lakini mimi ninachokuahidi kwamba nitajitahidi juu ya kadhia hii ili ituondokee kabisa nchini petu. Nadhani sina jibu jengine zaidi ya hilo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri suala la Mhe. Hamza Hassan Juma alilokuwa akitaka ni kwamba hawa wahalifu aina hii wawekwe hadharani. Sasa hapa ninachoweza kusema ni kwamba sisi tutahakikisha kwamba anapopatikana na hatia basi vyombo vyetu vya habari TVZ, redio tutazihakikishia kwamba lazima ziwatoe hadharani watu hawa ili jamii ielewe kwamba watu hawa wana matatizo haya na wamepata adhabu ya aina fulani.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alipokuwa akichangia alizungumza kwamba ni juzi tu imemfuata timu ya kuna ustadh ambaye kabaka lakini tayari sasa hivi wale wahusika wametakiwa dhamana. Kwa sababu mimi hoja yangu sio baada ya hawa kuhukumiwa lakini ni namna gani tutaweza kuwashughulikia hawa ambao wanahusika na hizi kesi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilichokuwa nakitaka mimi kwamba lazima kuwe na utaratibu kwanza wa kuwasaidia hawa wanaoshughulikia hizi kesi. Tatizo letu kwamba ile *One Stop Centre* iliyowekwa pale wao wanakuja kuangalia tu ule mchakato nani kaharibiwa lakini katika suala la mambo ya kisheria hawana mchango wowote. Ndio maana tukasema kwamba kwa kuwa kuna taasisi imeshafanya tathmini na wamehojiwa watoto wenyewe, wanazungumza sisi tukirudi skuli tunakwenda wapi na wapi, tunafanywa hivi. Kuwekwa hadharani watu hawa tunaona tabu ya nini.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, baada ya kupata majibu ya sasa hivi kuna ushauri vile vile nitataka kuutoa. Kwa sababu ukisema kwamba watakaopatikana na kesi watatolewa kwenye TV ndio kwanza kesi tano katika kesi 74 watoto wanaendelea kuharibika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi mkitaka ushahidi hebu nendeni kwa Raju pale usiku hatari tupu, vijana wa Kizanzibari wameshaharibika na hawakuharibika hivi hivi walianza kuharibiwa tangu watoto. Tunachukua hatua gani, tunataka tuisaidie serikali.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba Mhe. Hamza Hassan Juma aelewe na nina hakika anaelewa kwamba utaratibu wa sheria ni tofauti kidogo. Huwezi tu mtu ukamtuhumu halafu ukamtoa kwenye vyombo hilo ni tatizo na ni kosa. Kwa hivyo, lazima kwanza tuhakikishe na tukisha kumtia hatiani hapo tutakuwa na uhuru kisheria na ndivyo katiba inavyotaka.

Lakini jengine ambalo naweza kumwambia ni kwamba katika hiyo *One Stop Centre* ambayo anazungumzia tumezungumza na Mhe. Waziri tukaona matatizo yaliyopo na hivi sasa tumeshafanya mipango mizuri ya kuwaweka wanasheria ambao ni wazuri na watakaofuatilia kesi hizi. Nafikiri katika hotuba yake Mhe. Waziri alisema kwamba tutawapa mafunzo maalum wanasheria hawa ili waweze kuhakikisha kwamba wale wote wanaokamatwa watajitahidi, ili kupata ushahidi na kupata yale ambayo yanatakiwa ili watu wale ambao ni wahalifu au wanaoshukiwa kwamba ni wahalifu waweze kutiwa hatiani bila ya matatizo yoyote.

Kwa hivyo, hayo ndio tunayoweza kusema na ni vyema akajua tu kwamba haiwezekani kabla mtu hujamtia hatiani ukamtangaza katika vyombo hiyo itakuwa ni kinyume na utaratibu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anazidi kunichanganya. Mhe. Mwenyekiti, siku zote tunaona watu wanakamatwa wameiba nazi, wameiba kuku kabla kesi hazijatolewa wanaoneshwa kwenye TV tunawaona. Unajua Mhe. Mwenyekiti, hapa sisi tuna vita, hii ni tofauti na kesi nyengine. Tunaona tabu gani leo mtu ameshakamatwa kambaka mtoto wake anaoneshwa kwenye TV halafu kesi inakwenda tunakuja kusubiri baadae. Mbona hawa wanaoiba kuku, nazi na mihogo au wanaokamatwa na bangi wanaooneshwa pale. Ndio maana mimi nikawa nasema tuna hofu ya nini, tunaogopa nini.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kazungumza lakini hoja yake kwa hoja yangu mimi nimeshamshinda. Kwa nini wanaoiba kuku na wanaoiba nazi waoneshwe, wabakaji wa watoto wadogo wasioneshwe, sijapata jawabu.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo kusaidia suala hili. Kama alivyozungumza Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Ushirika na mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi ambao tumeteuliwa na Mhe. Rais kushirikiana na Mhe. Waziri kuhusu suala hili. Nadhani ni zuri kueleza labda juhudi tunazochukuwa anaweza Mhe. Hamza Hassan kidogo akatuelewa.

Mhe. Mwenyekiti, sisi bahati nzuri katika kulidhibiti suala hili tuliona kwa kuchukua jazba na hamasa hatutoliweza. Tulichokifanya tuliwaita viongozi wote wa Jeshi la Polisi, Mrajis wa Mahakama Kuu, Makamishna wa Polisi wa Mikoa, Katibu wa Mufti na viongozi wa dini zote za Kiislamu na Kikristo waliopo Zanzibar. Katika kuzungumza nao kwa kweli walitupa rai nzuri sana ya kulishughulikia suala hili. Kwa sababu ugumu wa suala hili Mhe.

Mwenyekiti, ni kwamba miongoni mwa hawa watu wanaofanya jambo hili ni watu wanaoheshimiwa sana katika jamii, wakiwemo walimu wa madrasa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa unaweza ukafikiria ni jambo rahisi labda mtu ambaye hajapelekwa mahakani ukamweka tu katika mnada ukamnadisha kama samaki, lakini sio rahisi lina ugumu wake, vyenginevyo baadae mnaweza kushtakiwa serikali mkalipa fidia kubwa sana ya kumdhalilisha mtu ambaye hajatiwa hatiani. Sasa Mhe. Mwenyekiti, suala hili kulichukua linataka hekima na mbinu kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikiri kwamba hili suala ni kubwa kuliko tunavyolielewa humu ndani, kwa sababu ukiangalia utafiti uliofanywa na *UNICEF*, basi hili suala ni kubwa mno na linatisha. Lakini mimi namuomba Mhe. Hamza Hassan Juma kidogo awe na subra, kwa sababu ile ripoti ambayo tumeipata kutokana na Masheikh, Katibu wa Mufti na Viongozi wa Kisheria ni lazima tuifanyie kazi vizuri na baadae nafikiri Mhe. Hamza Hassan matunda yake atayaona. Nafikiri Mhe. Mwenyekiti, nimesaidia kidogo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, bado Mhe. Hamza Hassan Juma namuomba afahamu kwamba kuna suala la utawala bora, hilo ni moja. Lakini pia kuna utaratibu wa kikatiba na sheria, hatuwezi kukiuka utaratibu wa kikatiba.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuje katika kifungu cha 12 cha katiba yetu ya Zanzibar tuliyoipitisha akiwa na yeye ni mjumbe, naomba nikisome. Kinasema.

Kifungu cha 12(6)(b)

> “kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria serikali itaweka taratibu zinazofaa na zitakazozingatia misingi kwamba mtu yeyote aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai hatotendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka atakapothibitika kwamba anayo hatia ya kutenda kosa hilo”.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hii ni katiba hatuwezi kwenda kinyume na katiba. Ndipo mimi nikasema kwamba hilo tunalofanya ni sawa sawa kwamba mtu anapokamatwa, huu utaratibu wote upite kwa mujibu wa katiba na pale tutakapomkuta na hatia basi tutamtangaza kwenye maredio, kwenye matelevisheni na kila sehemu. Lakini leo tukimshuku mtu na tukamtangaza halafu ikathibitika kwamba siye au ushahidi haupo na siye aliyetenda kosa, basi atadai fidia kwa serikali na fidia itakuwa kubwa, hatutaki twende huko, tunataka tufanye kitu kwa mujibu wa katiba na katiba ndiyo inayochukua nafasi hiyo. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, sheria tunatunga sisi, kuna wenzetu wanatafsiri sheria mahakama. Sasa sijui labda tuje tupate semina tena ya sheria. Kwa sababu mimi tatizo langu ni moja linakuja hapa. Hata huyo mtuhumiwa tunataka huyu mtuhumiwa wa kubaka mwanawe aonyeshwe.

Unajua Mhe. Mwenyekiti, ndio sawa sawa katiba, naijua na mimi tumeipitisha sote. Mhe. Mwenyekiti, katiba hii hii wale wanaoiba nazi na kuku inakuwa sio kuwa wakishaoneshwa katika TV ndio wameshafungwa hivyo, hapana. Kaiba nazi na kesi kesho inakwenda mahakamani. Sasa hizi sheria ziko vipi. Mimi nafikiria bado wanasheria nisaidieni. Tatizo langu mimi ni mkaidi sana, lakini nikishafahamu nakuwa mwalimu kwa wenzangu.

Mhe. Mwenyekiti, bado naona tunalionea haya hili suala na watoto wameshafika hali mbaya. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi ni hatari, kuna vijana sasa hivi. Mhe. Abubakar unaonesha hutembei tembei usiku, hebu tembea usiku. Siku hizi ile gari basi mtu anakusimamisha basi utaona labda anataka lift, yaani ukisimama basi keshafungua mlango keshaingia na kajaa tele, "nipelekeni hapo" (kwa sauti ya puani). Hii ni hatari Mhe. Mwenyekiti, yaani nchi imeshaharibika. Tunataka hatua za haraka ili kuokoa vizazi, tunataka kuokoa vizazi. Mhe. Mwenyekiti, hali imeshakuwa mbaya, nia yangu ni njema, wala sikusudii kupoteza muda. Mhe. Mwenyekiti, tunataka serikali iwasaidie watoto, tunamsaidia Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri, kuhusu takwimu ameshajitahidi, lakini vitendo hapa hatujaona kama hawa watuhumiwa watakuwa na hofu gani kuanzia tukitoka hapa ndani. Mhe. Mwenyekiti, hawa wanaonifanya niseme hivi ni wapigakura wangu, watoto wao wanaharibiwa ndio maana ninakuwa mkaidi nataka maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, sasa tumemfahamu Mhe. Hamza Hassan Juma anapoelekea, baada ya kutuelezea humo yanapotokea hayo matukio. Sasa kama alivyosema Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Mhe. Hamza Hassan yeye alikuwa waziri juzi na leo yeye ni mwakilishi ni lazima lazima taratibu kidogo tuzifuate.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosema kwamba kumtangaza mtu bila ya ushahidi moja kwa moja na wewe unaingia hatiani, akikushtaki je. Lakini sasa rai yake Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu Mhe. Hamza Hassan, keshatutajia mule ambapo wako hao watu na hao ambao yeye anawajua ndio wahujumu uchumi wakubwa na wazoefu wa hayo mambo.

Kwa hvyo, namuhakikishia Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba basi sisi kwa kushirikiana na uongozi wa wilaya na mikoa na serikali kuu pamoja na sisi tutazama *deep* pamoja sasa. Maana yake alivyotuelekeza tumeshamfahamu,

tunamshukuru kwa *in clue* yake, kwa vile tumeshaipata *in clue* yake basi tumeshajua sasa na sisi bunduki zetu tuelekee wapi, tutamkamata huyo anayemsema na hao wengine na tutawaonesha baada ya kuwatia hatiani.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, bora nitowe rai yangu sasa. Maana yake naona serikali hawajajipanga. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana wananchi wote wa Zanzibar sasa hivi, sisi tuko hapa kwa ajili yao. Watoto wanadhalilishwa sana, watoto wananyanyaswa sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kesi wakati mwengine mpaka zinapokwenda katika vyombo vya sheria huko, halafu zinaishia njiani watu wanachoka, nauli mtu hana, kila siku kwenda huku na huku. Serikali imeunda kamati yake Mhe. Mwenyekiti, na sisi *backbenchers* tutaunda kamati yetu. Tutaunda kamati yetu, sijui muongozo wa Mwanasheria atatuelekeza vipi. Mwenyekiti, kwa kawaida anachagua Spika, lakini kwa kuwa tumejichagua wenyewe, Mwenyekiti nitakuwa mwenyewe. Nitaandaa wajumbe ni lazima tufike hapa Mhe. Mwenyekiti, ili tuwasaidie hawa wanaopatwa na hizi kadhia ili kumaliza huu udhia. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri Baraza haliendeshwi hivi, Baraza linaendeshwa na utaratibu. Tumeshasema kwamba huu utaratibu ndio sheria inavyosema, huu ndio utaratibu katiba inavyosema. Sasa mwenzetu ambaye na yeye alishiriki katika kutunga katiba hii hataki. Sasa kama hataki alete mapendekezo ya kurekebisha hii katiba kwanza. Halafu hawezi tu kusimama akasema kwamba yeye ataunda kamati yake, kwa mamlaka gani aliyonayo, chini ya kanuni gani. Hatuwezi kwenda hivyo.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa muda tunao itabidi tuendelee, tumuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu atuongezee muda wa kuendelea.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu muda uliobaki kupitisha hoja ya makadirio ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto hautotosha. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likubali kutengua kanuni ya muda mpaka pale tutakapoweza kumaliza kupitisha hoja hii. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji kuhusiana na hoja hii ya Waziri. Wanaokubali. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan, nadhani maelezo ya kutosha yameshatolewa na Wanasheria yetu, kwa hivyo mimi nafikiria kwamba tuendelee kwa hili na baadae hatua bila shaka zinaweza zikachukuliwa ili kuhakikisha kwamba mtoto hatodhalilishwa kwa kiasi ambacho wewe umevyohisi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Sheria, alihoji kitu na kwa kuwa kahoji kitu ilikuwa lazima kwanza kijibiwe halafu tuendelee. Mimi nilikuwa nimeshasema tuendelee, lakini akajenga hoja. Sasa na mimi wacha nijibu hoja halafu baadae tutaendelea, sikusudii kupoteza muda.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako Mhe. Abubakar kaonesha katiba na mimi nilisema tulishiriki kikamilifu katika kupitisha katiba ile. Lakini mimi nilisema kwamba sisi wenyewe tutaunda kamati na kamati yetu sisi hatutounda humu Barazani. Ndio maana nikasema sisi tutajitolea, yaani wananchi tuwasaidie pale

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa hilo nafikiri ni nyinyi wenyewe nje sio hapa Barazani. Mheshimiwa amesema.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ndio, lakini sasa, nimekufahaku Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Mhe. Hamza, tunaendelea. Mhe. Mshimba.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi sikusudii kuzuwia kifungu hiki, lakini niweke Hansard vizuri kwa mama yangu. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipojibu suala lile la watoto la Forodhani, alijibu vizuri sana na nimpongeze kwa sababu katika mawaziri wote walioonesha jitihada ya kuleta waraka yeye ndiye wa kwanza katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kumuomba kidogo tu Mhe. Waziri ili niridhike na ule mkataba. Aidha, aniletee mimi mwenyewe mjumbe au anisomee ili wananchi wajuwe kwamba kweli lile suala mheshimiwa lilimtoka zamani, sasa

tutafute wizara husika wakati wa mbele ili tuweze kukamatana nayo. Naomba kujibiwa.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa hivi siwezi kuusoma mkataba. Kwa sababu nilitoa maelezo pale kwamba huu mkataba kuna matatizo, yaani kuna mambo ambayo bado yanaendelea kufanyiwa kazi. Sasa nitausoma vipi mbele ya hadhara hii leo hapa. Mimi naomba Mhe. Makame Mshimba aniamini kwamba mkataba upo, unafanyiwa kazi na ukishafanyiwa kazi tutauleta hapa na tutautangaza rasmi kwenu, tutatoa maelezo ya kutosha kwamba sasa hivi kwa nyumba ya Mazizini tumefikia hapa. Lakini kwa leo kuniambia niusome Mhe. Mjumbe naomba radhi sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, mimi naomba tu anitamkie kwamba huo kweli sio mkataba na hakuna maelewano yoyote.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, labda kwa kuongezea majibu ya Mhe. Waziri kama alivyotaka Mhe. Mshimba. Nadhani hilo tulilieleza wazi kwamba hii kazi tunaendelea kuifanya na kama mko kwenye kurekebisha na hamjaweka saini huo unakuwa sio mkataba. Kwa hivyo, na mimi nakubaliana naye kwamba mpaka sasa hakujakuwa na mkataba. Lakini kazi inaendelea kufanywa na kama alivyoahidi Mhe. Waziri huo utaratibu utafuata hapo mkataba utakapokamilika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, hili ndio Baraza la Umoja wa Kitaifa. Kwa hivyo, na mimi naungana na Mwanasheria Mkuu, siwezi nikamkiuka. Lakini kwa kumalizia naomba watoto warejeshwe Forodhani. Tuendelee.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	434,000,000
Kifungu 0501	Idara ya Wanawake na Watoto	116,000,000
Kifungu 0701	Idara ya Maendeleo ya Vijana	

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilitaka kujua kikamilifu kuhusu vijana hawa walioko kikundi hiki cha UVIKIUTA, ambao ni vijana waliokusanyika kutoka nchi mbali mbali. Tuwajuwe na tujuwe hiyo kazi wanayoifanya haina athari kwa vijana wetu kutokana na mila, desturi na utamaduni wetu, lakini sikupata jibu.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyokumbuka kwamba nilitoa maana ya UVIKIUTA, lakini kama mwenzangu Mhe. Mjumbe hakunisikia basi naomba

akubali nimuandikie vizuri, ile maana halisi hasa ya UVIKIUTA, halafu nimletee yeye pamoja na wajumbe wote niwape nakala, ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubali atuandikie ili wajumbe sote tujuwe. Lakini basiachwe kitu na ikiwezekana iwe kabla ya kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa. Tunaendelea.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia kwenye suala hili la ajira kwa vijana, nilisema kuwa kuna mahoteli sasa hivi. Hata nikatoa mfano wa Hoteli ya Going iliyokuwepo Kiwengwa, kuna kazi ambazo wanatakiwa wenyewe wananchi ili waweze kujiajiri na kupata fedha. Lakini sasa hivi wamechukuwa wazungu wanafanya hivyo na nilimtaka waziri amtume afisa wake ili aende akahakikishe na kuondolewa yule mtu mara moja ili wananchi waweze kujikimu wao wenyewe. Suala hili Mhe. Waziri hakunijibu, itakuwa kahafilika. Naomba jibu kwake.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mshimba arejee au akumbuke pale nilipofanya majumuisho ya wizara yangu. Suala la ajira kwa baadhi ya maeneo ambayo kwa mujibu wa sheria hawawajibiki wageni kufanya kazi. Nikachukua jukumu hapa kwamba wizara yangu italifuatilia suala hilo ili kuhakikisha kwamba yale maeneo yote ambayo wazalendo hawakupata fursa ile kisheria na wamepata wageni kinyume na utaratibu, basi tutahakikisha kwamba nafasi zile zichukuliwa na wazalendo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu mazuri Mhe. Waziri aniambie ni lini atakwenda katika hoteli ile, kwa sababu wananchi wamekaa tu pembezoni kule Kiwengwa na wanatutizama sisi hatuna cha kuwafanya. Sasa Mhe. Waziri ameeleza maneno mazuri, basi anihakikishie ni nini atakwenda na hao wataondolewa?

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, matatizo hayo yako katika maeneo mengi tu, tutajipanga na *Inshaallah* ikimalizika Ramadhani tutajipanga vizuri ili tuweze kwenda huko katika maeneo mbali mbali na tatizo hilo sio dogo kama tunavyoliona Mhe. Mwenyekiti. Ni tatizo kubwa na limegusa wananchi wenyewe. Tutajipanga vizuri, tumalize mwezi mtukufu wa Ramadhani *Inshaallah*. Hatukusudii kwamba mwezi wa Ramadhani hatufanyikazi, hapana, kwa sababu ni lazima tufanye utafiti wa kutosha na baadae tujuwe ni hoteli gani na hoteli na maeneo gani na gani, halafu baadae tukianza kazi. Kwa hivyo, kwa muda wa mwezi

mmoja huu wa Ramadhani tutakusanya takwimu zetu zote na kujua ni maeneo gani, tutakapokuja kuanza kazi basi tuanze kazi mara moja tukijaaliwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Sijakubali. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, ningojee mpaka mwezi wa Ramadhani, wakati huyu mwananchi anatafuta pesa kwa ramadhani ile kuweza kujisaidia na familia yake. Nimsubiri mpaka Ramadhani wakati maafisa wapo wengi tu, nikumtoa mtu tu aidha jioni au kesho na kwenda kuondoa tu mara moja. Yule mtu kaingia mule kwa mujibu sio wa kisheria.

Sasa kwa hivyo na wale wananchi wenyewe wameniambia wako wamekaa kama watoto yatima kule, nitawaambia nini wenyewe wananchi wa Kiwengwa. Naomba Mhe. Waziri aniambie ni lini, Ramadhani iko mbali.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachomuomba Mhe. Mshimba suala hili Mhe. Zaynab Mohammed sio lake. Sasa hivi tunajadili Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Naomba suala hili ilivyokuwa wizara yangu nilipoiwasilisha hapa niliitolea maelezo. Namuomba aje kesho afisini tutalimaliza.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, samahani sikumsikia vizuri Mhe. Waziri. Namuomba tena kidogo. Samahani sana.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, nimesema, suala hili halina uhusiano na wizara na inayohusiana na Mhe. Zaynab ni suala linalohusiana na Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Wakati nilipofanya majumuisho hayo nilieleza suala hilo.

Sasa Mhe. Makame Mshimba ili tuweze kuendelea na kwa sababu halimuhusu waziri anayehusika na masuala ya ajira katika sekta binafsi kama hizo. Nakuomba uje ofisini kesho *Inshaallah*. Tuna miadi kesho tutakutana, kwa hivyo njoo tutalizungumza na hilo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake, lakini hii ni wizara ya vijana na ajira na ukiniambia kama ni hivyo kuwa hahiusu kwa wizara ile basi hapo utanichanganya mimi. Lakini

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Makame Mshimba, suala hili halihusiani na ajira hili, inahusiana na vijana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Haya. Sasa ngoja basi.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Mhe. Mjumbe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ngoja basi, nazungumza masula ya vijana. Sijakuambia tuendelee Mhe. Mwenyekiti. Nakuambia sasa we tulia. Haya tunaendelea nitamfuata kesho asubuhi hakuna matatizo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu kifungu cha 96(6)(f) Mhe. Mwenyekiti, kifungu hicho kinasema kwamba

Kifungu cha 96(6)(f)

> "Maamrisho ya aya (e) yatatumika pia endapo mjumbe ametoa hoja ya kupunguza fungu kwenye kamati ya matumizi na endapo waziri anayehusika au Makamo wa Pili wa Rais anaweza kutoa ahadi ya kuondoa au kutekeleza jambo ambalo ni la msingi kwa hoja ya Mjumbe"

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee kwenye (g)

Kifungu 96(6)(g)

> "ikiwa baada ya hatua iliyoelezwa katika aya ya (f) haikukubaliwa na mjumbe na akashikilia hoja yake, basi kura itapigwa"

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba tuwape uhuru kwa sababu tunasema tunaongozwa kwa misingi ya katiba, sheria na kanuni zetu. Naomba tuwape uhuru ili mjumbe aridhike au tuende kwenye masuala ya kura. Ahsante.

Kifungu 0701	Idara ya Maendeleo ya Vijana	114,000,000
Kifungu	Idara ya Ustawi wa Jamii	

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilimuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho yake hapa anieleze kwa kina juu ya mambo mbali mbali kuhusu jengo lile linaloambiwa la *ZAYEDESA*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina hoja kidogo hapa juu ya jengo lile kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri, anasema kiwanja kile kilikuwa ni milki ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa hivyo, kikaondoshwa kupelekwa *ZAYEDESA*. Mimi ninavyofahamu hii *ZAYEDESA* sio taasisi ya serikali ni *NGO's*. Kwa hivyo, nilikuwa naomba ule utaratibu ambao ulitumika

kukihamisha kiwanja hiki kutoka mali ya serikali kwenda kwenye NGO, hilo moja.

Jambo la pili, ujenzi wa jengo lile kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri ulifanywa na wafadhili mbali mbali, lakini kwa jina la kuombea misaada kwamba wanajengewa watoto yatima. Je, kuna kikwazo gani sasa jengo lile kulikabidhi kwa watoto wale ikawa ni mali yao au ikawa ni mali ya serikali kwa ajili ya kulelea watoto wale.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimjibu Mhe. Mtando kwamba katika kutafuta ardhi ya kujenga kuna utaratibu wake ambao upo nchini na tuna utumia. Sasa inawezekana kiwanja kilikuwa cha so and so, lakini sasa hivi anataka hiki kiwanja so and so mwengine, basi wanakabidhiana kwa maandishi, ndio utaratibu wenyewe na hapa ndilo lililotumika hili. Watu walikabidhiana kwa maandishi. Ilimuradi ilikuwa tupate kile kiwanja *ZAYEDESA* wajenge nyumba ya kukaa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, bado hatujafikia makubaliano ya tuseme kama kuna mikataba na mambo mengine, lakini bado hatujafikia makubaliano, tukiwa tayari basi tutasema hapa Mhe. Mbarouk Wadi Mtando.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Naona Mhe. Waziri hajanijibu hata swali langu moja. Nilichouliza ni kuhusu utaratibu uliotumika katika kuhamisha mali hii ya serikali. Kile kiwanja kilikuwa ni cha Wizara ya Elimu na Wizara ya Elimu ni serikali, *ZAYEDESA* ni *NGO's* yaani ni taasisi binafsi.

Kwa hivyo, ninachouliza ni kuhusu utaratibu uliotumika ili kuhamisha mali ile ya serikali kuipeleka katika mikono mingine ambayo naweza kusema ni ya watu binafsi au *NGO's*, ndio huo utaratibu ambao nataka ulitumika pale.

Pili, ninachotaka, huu ujenzi ulisimamiwa na *ZAYEDESA*, lakini kwa ufadhili wa watu mbali mbali kama vile ambavyo maelezo tulipewa, lakini *ZAYEDESA* ilivyokuwa ikiomba misaada, ilikuwa ikiomba misaada kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha watoto yatima. Kwa hivyo, ilikuwa ni sawa sawa na mtu ambaye anaomba misaada kwa ajili ya ujenzi wa Msitiki ukimaliza unawakabidhi waumini wenyewe waendelee na kuswali. Sio lazima wewe uliyeomba ile misaada ndio uwe imamu. Kwa hivyo, ndio maana nilikuwa nahoji hapa, kwa nini sasa tunachelewa nini hawa *ZAYEDESA* wasiwakabidhi kile kituo wale watoto au wakaikabidhi serikali. Maana yeke nikisema wale watoto nakusudia serikali, ili serikali ikiendeleze kile kituo na itowe mkono wake pale. Hoja yangu iko hapo.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, wakati uli nilipokuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali *ZAYEDESA* walipoleta ombi lao la kiwanja kile kwamba wanaomba kwa ajili ya ujenzi wa taasisi hiyo au jengo hilo la Watoto Yatima.

Sasa ikiwa mwekezaji wa kigeni anakuja na kuwekeza kwenye ardhi na ardhi ni mali ya serikali popote pale ilipo Zanzibar na serikali inatoa. Kwa hivyo, kuna tatizo gani kwa *ZAYEDESA* taasisi yetu wenyewe Zanzibar kuipa ruhusa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tulichokifanya sisi tumepeleka Wizara ya Maji, Ujenzi Nishati na Ardhi wakati ule kwamba hatuna pingamizi kwa ardhi hiyo kutumika. Kwa kweli kama tulivyoiomba sisi wenyewe Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wakati tulipokuwa tunajenga jengo letu la Wizara ya Elimu tuliomba kuwa turuhusiwe kujenga jengo lile na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ikaturuhusu.

Sambamba na hilo tulitoa ardhi hiyo kwa Baraza la Mitihani wakati ule taasisi ambayo inajitegemea wenyewe Baraza la Mitihani, hivyo tukatoa ardhi ile. Sasa kwa vile walishindwa kuiendeleza basi serikali ikachukua wenyewe, kwa sababu ndio wenye ardhi na tukaikabidhi Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wakati ule. Kwa hivyo, taratibu zote zilifuatwa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ikatoa hati ambayo ipo na kukabidhiwa kwa jina la *ZAYEDESA*.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, labda kwa swali la pili alilouliza Mhe. Mjumbe nadhani tumelieleza vizuri, isipokuwa nimuongezee majibu tu. Kwa mujibu wa sheria hii inayoongoza *NGO's* ya mwaka 1995 ni kwamba mali ikeshakuwa ya *NGO's* kwanza haina maana ni mali ya mtu binafsi, hivyo hairuhusiwi mali ya *NGO's* na baadaye wakajiba wao wenyewe, kwa sababu inakuwa si ya kwao.

Mhe. Mwenyekiti, *NGO's* na wanachama, yaani ile ni mali ya umma inakuwa na ndio maana *NGO's* inapofungwa au inapovunjwa sheria inataka mali ile iende kwenye taasisi kama ile au inayofanana na ile kama hapana irudi serikalini.

Lakini haiwezekani na ninaomba niwatoe wasi wasi tusione kwamba *NGO's* hii inasimamiwa na fulani tukafikiri mali ile anaweza kuichukua na kuwa ya kwake binafsi, kwa mujibu wa sheria hili halikubaliki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, la pili kuhusu kukabidhi, nadhani pia tumelieleza wazi na sijui maelezo gani ya ziada. Kwa kweli tumelieleza haya makabidhiano ni

lazima yafanyike kwa maandishi. Sasa kwa sababu *ZAYEDESA* ndio walisimamia jambo hili, wanachotaka kuhakikishiwa na serikali ni kwamba itaendelea kuitunza, kuitumia kwa madhumuni ya lile jengo lenye limejengwa.

Kwa hivyo, hayo ni lazima yawekwe wazi ndani ya mkataba na yalikuwa hayajakaa wazi, ndio mambo tunayosema tukawashauri wenzetu hebu rudini mzungumze na *ZAYEDESA* na haya mambo tukubaliane na tutakapoyaweka kwenye mkataba basi yaonekane wazi.

Kwa maana hiyo, hakuna suala la kuficha au ghiba, yaani ni masuala yako wazi kwa sababu nia yao na ndio maana wameamua ile nyumba inatumika hata kabla ya huo mkataba wenyewe na kama nyumba ina mashaka hayo, basi wasingewaruhusu wale watoto kukaa. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuaminiane kama tumefika pahala hatuaminiani hilo ni suala jengine. Lakini mambo haya yanatayarishwa na *Inshaallah* yatakakamilika na sidhani kama yatachukua muda mrefu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nadhani kwa hapa umeridhika.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, bado sijaridhika na maelezo niliyopata. Kwa kweli maelezo yaliyotoka kwa Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu sijaridhika nayo naomba nipate ufafanuzi wa ziada katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu niliyoiuliza hapa ni utratibu ambao umetumika. Kwa hivyo, ningeomba ule utaratibu uliotumika kukitoa kiwanja kile kutoka mikono ya serikali na kukipelekwa kwenye *NGO's* na hiyo ndio hoja yangu niliyouliza na wala sijapata jawabu kuhusu hoja hiyo.

Pili maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu na mimi namheshimu sana Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, labda nikuulize hivi unaposema utaratibu, una maana utaratibu upi unaoutaka wewe zaidi ya huo Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ameshakueleza. Sasa ni utaratibu gani ambao wewe unautaka hebu tueleze. *(Makofi)*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kuna Sheria ya Uhaulishwaji ndio iliyofuatwa kwa hivyo nione *documents* ambazo zimepitia taratibu zote za uhaulishwaji wa kile kiwanja kutoka miliki ya serikali kwenda *NGO's* hiyo moja.

Pili utaratibu ambao Mhe. Mwanasheria Mkuu ameeleza mimi nashangaa kidogo kwamba kuweka mkataba Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto alitujibu katika Baraza lililopita, yaani liliulizwa suala hili juu ya mkataba na alisema mkataba uko kwa Mwanasheria Mkuu, lakini hautimii hata mwezi kikao kijacho nitakuleteeni na bahati nzuri leo tuko kwenye bajeti linarudi tena suala hili na bado mkataba ule haujawa tayari.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu pale ni kwamba kuna mambo yalikuwa yarekebishwa, sasa kwa nini yamechukua muda mrefu kiasi hichi, hakuna wanasheria wa kuweka hayo mambo yakaka sawa, kwa sababu naona ni kitu chepesi, lakini kimechukua muda mrefu. Kwa hivyo, naomba maelezo zaidi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa fusra hii, kwa kweli naomba sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba tuisome vizuri ile Sheria ya *Procurement* kabla ya kutoka hoja. Kwa kweli sheria ile ianzungumzia masuala ya manunuzi na mauzaji ya mali za serikali, lakini katika mazingira gani, mazingira yake ni ya kibiashara ndipo inapotumika Sheria ya *Procurement*. Kwa hivyo, naomba tuisome vizuri sana itatusaidia. *(Makofi)*

Kuhusu suala la uhaulishaji wa ardhi limeanza na msingi ile ulioelezwa ni kwamba ardhi yote ni mali ya serikali. Sasa serikali inapompa mtu inaweza ikarudi ikaichukue. Kwa mfano, tumechukua ardhi Mazizini kwa ajili ya kujengea afisi za serikali na wala hatukuinunua, isipokuwa imechukuliwa kwa taratibu kwa Sheria za Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inapotoa ardhi kumpa mtu mwengine hata kama imeshaandikwa kwenye serikali, basi kuna utaratibu wake, lakini inapoiuza kibiashara hapo ndipo linapokuja suala la Sheria ya *Procurement*, sasa hii haijauzwa kibiashara. Kwa kweli hii imetolewa kwa ajili ya *public use*, yaani haya ni matumizi ya umma tena ni matumizi mazuri kwa watoto wetu. Kwa hivyo, hii si biashara na Sheria ya *Procurement* haina nafasi.

Suala la muda kwa nini. Mhe. Mwenyekiti, nasema mnapofanya *negotiation* au mnapoelekezana na hili jambo haliko serikalini tu liko kwa *ZAYEDESA* ambayo ni taasisi binafsi. Kwa hivyo, wamepelekewa mapendekezo na wao wana muda wao pamoja na kazi zao, hivyo huwezi kuwaambia kuwa kesho tunawaka. Kwa kweli tunachoweza kuambiana ni kwamba jambo hili tuharakishe.

Mhe. Mwenyekiti, nasema msingi wa hili ni kuaminiana kama hatuaminiani kuwa hili linashughulikia hilo ni suala jengine. Lakini ninachoweza kusema mimi binafsi hiyo ndio taarifa niliyoipa, umekuja mkataba na nimepewa maelezo kwamba maelekezo yaliyotolewa ni haya, nadhani kwa nia njema.

Kwa hivyo, suala la kuchelewa kuwaweza kuna na sababu nyingi na wala siwezi kujua hasa ni sababu gani. Sasa ninachoweza kusema ucheleweshaji wowote si kwa nia mbaya wala ghiba ama kudanganya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakuomba uridhike na haya ambayo umeelezwa, ili tuendelee. Kwa kweli sifikiri kama mpaka hivi sasa kuna jengine ambalo utaweza kuambiwa ukaridhika kwa hapa. Kwa hivyo, nakuomba tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, wakati nipokuwa nikichangia nilimuomba Mhe. Waziri anipe maelezo huku wazee walioko Makundeni. Lakini kwa bahati mbaya Mhe. Waziri alisahau suala la wazee walioko Makundeni hakunijibu. Kwa hivyo, naomba anipe maelezo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nilisahau kidogo kuhusu wazee walioko Makundeni hivi sasa hawako kwetu sisi. Kwa hivyo, tunachofanya sisi tunawapa msaada wa shilingi 25,000/= kama tunavyowapa wazee kwa kuwasaidia na wale wako chini ya wilaya na mikoa hivi sasa na hawako katika wizara yetu. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Mhe. Waziri, nadhani wizara yake ndio inayoshughulikia masuala ya ustawi wa jamii. Sasa na wale ni jumla ya wazee tena ni wagonjwa, kwa sababu baada ya huu uzee ni wagonjwa na hali zao ni taabani. Kwa kweli wale tokea zamani serikali ilikuwa inaaenzi, kuwalea pamoja na kuwasaidia walikuwa na majumba na hospitali hivi sasa hazipo tena. *(Makofi)*

Sasa nilimtaka Mhe. Waziri anieleze kuhusu hawa wazee atawasaidia vipi na wala sina hoja ya kumpinga au nia ya kuzuia bajeti, isipokuwa nataka maelezo ya kwamba wazee wetu atawasaidia vipi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, Makundeni zamani ilikuwa Kambi kwa ajili ya Walemavu wa Ukoma. Kwa hivyo, hivi sasa Makundeni ni kijiji kwa ajili ya Walemavu wa ukoma, ndugu zao pamoja na watoto wao. *(Makofi)*

Kwa kweli pale hivi sasa kuna walemavu 32 waliobakia hai, lakini kijiji kina watu wengi zaidi ya hao na wale si wagonjwa ni walemavu kama walemavu wengine, ambao waliopata ulemavu kutokana na Ugonjwa wa Ukoma.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilifanyakazi na *Program* ya Kifua Kikuu na Ukoma mpaka mwaka 2006. Kwa kweli wale tunawashughulikia Wizara ya Afya mahitaji yao yote na watu wa Ustawi wa Jamii wanawashughulikia kwa kuwalipa pamoja na *NGO's* maalum ya Ulemavu wa Ukoma ambayo inaitwa *Tanzania Leprosy Association*.

Katika *NGO's* hiyo nilikuwa Katibu mpaka nilipochaguliwa kuwa Naibu Waziri wa wizara hii na bado tunaendelea kuwafanyiakazi na tunawapa miradi, tumewajenga nyumba, tumewatilia umeme wa *Solar Power* na wanaishi maisha yote, ambayo watu wengine wanaishi.

Kwa hivyo, kile ni kijiji na wala sio hospitali tena hospitali yao ya kawaida ipo ambayo wananchi wote pale wanahudhuria. Kwa hivyo, naomba tusiwahesabu hivyo kwamba ni wagonjwa ile ni jamii kama jamii nyengine na kile ni kijiji ambacho watu wanaishi maisha yao. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Kwanza naomba Mhe. Waziri kwa kuweka sawa …

Mhe. Omar Ali Shehe: Waheshimiwa bado mimi narudia turudie Kanuni kifungu 96 (6) (c). Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu kidogo.

> Kifungu cha 96 (6) (c) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi kinasema hivi:-
>
> > "Ikiwa baada ya Mjumbe kueleza nia yake na sababu zake za kutaka kutoa hoja hiyo, waziri anayehusika atashindwa kumtosheleza Mjumbe, basi Kiongozi wa shughuli za Serikali katika Baraza au waziri mwengine yeyote anaweza kutoa ufafanuzi zaidi dhidi ya sababu ya Mjumbe kutoa hoja hiyo."

Sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba *backbencher* tunapotaka kutoa hoja mawaziri ndio watujibu sio Manaibu Waziri.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba niweke sawa maelezo ya Mhe. Naibu Waziri ndio niendelee huko. Kwanza Mhe. Naibu Waziri anasema nimesema kama ile ni hospitali sio kijiji, lakini na mimi

sikumwambia kwamba ni hospitali nilimwambia kwamba ni kijiji kinachokaa wazee wetu ambao wanahitaji kusaidiwa na zamani serikali ilikuwa ikiwatunza.

Sasa ndio nimesema kwamba walikuwa na hospitali yao pale, walikuwa na nyuma pale, na hayo majumbe mengi yameshavunjika hayapo tena na ile hospitali iliyokuwepo haipo ndicho nilichozungumza sijasema ni hospitali. Lakini sasa nilitaka kujua kama wizara yake inawasaidia vipi, kwa sababu na wale ni jumla ya ustawi wa jamii waliomo ndani ya jamii ambao wanahitaji kusaidiwa.

Hapo alipoeleza Mhe. Naibu Waziri kwamba kuna wazee wa Welezo ni wazee kama wale. Ninavyojua mimi Welezo ni wazee kama wale ndio wanaosaidiwa kwa kupewa chakula, nguo, malazi na mambo mengine. Sasa nikataka kujua hawa wazee walioko Makundeni je wao hawasaidiwi kama hivyo kwa nini?

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema hivi, sikushindwa kujibu, nasema kila jambo lina mipaka yake. Mimi katika sehemu yangu ya kazi ya Ustawi wa Jamii kazi yangu kubwa ni kuwasaidia na kuwapa msaada wale wazee walioko Makundeni basi, lakini hawako ndani ya wizara.

Sasa wale ninavyokumbuka zamani walikuwa Wizara ya Afya na huko Wizara ya Afya nako waliachiwa tena wakaambiwa warudi majumbani mwao, lakini wakasema kwa sababu wako katika kile kijiji ambacho wameshakizowea basi wataendelea kukaa pale pale na kwa kweli wamezowea pale hawawezi kuhama. Lakini sisi kila mwisho wa mwezi tunawapa shilingi 25,000/-.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mhe. Waziri kuwa kanijibu majibu yaliyokuwa mazuri, lakini sasa wengine wanaipotosha hii hoja. Sasa hoja yangu nilikuwa nataka kujua kama hawa wazee mwenzangu mmoja alipochangia alisema, kuna wazee waliokuwa ni daraja ya kwanza na kuna wazee wa daraja ya pili? Kwa sababu wazee walioko Welezo ni sawa sawa na wale, sasa wale wa Welezo wanapewa chakula, malazi, nguo na shilingi elfu saba mwisho wa mwezi, sasa hawa wanapewa shilingi 25,000/- na hawa walioko kule ni bora matatizo kuliko hawa.

Kwa hivyo, nilitaka kujua kwa nini hawa hawapewi kama hawa waliokuwa hapa. Nataka Mhe. Waziri anambie atawasaidia vipi ili kuwatunza kama waliopo hapa ili wasibaguke kukawa na wazee wa daraja ya kwanza na wa daraja ya pili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Subeit ninavyofahamu mimi kwamba wale wazee wa Welezo kuna jumuiya ambayo inawasaidia. Sasa labda tumuombe Mhe. Waziri

watafute wafadhili wengine pamoja na *NGO's* ambazo zitaweza kusaidia huko unakokusema. Tumuombe Mhe. Waziri atufanyie hivyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Sawa tumuombe Mhe. Waziri awaombee mimi niko tayari.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tutatafuta wafadhili. *(Makofi)*

Kifungu 1101 Idara ya Ustawi wa Jamii

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi hii juu ya kutaka kupata ufafanuzi zaidi. Wakati nilipochangia katika kifungu hiki nilisema kuna wazee ambao kwa makusudi serikali inawasaidia wakiwa wale wanaopata welfare shilingi 5,000/= na wale walifanyakazi kwenye serikali kwa muda mrefu na kusataafu wengine wanapata shilingi 20,000/=.

Kwa hivyo, nikasema hakuna kutokana na maisha yalivyopanda wakasaidiwa wakapata kitu ambacho kinaweza kuwasaidia angalau kiwasaidia kwa mwezi.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa hivi sasa siwezi kutoa kauli ya kusema kwamba watapata nyongeza fulani, lakini hali ikiruhusu basi watasaidiwa. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Lakini nasisitiza hawa watu wamo katika hali ngumu sana kwa sababu shilingi 5,000/= au 20,000/= kwa mwezi hazisaidi mtu. Kwa hivyo, suala hili alipe mkazo wa hali ya juu tuone kuwa na wao wametizamwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, sawa tunaendelea.

Kifungu 1101	Idara ya Ustawi wa Jamii	438,000,000/=
Kifungu 1201	Idara ya Utumishi na Utawala	136,000,000/=
Jumla ya Fungu		**1,540,000,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0701	Idara ya Maendeleo ya Vijana	497,406,000/=
Jumla ya Fungu		**497,406,000/=**

(Kijifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya mwaka 2011/2012 ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshishima Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubali hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nachukua fursa hii kukushukuruni sana kwa utulivu pamoja na umahiri wenu na ninaamini kwamba, bajeti hii isingepita bila ya mabuti. Kwa hivyo, nakushukuruni sana na tukijaalia kesho tarehe 26/07/2011 tutakutana hapa saa 3:00 asubuhi.

(Saa 2:16 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 26/07/2011 saa 3:00 asubuhi)